
Nipashe
Jumatano Machi 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579858
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Hakimu aahirisha kesi mshtakiwa kuwa chakari

UKURASA 3


MAKALA: Marafiki Rwanda, Uganda wanavyotunishiana misuli

KIMATAIFA:

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Waziri Mkuu Netanyahu mtuhumiwa anayejiandaa uchaguzi mkuu Aprili

Msomi afunguka mambo 12 yanayohusu kuhama Lowassa

Wakuu imetosha, acheni kuwasukuma ndani raia

UKURASA 13

# Viongozi dini watoa tamko

• **Ni** kuhusu ulinzi kwa watoto, wakuu wa Bakwata, CCT, TEC waungana na kutaka usalama wao udumishwe... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**'WAFUNGWA, MAHABUSU 340 WANAISHI NA VVU'**

KATI ya wafungwa na mahabusu 15,250 nchini waliopima Virusi vya Ukimwi (VVU) kabla ya kuingia...

UKURASA WA 26

**MTUHUMIWA UJAMBAZI AJISALIMISHA POLISI**

EMANUEL Mwakilili, mkazi wa Dodoma aliyedai anajihusisha na vitendo vya uhalifu...

## Wagonjwa wajisaidia kwenye mifuko ya plastiki

UKURASA 3



Baadhi ya madiwani wa CCM, Jimbo la Magu mkoani Mwanza, wakizungumza na Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, walipomtembelea ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana. Madiwani hao walimwomba Lowassa kutembelea Jiji la Mwanza baada ya uamuzi wake wa kurejea chama tawala. **NA MPIGAPICHA WETU**



UK.2

## Kusuka, kunyoa rufani ya Mbowe

MICHEZO **AUSSEMS AJIAMINI SIMBA BILA OKWI** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Viongozi dini watoa tamko

**Na Gwamaka Alipipi**

VIONGOZI wa dini nchini wametoa tamko la pamoja la kukubaliana kuisaidia serikali kuhakikisha suala la ulinzi na usafi wa mazingira kwa watoto linatiliwa mkazo kutokana na madhara kuendelea kuwa makubwa nchini.

Viongozi hao wamekubaliana kwenda kuwahamasisha waumini kupitia mahubiri ili wafahamu umuhimu wa kulinda watoto na kuishi katika hali ya usafi wakati wote.

Tamko hilo lilitolewa na viongozi wa dini kutoka Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC), Baraza Kuu la Waislamu (Bakwata), Ofisi ya Mufti Zanzibar (MoZ) na Ofisi ya Mufti Tanzania Bara.

Viongozi hao ni Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabhi; Mwenyekiti wa CCT, Askofu Dk. Alinikisa Cheyo; Katibu Mkuu wa TEC, Dk. Charles Kitima na Mwenyekiti wa Muungano wa Taasisi za Dini unaoshughulikia Haki na Ulinzi kwa Watoto (TIAC), Sheikh Suleiman Lolila.

Kupitia muungano huo, viongozi hao walikubaliana kwa pamoja kufundisha, kuelekeza, kuhamasisha na kukuza Programu ya Maji, Usafi na Afya (Wash).

Akisoma tamko hilo kwa niaba ya viongozi wengine, Sheikh Lolila alisema asilimia nane ya vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, inatokana na maambukizi ya magonjwa kupitia maji.

"Sisi viongozi wa taasisi za dini katika muungano wetu, kwenye masuala ya kijamii tumekubaliana kwamba, suala hili la usafi wa mazingira kwa watoto tutilie mkazo kwa sababu lina madhara makubwa," alisema.

Sheikh Lolila aliongeza: "Tusipochukua hatua ya kutosha, watoto wetu wengi watapata matatizo ya kiafya na kudumaa katika makuzi yao.

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (kushoto), akiwaongoza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi walipowasili katika Gereza la Wanawake Kingolwira mkoani Morogoro, kuzungumza na wafungwa ikiwa ni ziara ya kufuatilia utekelezaji wa serikali. **PICHA: WMN**

# 'Sikwenda Lushoto kwa suala la shamba la Mnazi'

**Na Mwandishi Wetu,** MBOZI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbozi, mkoani Songwe, Kazimbaya Makwega, amesema hajapata mwaliko wa kwenda wilayani Lushoto kukutana na kamati iliyoundwa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mwita Waitara, kama ilivyodaiwa na baadhi ya vyombo vya habari.

Akizungumza na gazeti hili jana mjini hapa, Makwega alisema anasikitishwa na baadhi ya waandishi wanaotumiwa na watu 'aliowaita waharibifu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na Lushoto' kutumia vyombo vya habari kumchafua. Makwega alidaiwa kuitwa kwenda wilayani Lushoto kujibu tuhuma ya upotevu wa Sh. milioni 200 zilizotokana na uuzwaji wa shamba la Mkonge Mnazi.

Makwega alielezea kusikitishwa na habari hiyo na kuwa haina ukweli wowote bali zimekuwa na lengo la kumchafua kwa maslahi ya watu fulani waliokuwa na mzozo wao wa kisiasa.

INAENDELEA UK. 7

# Kusuka au kunyoa rufani ya Mbowe

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, imepanga kusikiliza leo rufani ya kutenguliwa dhamana ya Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, na mwenzake baada ya Mahakama ya Rufani kuagiza hivyo.

Mbali na Mbowe, mrufani mwingine katika kesi hiyo ni Mbunge wa Tarime Mjini kwa tiketi ya Chadema, Esther Matiko. Wote kwa pamoja wamekata rufani wakipinga kutenguliwa kwa dhamana yao na Hakimu Mkazi Mkuu, (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu) Wilbard Mashauri.

Mapema wiki iliyopita, Mahakama ya Rufani ilitupilia mbali rufani ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) ya kupinga Mbowe na mwenzake kusikilizwa na Mahakama Kuu.

Kwa mujibu wa chanzo cha Nipashe mahakamani hapo, rufani hiyo itasikilizwa saa 3:00 asubuhi mbele ya Jaji Sam Rumanyika.

Katika maombi yao, walalamikaji wanadai kwamba Mahakama ya Kisutu ilikosea kufuta dhamana kwa washtakiwa wakati wao wenyewe walifika mahakamani Novemba 12, 2018 na Novemba 23,2018 pia walihudhuria mahakamani siku dhamana yao ilipofutwa.

Sababu ya pili ya rufani yao, Mahakama ya Kisutu ilikosea kufuta dhamana kwa washtakiwa bila kuwapa wadhamini nafasi ya kuonyesha kwa nini dhamana yao isifutwe.

Kadhalika, Jaji Rumanyika alielekeza pande zote mbili kutoa hoja iwapo ilikuwa sawa kwa Mahakama ya Kisutu kuzingatia kiapo cha Wakili wa Serikali Zainab Mango kilichoambatana na kiapo cha aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Ilala, Salum Hamduni na kiapo cha Ofisa Uhamiaji Steven Mhina bila kuwapa washtakiwa nafasi ya kupeleka kiapo kinzani na kisha kutumia kiapo hicho katika uamuzi wa kufuta dhamana.

Hata hivyo, upande wa walalamikiwa ukiongozwa na jopo la Mawakili wa Serikali Wakuu, Dk. Mango, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, Wakili wa Serikali Wankyo Simon ulidai kuwa walalamikaji wamefungua maombi hayo bila kuambatanisha nakala ya mwenendo wa uamuzi wanaoukatia rufani kama matakwa ya kifungu cha 392 kidogo cha (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kinavyoelekeza.

Jaji alitupilia mbali pingamizi la walalamikiwa na kukubali kusikiliza rufani hiyo.

Pia alisema wakati wa usikilizwaji wa rufani hiyo atapenda kujua kama washtakiwa walipewa fursa ya kujibu kiapo cha Kamanda Hamduni.

INAENDELEA UK. 8


**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**CHRISTIANIA GROUP OF COMFTIN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 862 DHX EICHER STARLINE**. Chassis namba **MC2A3LRFOFJ324262.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ILA/TR/RB/1558/2019.**

115096102

**PASIPOTI IMEPOTEA**



**Faith Mikidadi Omar** anatangaza kupotelewa kwa pasipoti ya kusafiria yenye namba **TAE 065631,** Iliyotolewa tarehe 9 November 2018,,Dar es salaam,Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nae,Taarifa ya polisi **TAN/RB/136/2019**

215097002

**IN THE HIGH COURT FOR ZANZIBAR HOLDED AT VUGA**

**PETITION CASE NO. 01 YA 2019**

**PAULO SAMSON MAKOLEA............PETITION**

**Versus**

**ELIZABETH KIVILISHE MAHUMBILE...DEFENDANT**

**TANGAZO**

Mahakama Kuu Zanzibar inataka umtangazie mdaiwa ELIZABETH KIVISHILE MAHUMBILE popote alipo ahudhurie mbele ya Mahakama siku ya Jumatatu ya tarehe 25 ya mwezi wa Machi, 2019, kuja kusikiliza dai lililofunguliwa dhidi yake na mdai PAULO SAMSON MAKOLEA, asipofika Mahakamani, Mahakama itasikiliza kesi upande mmoja na kutoa maamuzi.

Imetiwa sahihi na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 Februari, 2019.

115096702

**IN THE REGIONAL COURT FOR ZANZIBAR HOLDED AT VUGA**

**CIVIL CASE NO. 01 YA 2019**

**SAID MOHAMED SAID...............PLAINTIFF**

**Versus**

**SAAD SULEIMAN SAID............DEFENDANT**

**TANGAZO**

Mahakama Kuu Zanzibar inataka umtangazie mdaiwa SAAD SULEIMAN SAID popote alipo ahudhurie mbele ya Mahakama siku ya Jumatatu ya tarehe 18 ya mwezi wa Machi, 2019, kuja kusikiliza dai lililofunguliwa dhidi yake na mdai SAID MOHEMED SAID, asipofika Mahakamani, Mahakama itasikiliza kesi upande mmoja na kutoa maamuzi.

Imetiwa sahihi na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 26 Februari, 2019.

115096802

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**THERESIA CORNEL SETEBE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 291 CMH X-TRAIL.** Chassis namba **NT30132061.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/01334/2018.**

115096202

## HABARI KITAIFA

# Kesi yaahirishwa kisa harufu ya pombe

**Na Jumbe Ismailly,** MANYONI

HAKIMU Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, Stela Kiama, ameahirisha kesi baada ya mmoja wa washtakiwa kwenye kesi ya wizi, kuingia mahakamani akiwa amelewa chakari.

Kesi hiyo ya wizi na kuharibu mali inayowakabili wakazi watatu wa tarafa ya Itigi, wilayani Manyoni, ilikuwa isikilizwe jana lakini ilishindikana kutokana na kisa hicho. Washtakiwa kwenye kesi hiyo ni Mussa Haruna (47), Yohana Simon (42) wote wakazi wa Mtimkavu na Joseph Alphonce (39) mkazi wa Mlowa.

Majira ya saa 7:30 mchana, Karani wa Mahakama aliwaita washtakiwa hao ili waingie ndani ya mahakama hiyo kwa ajili ya utetezi wao lakini walipoingia Hakimu alimshtukia mshtakiwa mmoja kwamba amelewa na hajiwezi.

Baada ya washtakiwa hao kuingia mahakamani hapo, Hakimu alihisi harufu kali ya pombe mahakamani na mahojiano kati ya Hakimu na mshtakiwa huyo yalikuwa kama ifuatavyo;-

**Hakimu:** Mshitakiwa namba mbili vipi mbona unapepesuka na unaonekana hauko sawa. Unaonekana kabisa umelewa pombe, hivi kweli utaweza kusikiliza kesi yako?

**Mshitakiwa:** Mheshimiwa Hakimu mbona mimi niko vizuri tu na wala si kama nimekunywa pombe leo (jana) asubuhi. Hizi ni za jana na nina uwezo wa kusikiliza kesi yangu bila tatizo lolote lile.

**Hakimu:** Hivi Mwendesha Mashtaka kama mimi tu niliyekaa mbali na mshtakiwa nasikia harufu kali kiasi hiki je, wewe ambaye uko karibu naye itakuwaje?

**Mwendesha Mashata:** Hata mimi Mheshimiwa Hakimu nasikia kabisa harufu ya kilevi alichokunywa mshitakiwa huyu na kwa kweli namwona hayuko 'serious' (makini) na kesi inayomkabili.

**Hakimu:** Hivi wewe mshitakiwa una uwezo wa kuendelea kusikiliza kesi yako au tuahirishe shauri lako mpaka siku nyingine utakapokuja ukiwa hujanywa mipombe yako?

**Mshitakiwa:** Mheshimiwa Hakimu nakuthibitishia kwamba nina uwezo kabisa wa kuendelea na shauri langu kwa sababu hizi pombe sijanywa leo (jana) asubuhi wakati nakuja mahakamani. Nilikunywa jana ingawa leo bado naonekana kama bado zipo kichwani.

**Hakimu:** Wewe mshtakiwa usipende kuwaudhi watu kwa mambo yako ya ajabu. Hivi unadhani sisi sote hatuna uwezo wa kufahamu mtu aliyekunywa kilevi na ambaye hajanywa kilevi?

**Mshitakiwa:** Si mheshimiwa Hakimu, mimi nakuruhusu uendelee kusikiliza shauri hili na mimi nitajitetea kwa kadiri ya uwezo wangu.

**Hakimu:** Mshitakiwa nakupa onyo mara ya mwisho na iwapo utarudia tena kutenda kosa kama hili nitakufutia dhamana yako ili upelekwe mahabusu ukajifunze zaidi kutii sheria za nchi. Utakapokaa gerezani ndipo akili yako itakuwa sawa maana hautapata muda wa kunywa mataputapu yako kama unavyofanya sasa na utakapokuja mahakamani utakuwa na uwezo wa kujitetea kama wengine. Usitake kutuchefua watu wengine huwa hatutaki kuongea sana na usidhani wewe ndiye una akili kupita watu wengine hapa mahakamani. Mimi naweza kukubadilikia muda si mrefu halafu usije kunilaumu.

INAENDELEA UK. 8

## Wagonjwa wajisaidia kwenye mifuko ya rambo

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

BAADHI ya wagonjwa wanaolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora na ndugu wanaokwenda kuwauguza, wako hatarini kupatwa na magonjwa ya kuambukiza kutokana na kujisaidia kwenye mifuko ya plastiki.

Watu hao wanatupa vinyesi hivyo kutokana na matundu ya vyoo wanayotumia kufungwa na ofisa afya baada ya kujaa.

Baadhi ya ndugu wanaowauguza ndugu zao waliolazwa katika wodi namba 3,6,8 na 9, Juma Jackson, Luciano Lazaro, Jilungano Jilelema na Amina Jeremiah, walisema wanaposhikwa haja kubwa nyakati za usiku wamekuwa wakijisaidia kwenye mifuko ya plastiki, maarufu kama 'Rambo' na kisha kinyesi hicho hukitupa kwenye nyasi.

"Kwa kweli si siri, tunalazimika kujisaidia kwenye mifuko ya rambo kwani inapofika nyakati za usiku tunapata shida sana kutokana na harufu kali inayotoka kwenye vyoo kwa sababu ya kujaa, ndiyo maana wataalamu wa afya wamefikia uamuzi wa kuvifunga," alisema Juma.

Pia waliweka wazi kwamba licha ya hospitali hiyo kukabiliwa na changamoto ya matundu ya vyoo, wanashangazwa pia kuona jirani ya majengo ya hospitali hiyo kumejengwa dampo la taka ambalo nalo limekuwa likitoa harufu kali licha ya baadhi ya viongozi wenye dhamana kupita katika eneo hilo na kuliona suala hilo kama ni la kawaida.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wamemwomba Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuitembelea wilaya ya Igunga ili kujionea adha wanayoipata wagonjwa wanaofuata huduma za matibabu pamoja na ndugu wanaokwenda kuwauguza.

INAENDELEA UK. 8




# Serikali kuboresha huduma magonjwa adimu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kuendelea kuboresha huduma kwa watu wenye magonjwa adimu (rare diseases), ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa dawa.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Magonjwa Adimu Duniani jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema serikali inatambua changamoto zinazowakabili watu wenye magonjwa hayo na kwamba imechukua hatua kuhakikisha inahuisha upatikanaji wa dawa zake ambazo ni adimu.

Alisema mchakato wa kuingiza dawa nchini huwa mrefu na kwamba magonjwa adimu husababisha changamoto ya kuwapo kwa mahitaji kidogo ya dawa husika.

Alisema serikali imeondoa kodi na malipo mengine kwa dawa hizo ili ziingizwe nchini bure.

"Kwa kawaida, kuna utaratibu mrefu wa kuingiza dawa nchini ambao unaongeza gharama pia. Sasa kwa mtu ambaye anataka kuingiza dawa za magonjwa adimu, ambazo unaweza kukuta zitatumiwa na watu 100 tu nchi nzima, kumwekea gharama, tunaona hatumtendei haki," alisema.

Dk. Ndugulile aliongeza: "Serikali imeondoa ushuru na malipo mengine kwa dawa hizi ili ziingie nchini bure. Serikali inatambua uwapo wa magonjwa haya ndani ya nchi na tunaendelea kuboresha mifumo yetu ya afya.

"Ziko changamoto za matibabu; kuna takribani magonjwa 6,000 ambayo ni magonjwa adimu na mengine hatuwezi kuyatibu. Kikubwa hapa ni kuhakikisha kwamba yule ambaye ameupata huo ugonjwa aweze kuwa na maisha bora yanayomsaidia kuendelea kuishi.

"Inapaswa mifumo nayo itambue kwamba huyu mtoto siyo kwamba anadeka au anauguaugua, ni lazima mifumo ielewe kwamba hawa wana mahitaji maalum," alisema.

Magonjwa adimu ni yale yanayowapata watu wachache kwenye jamii na wakai mwingine dawa zake huitwa dawa yatima kutokana na ugumu wa kuzipata.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kuna takribani magonjwa adimu 6,000 yanayowakumba watu takribani milioni 300 duniani kote. Magonjwa mengi adimu hutokea katika hatua za mwanzo za ukuaji wa mtoto na asilimia 30 ya wagonjwa hufariki dunia kabla ya kufikisha miaka mitano.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James (kulia), pamoja na Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk. Alex Mubiru, wakionyesha mkataba wa mkopo wa masharti nafuu baada ya kusaini katika ofisi za Hazina jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 600/- kupeleka lami Kigoma

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imepewa mkopo wa Sh. bilioni 589.2 na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ili kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 260 kutoka Kabingo hadi Manyovu mkoani Kigoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya kutia saini mikataba miwili inayohusina na mkopo huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema mkopo huo ni wa masharti nafuu na utatumika kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara hiyo itakayopita Kasulu na kuboresha miundombinu ya huduma za jamii.

Alisema benki hiyo imekuwa mshirika wa muda mrefu wa serikali katika maendeleo ya miundombinu na uwekezaji wenye ufanisi na matokeo ya kuridhisha.

James alisema utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya mkakati wa serikali ya awamu ya tano wa uimarishaji wa miundombinu ya usafirishaji ili kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kupunguza umaskini na kuimarisha ushirikiano wa kikanda.

Alisema barabara hiyo ni kiunganishi muhimu katika maendeleo na uboreshaji wa biashara ndani na nje ya nchi.

"Mradi wa ujenzi wa barabara hii utakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya Rumonge-Gitaza yenye urefu wa kilometa 45 nchini Burundi ili kuboresha mtandao wa barabara za Afrika Mashariki," James alisema.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa mradi huo kutaunganisha Bandari ya Dar es Salaam na mikoa ya Magharibi mwa Tanzania na kufungua masoko ya kikanda Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

James alisema mradi huo pia utachangia kupunguza gharama za uendeshaji magari na kuboresha usalama wa barabara, kupunguza gharama za usafirishaji na kuboresha upatikanaji wa miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi kwenye maeneo ya mradi.

"Kama mnavyoelewa, miundombinu ya hizi barabara ni mibovu, hivyo gharama za matengenezo ya magari zinakuwa kubwa, tunapokwenda kuweka lami, hizi barabara zitasaidia kupunguza gharama na hata ajali zitapungua," alisema.

James alisema mradi huo unatarajia kukamilika mwaka 2024 na kuifanya Tanzania kutokuwa na mkoa ambao barabara zake hazijaunganishwa kwa kiwango cha lami.

Meneja Mkazi wa AfDB, Allex Mubiru, alisema benki yake itaendelea kuisaidia Tanzania katika masuala mbalimbali ikiwamo miundombinu ili kupunguza umaskini.

# 'Wafungwa, mahabusu 340 wanaishi na VVU'

**Na Mwandishi Wetu**

KATI ya wafungwa na mahabusu 15,250 nchini waliopima Virusi vya Ukimwi (VVU) kabla ya kuingia gerezani mwaka jana, waliobainika kuwa na maambukizo ni 340.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa kuhusu hali ya maambukizo ya VVU na upatikanaji wa tiba ya magonjwa nyemelezi na udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya magerezani kwa mwaka uliopita.

Masauni alisoma taarifa hiyo ya hali ya mambukizi magerezani mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi iliyofika kwenye Gereza Kuu la Wanawake Kingolwira mkoani Morogoro.

Alisema upimaji huo ulifanyika kwa ushirikiano wa Jeshi la Magereza na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ambao ulilenga kutoa elimu ya upimaji kwenye magereza nchini.

Akisoma taarifa hiyo, Masauni alisema kuwa kati ya mahabusi na wafungwa 15,250 waliopima, wanaume waliokutwa na maambukizi ni 292 na wanawake ni 48.

"Wizara yangu kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Wizara ya Afya, wanahakikisha huduma za afya zinaboreka magerezani ikiwamo lishe nzuri kwa wanaothibitika wana maambukizo," alisema.

Alisema jumla ya wafungwa na mahabusu 1,496 wanatumia za kupunguza makali ya VVU (ARVs) wakiwa gerezani.

"Elimu ya kifua kikuu na upimaji pia inatolewa kila siku magerezani kwa wafungwa na mahabusu," Masauni alisema, "kwa mwaka jana, jumla ya waliopima ni 12,870 huku waliobainika kuwa na maambukizi wakiwa ni 167.

"Tunashirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) kuandaa Mpango Mkakati wa Ukimwi na kifua kikuu kwa miaka mitano."

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kuwatembelea wafungwa katika gereza hilo, wajumbe wa kamati hiyo, walilipongeza Jeshi la Magereza kwa kuwahudumia mahabusu na wafungwa wanaoishi na maambukizi magerezani.

Vilevile, wajumbe hao waliwaomba wafungwa wanaoishi na VVU kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao kuhusiana na maambukizi ya virusi hivyo.

Akizungumza mbele ya kamati hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Afya na Lishe wa Jeshi la Magereza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Dk. Hassan Mkwiche, alisema magereza yana utaratibu wa kupima afya za mahabusu au wafungwa siku ya kwanza tu anayoingia.

"Wakati wanaingia magerezani, mahabusi na wafungwa huwa wanapimwa ujauzito, Ukimwi, kifua kikuu na magonjwa mengine ili waweze kuhudumia kila mfungwa na mahitaji yake," alisema.

Aliongeza kuwa, mfungwa anapoingia gerezani, hukutana na kazi mbalimbali, hivyo ni muhimu kujua afya ya kila mmoja wao tangu siku ya kwanza anapoingia.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akisalimiana na wananchi wa Kilwa Kivinje baada ya kuwasikiliza wavuvi wa eneo hilo jana na kutangaza kuundwa kwa kanda kuu ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi Bahari ya Hindi. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Mpina aunda kanda mpya kulinda rasilimali uvuvi

**Na Mwandishi Maalum,** KILWA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametangaza kuundwa kwa kanda kuu mpya ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwenye Bahari ya Hindi ili kukabiliana na uvuvi haramu ulioshamiri kwa muda mrefu katika ukanda huo.

Alisisitiza kuwa Serikali ya awamu ya tano ina nia thabiti ya kulinda rasilimali hizo ili ziweze kulinufaisha taifa.

Waziri Mpina alitangaza uamuzi huo wakati akizungumza na wavuvi wilayani Kilwa, mkoani Lindi kuhusu juhudi zinazofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kulinda rasilimali hizo na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maombi ya wavuvi ikiwamo kuomba kuruhusiwa kutumia majenereta na taa za sola katika shughuli zao za uvuvi wawapo baharini baada ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 kukataza zana hizo.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na wavuvi katika maeneo ya Kivinje na Somanga, wilayani Kilwa, Waziri Mpina alisema, Serikali ya awamu ya tano, haina nia ya kumuonea mwananchi yeyote bali kinachofanyika ni kulinda rasilimali hizo kwa mujibu wa sheria ili ziwe endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

"Naomba niwaulize ndugu zangu wa Kilwa mtu anayekuja kulinda samaki na dagaa wasitoweke kwa kudhibiti uvuvi haramu na yule anayekuja na kuwaambia mtumie zana haramu na kesho samaki wote wakaisha nani mwenye uchungu na wananchi," alihoji.

Mpina alisema katika kuwasilikiza wavuvi nchini, serikali imeamua kuifumua Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 ili kuondoa maeneo ambayo yanakwaza shughuli za uvuvi ikiwamo kufuta vipengele vilivyokuwa vinalalamikiwa kwa muda mrefu.

"Nimekuja leo Kilwa kuwasilikiza mimi mwenyewe shida zenu, changamoto zenu na niwaambieni nimeamua kuifumua Sheria ya Uvuvi kama sehemu ya kuwasikiliza ili kuondoa maneno ambayo saa zingine yalikuwa yanakwaza shughuli zenyewe za uvuvi," alisema.

Hata hivyo, Waziri Mpina alikubali ombi hilo la wavuvi hao la kuomba kuhurusiwa kutumia taa za sola na majenereta.

Pia Waziri Mpina aliwaomba wavuvi kuwa na subira kuhusu ombi la kutaka kuruhusiwa kutumia nyavu za chini ya milimita nane, kwa kuwa sheria iliyopo ya uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni yake ya mwaka 2009, imeweka masharti ya kuzuia matumizi ya nyavu hizo kwenye ukanda wa bahari na kuwataka kuwa watulivu na kusubiri sheria hiyo ifanyiwe marekebisho

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai, alimshukuru Waziri Mpina kwa kutoa ufafanuzi utakaoondoa sintofahamu iliyokuwa imetanda miongoni mwa wavuvi wa wilaya huku akiwaomba kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali za kulinda rasilimali hizo za uvuvi.

Mmoja wa wavuvi wa Somanga Kilwa, Mohamed Kimbwembe, aliiomba radhi serikali ya awamu ya tano kutokana na wavuvi wengi kujihusisha na uvuvi haramu na kuua mazalia ya samaki na kwamba wengi walifanya hivyo baada ya serikali zilizopita kushindwa kuchukua hatua dhidi ya wahalifu hao.

Aliongeza kuwa mazoea hayo yalifanya wananchi waone kama wanaendelea vizuri kumbe walikuwa wanafanya mambo kinyume cha sheria za nchi.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, Hamida Abdala, alimshukuru Waziri Mpina kwa kuruhusu matumizi ya majenereta na taa za mwanga wa jua pamoja kuruhusu wavuvi kutumia leseni.

## Mbarawa azibana mamlaka za maji ukusanyaji mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ameziataka mamlaka za maji nchini kuongeza nguvu katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma.

Prof. Mbarawa aliyasema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akifungua kikao cha kujenga uelewa wa pamoja kuhusu uanzishwaji wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa).

Alisema suala la ukusanyaji wa mapato katika mamlaka mbalimbali za maji nchini limekuwa na changamoto mbalimbali hasa katika usimamizi.

Prof. Mbarawa alisema toka ameteuliwa kuongoza wizara hiyo pamekuwapo na mabadiliko katika maeneo mbalimbali katika kuongeza mapato katika mamlaka husika.

"Katika maeneo mbalimbali wakati naingia katika Wizara hii Julai, mwaka jana, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Dar es Saalam (Dawasa) ilikuwa inakusanya Sh. bilioni 8.5, Dodoma (Duwasa) ilikuwa inakusanya Sh. bilioni 1.2, lakini mwezi huu ulioisha wa Februari, imekusanya Sh. bilioni 1.85 na Moshi walikuwa wanakusanya Sh. milioni 600, lakini hivi sasa wanakusanya zaidi ya Sh. milioni 800," alisema Mbarawa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
04 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 12-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es -Salaam** kuelekea **Singida**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 135 CCP / T 161 BDU**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 28
Upana - mita 3.7
Kimo - mita 5.4

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Singida Kupitia Morogoro,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

XXXXXXXX



**SUMAJKT AUCTION MART**

**MNADA WA HADHARA**

**Suma Jkt Auction Mart** kwa idhini tuliyo pewa na **Tujijenge Tanzania Limited** tunatoa **notisi ya siku 14** kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa wadaiwa walio tajwa kwenye jedwali hapo chini mali zao zitauzwa katika mnada wa hadhara. Muda ni kuanzia saa nne asubuhi.

| no | JINA | MAHALI ZILIPO | DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Gration Grevas Kyaruzi | Buswelu - Mwanza | Nyumba | 26/03/2019 |
| 2 | Winifrida Gerald Musiba | Buswelu - Mwanza | Nyumba | 26/03/2019 |
| 3 | Festo Bazila Penuluzo | Buhongwa - Mwanza | Kiwanja | 27/03/2019 |
| 4 | Masagen'ghe Ndura Malongo | Sengerema– Mwanza. | Kiwanja | 29/03/2019 |

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mteja anatakiwa kulipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14
2) Endapo Mteja atashindwa kumalizia 75% ya salio lililobaki ndani ya siku 14 hatarudishiwa kiasi alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
3) Gharama zote za kubadili HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI.

Kwa mawasiliano zaidi piga namba: **0716004554 NA 0753063481**

215096002



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
05 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 13-03-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Tanga** kuelekea **Dar-Es-Salaam**, gari hizo zenye namba za usajili:

**T 316 CZS / T 969 CPS**

**T 257 BXH / T 310 DDH**

**T 863 BZM / T 974 CPS**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 20
Upana - mita 2.84
Kimo - mita 4.80

3. Njia itakayotumika: **Tanga hadi Dar-Es-Salaam Kupitia Chalinze,** gari zitasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

215096502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Operesheni kubaini wauaji watoto, vikongwe, wenye ualbino ilete tija

**KUIBUKA** kwa matukio ya mauaji ya watoto, wazee na watu wenye ulemavu wa ngozi katika maeneo mbalimbali nchini kumeleta hofu kubwa miongoni mwa jamii na kuamua kutafuta suluhisho la tatizo hilo kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi.

Hatua hiyo imechukuliwa mkoani Kigoma baada ya Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na chama cha waganga wa tiba asili na wakunga wa jadi wanaotetea watu wenye mazingira hatarishi nchini (ASIDEP), kukubaliana kuanza operesheni ya kubaini wahalifu hao. Kwa kauli moja waganga hao, wenyeviti wa serikali za mitaa na madiwani, wamekubaliana kuanzisha operesheni hiyo, itakayosaidia kuwasaka wanaoendesha vitendo hivyo na wananchi waendelee kuishi kwa amani.

Matukio ya mauaji mara nyingi yamekuwa yakihusishwa na imani za kishirikina kwa watu kudaiwa kutaka kujipatia utajiri.

Matukio hayo pia yanahusishwa na watu wanaotaka nafasi mbalimbali za uongozi maeneo ya kazi na shughuli za kisiasa.

Shutuma za mauaji hayo huelekezwa kwa waganga wa jadi ambao hudaiwa kuwashawishi wateja wao kutekeleza vitendo hivyo kwa lengo la kupata viungo vya binadamu kwa madai kuwa vikitengenezwa dawa, malengo yao yatafanikiwa.

Tukio la kusikitisha lililotokea siku za hivi karibuni mkoani Njombe la mauaji ya watoto, limehuzunisha Watanzania wengi huku wafanyabiashara mashuhuri wakikamatwa kwa kutuhumiwa kujihusisha na matukio hayo.

Wafanyabiashara hao wanatuhumiwa kutekeleza mauaji hayo kwa kuwakata waathiriwa viungo vya mwili kama macho, meno na kunyofoa sehemu zao za siri.

Katika maeneo mengine nchini mauaji hayo yamekuwa yakifanyika kwa kuwaua wazee wakiwatuhumu kufanya vitendo vya kichawi kutokana na mwonekano wao wa kuwa na macho mekundu. Vilevile mauaji hayo yanafanyika kwa watu wenye ulemavu wa ngozi (albino), ambao inadaiwa viungo vyao ni dawa ya kuongeza utajiri kwenye shughuli za uvuvi, uchimbaji madini na kupata vyeo sehemu za kazi.

Imani hizo potofu zimepoteza uhai wa maisha ya Watanzania wengi wasiokuwa na hatia kwa sababu tu ya tamaa ya utajiri wa watu wachache. Vitendo hivyo, vimedaiwa kufanyika kwa wahusika kushawishiwa na watu wanaojiita waganga wa jadi.

Ni jambo la faraja kusikia kuwa waganga wa jadi na serikali za mitaa wameamua kushirikiana na Jeshi la Polisi kuanzisha operesheni hiyo ili kuwatambua waganga wote na kukagua kazi zao. Operesheni hiyo imelenga kuwabaini waganga wanaovunja sheria kwa matumizi yasiyo halali ya tiba na matumizi ya nyara za serikali.

Chama cha ASIDEP kimebaini kuwa kuongezeka kwa vitendo hivyo vya mauaji ya watoto, wazee na wenye ulemavu wa ngozi, chanzo ni waganga feki. Hali hiyo imewafanya waganga wote wa jadi kuonekana wauaji na kuharibu taswira yao kwa jamii.

Hata hivyo, chama hicho kimelaumu kutengwa na baadhi ya idara za serikali kwa kuwaona kuwa waganga wote wa jadi ni wauaji badala ya kushirikiana nao kwa kuwaelimisha ikiwamo shughuli za ukunga ambazo huisaidia serikali maeneo ambayo hakuna vituo vya afya, kwa kuokoa maisha ya kinamama.


Wameishauri serikali kutoa elimu itakayowafikia watu wengi na kutambua umuhimu wao katika jamii badala ya kuwaona kuwa wote ni waovu. Mwamko huu ulioanzishwa na ASIDEP mkoani Kigoma, unapaswa kuigwa pia na mikoa mingine ambayo imeshamiri kwa vitendo hivyo ili wananchi wasiendelee kuishi kwa hofu na kuathiri shughuli zao za maendeleo.

Vyama hivi vinavyoanzishwa kwa lengo vya kusaidia jamii havina budi kushirikiana na vyombo vya dola katika kuleta matokeo chanya ya kukomesha vitendo vya uhalifu badala ya kuwa vichocheo vya kueneza vitendo hivyo.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**KUB ADILISHA TAREHE YA KUZALIWA**
**KATIKA MIFUMO YA KULA HELA ZA UMMA, KUNA MCHEZO WA KUBADILISHA TAREHE YA KUZALIWA KABLA YA KUSTAAFU ILI KUENDELEA KUFANYA KAZI. WANAAPA MAHAKAMANI WAKIENDELEA KUBAKI KAZINI KULA JAMBO LA WENGINE. HOJA HIYO!**
**NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

# Vijana, uchaguzi serikali za mitaa unawahusu

**AGOSTI** mwaka huu ni uchaguzi wa serikali za mitaa ambao unajenga msingi wa uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba mwakani. Watanzania wanalo jukumu la kuchagua viongozi kuanzia ngazi za vitongoji hadi taifa.

Katika uchaguzi wa serikali za mitaa viongozi watakaochaguliwa ni wenyeviti wa vijiji na vitongoji kwenye halmashauri za wilaya na wenyeviti wa mitaa kwa upande wa manispaa na majiji.

Kwa kipindi kirefu tangu kuanza kufanyika kwa uchaguzi huo wengi wanaochaguliwa kuongoza vijiji na mitaa ni wenye umri mkubwa. Ni kwa nadra kukuta vijana wanaaminiwa na kupewa nafasi ya kuongoza.

Ni ukweli kwamba vijana wengi hutumika kufanya kampeni kwa ajili ya wenye umri mkubwa au wazee kuingia madarakani na wakati mwingine, huwa nyuma yao kwa kuwapa mbinu na sera za kuwashawishi wapiga kura ili kuwawezesha kuibuka washindi.

Katika uchaguzi wa mwaka 2014 vijana wengi hasa wasomi walitoka kwenye maeneo waliyozaliwa kwa ajili ya elimu na kutafuta maisha na baadaye walirudi kwenye maeneo yao kwa ajili ya kuleta mabadiliko, waliingia kwenye kinyang'anyiro cha uongozi lakini kwa bahati mbaya walipigwa vita na kujiondoa.

Hali kadhalika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 vijana wengi walijitokeza kwenye vyama vyao kuwania nafasi mbalimbali kuanzia kata hadi taifa, lakini wengi wakiwa na ari ya mabadiliko kutoka hali iliyokuwapo kwenda kwenye hali nyingine ambayo ni kulibadili taifa.

Vijana wengi waliishia kuwa wapiga kampeni wa wazee badala ya kuingia kwenye ulingo na wazee kuwa wapanga mipango na waongoza njia, na mwisho wa siku wengi huishia kutumika kwa ajili ya kuwatengenezea njia wengine.

Kwa uchaguzi wa mwaka huu ni vyema kwenye ngazi za serikali za mitaa kukawa na damu mpya, yaani vijana. Ingefaa kama nao wanapewa fursa na vyama vyao kugombea nafasi hizo pasipo kuwazuia au kuwakatisha tamaa kuwa uongozi ni kazi isiyowastahili.

Yapo mambo kwenye ngazi za vijiji na serikali ambayo wakati mwingine yanahitaji vijana kushika nafasi hizo na kuyasimamia, wanahitaji kukimbizana huku na kule kusimamia uwajibikaji kwenye ngazi hiyo.

Wazee wanatakiwa kuendelea kuwapo kwa ajili ya kutoa busara na ushauri kwa viongozi, lakini kwa ujumla vijana wanahusika na ndiyo wadau katika kushika nafasi hizo ili wapeleke michango, akili na ubunifu wao kwenye uongozi wa serikali za mitaa na vijiji.

Kama ambavyo uchaguzi wa serikali za mitaa ulivyo msingi wa kujenga uchaguzi ujao ambao ndiyo mkuu unaoamua maisha ya Watanzania kwa miaka mitano ijayo, inatakiwa msingi imara kuhakikisha nyumba inayojengwa ni nzuri kwa maendeleo endelevu.

Malengo ya maendeleo endelevu (SDG's) yote yanawashirikisha vijana katika mipango yote ya maendeleo, kwamba unapotaka kupambana na umaskini, elimu bora, usafi wa mazingira, viwanda, miundombinu, usawa, demokrasia vyote hivyo vinawagusa vijana.

Kama dunia inatambua umuhimu wa vijana na kuwapa nafasi za uongozi na kufanya maamuzi, basi ni vyema wakapewa nafasi ya kugombea kwenye mitaa, vijiji na vitongoji ili waweze kuleta michango, mawazo na ubunifu unaohitajika.

Popote ambapo vijana wamepewa nafasi na mwongozo mahiri wamefanya mambo makubwa yenye mchango chanya kwa maendeleo ya taifa na kuleta mabadiliko kwenye maeneo waliyoyaongoza.

Mathalani, kwenye mitaa mingi zipo changamoto za wananchi hasa vijana kushiriki shughuli za maendeleo za kujitolea, naamini kwa kuwatumia vijana wataweza kuwaleta pamoja vijana na makundi yote na hivyo kushiriki shughuli za maendeleo.

Kwa umuhimu huo vijana wanapojitokeza kuomba idhini ya chama kugombea nafasi hizo wasipigwe vita bali waungwe mkono.

Na ikifikia mahali ikaonekana kwamba vijana bado hawajaiva basi washirikishwe hatua kwa hatua ili kuivishwa kwa kuwa viongozi huandaliwa, hufundishwa na kupewa mwelekeo.

Ni vyema vijana wakapewa agenda za makundi mbalimbali kwenda nazo kwenye uongozi, watakazozisukuma hadi Baraza la Maendeleo la Kata (WDC) na kwenye Baraza la Madiwani katika halmashauri.

HABARI KITAIFA

# ‘Sikwenda Lushoto kwa suala la shamba la Mnazi’

INATOKA UK. 2

“Sikwenda Lushoto kuitikia wito wa Naibu Waziri, hizo habari si za kweli, zenye lengo la kunichafua, wapo watu wanawatumia waandishi kwa maslahi yao na wengine wanatumia nafasi hiyo kwa ajili ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020,” alisema Makwega.

Hata hivyo, Makwega alikiri kuwa Februari 27, mwaka huu, alikwenda wilayani Lushoto kwenda kumkabidhi kwa mara ya pili ofisi Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Ikupa Mwasyoke, ambaye hakuwa tayari kulipa madeni yaliyoachwa na Makwega.

“Ni kweli nilikwenda Lushoto Jumatano iliyopita, lakini sikwenda kwa suala linalodaiwa, nilikwenda kukabidhi ofisi kwa mkurugenzi niliyemwachia ofisi tangu Agosti mwaka jana,” alisema.

Kuhusu madai ya shamba la Mnazi, Makwega alisema anaheshimu kauli ya Naibu Waziri aliyoitoa alipokuwa wilayani Lushoto kwa ziara ya kawaida na kwamba ataitikia wito endapo ataitwa ili aweze kutoa ufafanuzi wa namna matumizi hayo yalivyofanyika kwa kuhusisha Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati), akimsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, George Simbachawene (kushoto), wakati alipokuwa akiuliza masuala ya uzalishaji transfoma kiwanda cha Tanelec kwa Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Zahir Saleh (kulia mwa waziri), walichotembelea jana ili kujionea uzalishaji wake. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Mahakama yaamuru Malinzi, Mwesigwa kuhojiwa Takukuru

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeagiza mshtakiwa wa kwanza, Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na wa pili Mwesigwa Selestine kwenda kuhojiwa na Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Malinzi, Mwesigwa na wengine watatu wanakabiliwa na mashtaka 30 ikiwamo kula njama, kughushi na kutakatisha Dola za Marekani 173,335.

Kesi hiyo imepangwa kuendelea kusikilizwa Machi 19, mwaka huu mbele Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Hakimu alisema mahakama yake imeruhusu upande wa Jamhuri kwenda kuwahoji mshtakiwa wa kwanza na wa pili Machi 8, mwaka huu.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mwesigwa (46) ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa TFF, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga (27), Meneja wa Ofisi ya TFF, Miriam Zayumba na Karani wa TFF, Flora Rauya.

Washtakiwa hao Kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 30 katika kesi ya jinai namba 213 ya mwaka 2017 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha wa USD 173,335 na Sh 43,100,000.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wako rumande kwa kukabiliwa na mashtaka ya utakatishaji wa fedha kuwa miongoni mwa mashtaka ambayo kwa mujibu wa sheria hayana dhamana huku Zayumba na Frola wakiwa nje kwa dhamana.

# Bilioni 2.4/- kuendeleza miradi bunifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema iko kwenye mchakato wa kufadhili na kuendeleza miradi bunifu 47 yenye thamani ya Sh. bilioni 2.4.

Aidha, Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (Costech) kuacha utaratibu wa kusubiri wabunifu kuwafuata na badala yake iwafuate wabunifu waliko.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mashindano ya ubunifu katika sayansi na teknolojia yaliyoambatana na utoaji tuzo kwa washindi. Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo iko kwenye mchakato wa kufadhili miradi hiyo.

“Ni matumaini yangu kuwa itachangia maendeleo ya uchumi wa viwanda,” alisema.

Alisema serikali inaendelea kupeleka nguvu kwenye bunifu ambazo zinaweza kusaidia nchi kupiga hatua kimaendeleo.

“Ubunifu si chochote kama hausaidii kutatua changamoto na si chochote kama hauwezi kutumika la sivyo utakuwa unajifurahisha,” alisema.

Ole Nasha alisema wanapobuni wahakikishe ubunifu wao unaendana na uhalisia na kufanya utafiti kujua matatizo yanayowakabili wananchi.

Akizungumzia suala la Costech, Naibu Waziri huyo alisema utaratibu uliopo hivi sasa wa kila mbunifu kuandika barua ili kuomba kusaidiwa si mzuri.

Alisema si kila mbunifu anauwezo wa kuandika andiko kwenda katika tume hiyo kwa kuwa wapo wabunifu wazuri lakini hawana elimu ya juu.

“Unajua ubunifu ni jambo ambalo mtu anazaliwa nalo na siyo lazima uwe na elimu kubwa,” alisema.

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema mashindano hayo yameshirikisha wabunifu 60 ambao wametengeneza vitu mbalimbali kwenye sekta za kilimo, uvuvi, afya na zingine muhimu.




# Viongozi dini watoa tamko

INATOKA UK.2

"Tumekubaliana tufanye jitihada katika maeneo yetu ya ibada tuweze kuhamasisha waumini wetu waweze kufahamu umuhimu wa kuishi katika hali ya usafi wakati wote.

"Wakati umefika kutambua kwamba misikiti na makanisa inatumika kuzungumzia masuala haya ya usafi kwa sababu kazi yetu ya kitume, sisi Wakristo na Waislamu ni kuonyesha upendo, msaada na kujali, kutoa elimu na kutoa uelewa kwa jamii zinazotuzunguka."

Alisema wamekubaliana kuelimisha kuhusu masuala ya matumizi ya maji salama, utunzaji wa vyoo, kuhudumia watoto wa kike walio katika hedhi pamoja na kuisaidia serikali kuhamisha usafi wa mazingira.

Naibu Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (Unicef) ambaye pia anayeshughulikia Wash Tanzania, Rene van Dongen, alisema watoto wa Tanzania wanahitaji sauti za viongozi wa dini ili kuhakikisha wanakua na kufikia ustawi wao.

Alisema kuimarisha programu ya Wash kutasaidia kupambana na magonjwa yanayotokana na kuhara, kupunguza vifo vya watoto, kuongeza mahudhurio ya watoto shuleni, uboreshaji wa mazingira, kuondoa umaskini na njaa.

"Kutoimarisha programu ya Wash, kunaleta madhara kwa watoto wa kike hususani wanaoishi vijijini, watoto wenye ulemavu pamoja na wale wanaoishi katika mazingira magumu," Van Dongen alisema.

Aliongeza kuwa viongozi wa dini wana umuhimu na ushawishi mkubwa katika jamii, hivyo wana nafasi ya kuwaelimisha waumini wao kuhusu umuhimu wa programu hiyo.




Mrakibu msaidizi Idara ya Uhamiaji, Godfrey Silvanas (kushoto), akisalimiana na mkurugenzi wa kampuni Tanzu ya Labbaik travel & Travel kutoka Dubai, Nadhim Adam wakati wa uzinduzi wa safari za Hijja nchini jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja wa kampuni hiyo, Farid Abdallah Jabil. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kusuka au kunyoa rufani

INATOKA UK. 2

Kadhalika angependa kuelezwa kwamba masharti ya dhamana yaliyotolewa na mahakama kwa nini yalifuatiliwa na Jeshi la Polisi.

Novemba 23, mwaka jana, Mahakama ya Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mashauri iliwafutia dhamana Mbowe na Matiko baada ya kushindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yao ilipopangwa kati ya Novemba Mosi na 8.

Hakimu alisema Novemba Mosi, mdhamini wa Mbowe alidai mahakamani kwamba ameugua gafla yuko mahututi hawezi kuongea amepelekwa kutibiwa nje ya nchi.

Pia wakili wa utetezi, Peter Kibatala alidai kuwa mshtakiwa ni mgonjwa mahututi amepelekwa nchini Afrika ya Kusini.

Alisema Wakili wa Serikali Mkuu Faraja Nchimbi alipinga sababu zilizotolewa na utetezi na kuiomba mahakama kuamuru utetezi kuwasilisha vielelezo kuhusu maradhi ya Mbowe.

Mahakama iliamuru washtakiwa wakamatwe na kufikishwa mahakamani kujieleza kwanini wasifutiwe dhamana lakini Novemba 12, Mbowe na Matiko walijisalimisha mahakamani.

Mbowe wakati akijitetea ili asifutiwe dhamana alidai kuwa aliondoka nchini Oktob 28 mwaka huu kwenda nchini Marekani na alianza kuugua akiwa huko Oktoba 31, mwaka huu.

Alidai kuwa Novemba 2, alikwenda nchini Ubelgiji wakati akisubiri ahadi ya kuonana na daktari wake Novemba 8 na kwamba alishauriwa asisafiri mwendo mrefu akiwa angani.

Kwa upande wake, Matiko alidai kuwa alishindwa kufika mahakamani kwa sababu alihudhuria mkutano wa michezo kwa Mabunge ya Afrika Mashariki akiiwakilisha Tanzania.

"Nchi yetu inaendeshwa kwa matakwa ya sheria, pamoja na nyadhifa walizo nazo mshtakiwa wa kwanza na wa pili, wanakabiliwa na makosa ya jinai wanapaswa kutii amri za kisheria," alisema Hakimu na kuongeza:

"Kwa kuwa mshtakiwa wa kwanza taarifa zake zinakinzana, hati yake ya kusafiria inatofautiana na maelezo yake, mshtakiwa wa tano pia sababu zake hazina mashiko, mahakama yangu inawafutia dhamana kuanzia leo," alisema Hakimu Mashauri.

Katika kesi ya msingi, mbali na Mbowe na Matiko, wengine ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya; na Katibu Mkuu wa chadema, Dk. Vincent Mashinji.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, yakiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kushawishi utendaji wa kosa la jinai kati ya Februari Mosi na 16, mwaka jana jijini Dar es Salaam.

## Kesi yaahirishwa kisa harufu

INATOKA UK. 3

Baada ya mshitakiwa huyo kupewa onyo, Hakimu aliwauliza washtakiwa wengine kama watakuwa tayari kuendelea na kesi na walikubali.

Ingawa washtakiwa hao walimruhusu kuendelea, Hakimu aliposhauriana na mwendesha mashtaka, walikubaliana kuahirisha kesi hiyo hadi Machi 12, mwaka huu.

Ilidaiwa mahakamani kuwa Septemba 17, 2017 majira ya saa 3:00 asubuhi katika Kijiji cha Kitopeni, washitakiwa waliiba alama tano za barabarani zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 4.8.

Kesi hiyo iliyofunguliwa mwaka 2017 imefikia hatua ya washtakiwa kuwasilisha utetezi wao mbele ya mahakama pamoja na kupeleka mashahidi.

## Wagonjwa wajisaidia kwenye mifuko ya rambo

INATOKA UK. 3

Mzabuni wa usafi katika hospitali hiyo, Amina Ramadhani, alisema wafanyakazi wake wamekuwa wakikumbana na changamoto kubwa ya mifuko ya plastiki ikiwa na vinyesi wanapokuwa wakifanya usafi jambo ambalo alisema ni hatari kwa usalama wa afya zao.

Kaimu Ofisa Afya wa Wilaya ya Igunga, Andrew Ndomondo, alikiri kwamba vyoo hivyo vimefungwa ili kunusuru maisha ya wagonjwa waliolazwa pamoja na watu wengine wanaofika kwa ajili ya kufuata huduma za afya.

Ndomondo alisisitiza kwamba ni muda mrefu sasa tangu alipoiandikia mamlaka inayohusika barua ili kushughulikia matengenezo ya miundombinu ya kupitisha maji taka, lakini hadi sasa hakuna utekelezaji uliofanyika.

Alionya kuwa endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kutengeneza miundombinu hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa kutokea mlipuko wa magonjwa kutokana na vinyesi vinavyowekwa kwenye mifuko ya rambo na kutupwa ovyo kwenye manyasi yaliyopo ndani ya hospitali hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Igunga, Dk. Merchades Magongo, alisema zaidi ya Sh. milioni 3.5 zinahitajika kukamilisha matengenezo ya miundombinu ya majitaka kutokana na iliyopo kuwa chakavu. Alisema ni muda mrefu tangu ilipojengwa na kuahidi kuwa tayari wameshajipanga kutengeneza yote upya katika muda si mrefu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Igunga, Joseph Elias, alikiri kwamba jirani la majengo ya hospitali hiyo kuna dampo la uchafu na kwamba limekuwa kero kwa wagonjwa na wananchi wanaokwenda katika hospitali hiyo kutibiwa.

Hata hivyo, alisema wamejipanga kulihamisha dampo hilo huku akiwatahadharisha wananchi kutoendelea kutupa taka katika eneo hilo.

# Wajasiriamali Dar waipongeza TBS

**Na Elizabeth Zaya**

WAJASIRIAMALI wenye mashine za kusaga na kukoboa mahindi wameunga mkono utaratibu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) wa kuwafuata hadi ngazi ya chini na kuwapatia elimu kuhusu umuhimu wa unga wanaouzalisha kuwa na viwango ili kulinda afya za watumiaji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika mtaa wa Muungano, Manzese jijini Dar es Salaam juzi, wafanyabiashara hao walisema wamefarijika kuona maofisa wa shirika hilo wanawafuata na kuwapatia elimu.

Mjasiriamali Severine Thomas, alisema hatua hiyo inaonyesha TBS ilivyodhamiria kuwasaidia kuzalisha unga wenye viwango, hivyo hawana sababu ya kuogopa kutoa ushirikiano.

"Wenye mashine za kusaga mahindi tusiogope kutoa ushirikiano kwa sababu shirika hili linataka kutufikisha juu na hatimaye tukaweza kupata masoko nje ya nchi badala ya kutegemea wateja wa ndani peke yao," alisema Thomas.

Mfanyabiashara mwingine, Peter Swai, alisema elimu waliyoipata kutoka kwa maofisa wa shirika hilo itawasaidia kuzalisha unga wenye viwango hivyo kuhimili ushindani kwenye soko.

Kwa upande wake, Mkaguzi wa TBS, Baraka Mbajije, alisema ukaguzi wa bidhaa soko pamoja na kutoa elimu kwa wazalishaji kunalenga kuhakikisha bidhaa husika zikakidhi viwango.

Alisema mwishoni mwa wiki maofisa wa shirika hilo waliingia mitaani na kununua sampuli za unga kutoka kwenye mashine ili ukapimwe kwenye maabara kujua kama unakidhi matakwa ya kiwango TZS 328 cha mwaka 2016.

Alisema wameamua kununua sampuli za unga ili zikapimwe kwenye maabara baada ya kuwepo kwa madai mengi ya kutokidhi viwango, huku kikiwa ndicho chakula kinachotumiwa na Watanzania wengi.

"Kwa hiyo mbali na kununua sampuli kwa ajili ya kuzipima kwenye maabara zetu tunatoa elimu kwa wazalishaji namna bora ya ufungashaji wa bidhaa hiyo," alisema Mbajije.

Alifafanua kuwa Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 inaelekeza bidhaa zote zilizopo sokoni kutakiwa kukidhi viwango, hivyo wamekuwa wakifanya ukaguzi kwa wazalishaji na kwa wenye maduka nchi nzima.

Wakati huo huo, Mbajije aliwataka wajasiriamali wazalishaji wa unga kutumia fursa zinazotolewa na serikali kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha kwa lengo la kusaidia ukuaji wa uchumi.

Alisema serikali inagharamia upimaji wa bidhaa za wazalishaji na kupatiwa leseni ya kutumia alama ya ubora bure kwa miaka mitatu na baada ya hapo, ndipo wajasiriamali wanaanza kuchangia kidogo kidogo.

Alisema wanafanya hivyo kwa kutambua kwamba wajasiriamali ndilo kundi muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi, kupunguza umaskini na kutengeneza ajira kwa Watanzania.

# Waziri ahimiza usambazaji mbegu, pembejeo kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema uimarishaji wa mitandao ya usambazaji mbegu na viuatilifu ni muhimu katika kuhakikisha tija inaongezeka kwenye uzalishaji wa mazao nchini.

Hasunga alisema hayo jana wakati akizindua Mpango wa Kuimarisha Mitandao ya Usambazaji wa Mbegu na Viuatilifu, unaotekelezwa na mradi wa nafaka na kampuni ya kimataifa ya Corteva katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Katika hafla hiyo iliyofanyika jijini hapa, Hasunga alisema kuimarisha usambazaji mbegu na viuatilifu utamsaidia mkulima kuwa na uhakika wa chakula na kuongeza pato lake hivyo kusababisha Tanzania kufikia uchumi wa kati.

Alisema wakulima nchini wanategemea sekta ya kilimo kuchangia katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa kuwa inatoa ajira kwa asilimia 65 ya wananchi na ina uwezo wa kutoa malighafi ya viwanda kwa asilimia 66 pamoja na kuchangia asilimia 100 ya chakula kinachopatikana.

**Serikali inatambua mchango unaotolewa na Shirika la Misaada la Marekani (Usaid) katika miradi mbalimbali husasani katika sekta ya kilimo.**

Kwa mujibu wa Hasunga, kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hiyo, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya II (ASDP II) inayolenga kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo.

Programu hiyo ya miaka 10 imeanza kutekelezwa kuanzia mwaka jana, inafanyia kazi maeneo ya usimamizi endelevu wa ardhi na maji, kuongeza tija (kuongeza matumizi ya pembejeo), kuongeza masoko na kuongeza thamani ya mazao, kuboresha mazingira ya uwekezaji katika kilimo.

"Ni imani yangu kuwa kufanikiwa kwa kazi hii ya mradi wa Nafaka ni kufanikiwa katika utekelezaji wa sehemu ya ASDP II. Mradi huu pia utaendelea kuimarisha uhusiano uliopo baina ya serikali na sekta binafsi katika kuendeleza kilimo nchini," alisema.

Kadhalika, Hasunga alisema serikali inatambua mchango unaotolewa na Shirika la Misaada la Marekani (Usaid) katika miradi mbalimbali husasani katika sekta ya kilimo.

Mradi wa Nafaka ni moja ya michango ya Usaid katika kuongeza tija kupitia mashamba darasa, uendeshaji wa vikundi na vyama vya wakulima, kuongeza thamani kwenye usindikaji wa mahindi kwa njia ya virutubisho kwenye unga, kuunganisha wakulima na huduma za kifedha masoko na bima ya mazao.

Alisema shughuli hizo zinazotekelezwa na mradi wa Nafaka kwa kushirikiana na Corteva unaenda sambamba na jitihada za Wizara ya Kilimo katika kuendeleza kilimo.

Alisema moja ya maeneo ya kipaumbele yanayotekelezwa na wizara ni kuongeza tija katika uzalishaji kwa kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, na kuimarisha huduma za ugani.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akiwa na watoto baada ya kukabidhi kadi za bima ya afya (NHIF) za Toto Afya zilizodhaminiwa na benki ya Stanbic Tanzania kwa watoto wa kituo cha Hisani jijini Mwanza. Msaada huo ulitolewa na benki hiyo kwa watoto 105 wanaoishi katika mazingira magumu mkoani hapo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Maambukizi VVU Tanga yapanda maradufu

**Na Steven William,** MUHEZA

MAAMBUKIZI ya virusi vya Ukimwi katika mkoa wa Tanga yameongezeka kutoka asilimia 2.4 mpaka tano, jambo ambalo linaongeza wasiwasi kwa wakazi wa mkoa.

Hayo walibainika juzi katika kikao cha mkutano wa viongozi wa asasi zisizo za kiserikali zinazoshughulika na mapambano dhidi ya Ukimwi kilichofanyika mjini hapa na kusimamiwi na Progaramu ya Uimarishaji wa Mifumo ya Afya na Ustawi wa Jamii (CHSSP).

Mratibu wa Tume ya Taifa ya Ukimwi (Tacaids) Mkoa wa Tanga, Billingi Jemms, alisema takwimu za maambukizi ya Ukimwi kitaifa zinasema mkoa wa Tanga maambukizi ya Ukimwi yamepanda kwa kiasi hicho.

Alisema kuongezeka kwa maambukizi hayo inawezekana kuna sehemu wameteleza katika mikoa ya karibuni kwa wahusika kutokutoa elimu katika sehemu husika ambazo kuna mwingiliano mkubwa na wageni.

Mratibu huyo alisema katika mkoa wa Tanga maambukizi yameongezeka kwa kasi katika wilaya za Tanga, Muheza, Korogwe na Lushoto.

Naye Mratibu wa Ustawi na Ulinzi wa Mtoto, Elias Hackee, kutoka shirika la JSI Research and Training Inc, alisema mradi huo wameuleta wilayani Muheza kutekelezwa kwa mwaka mmoja kwa ajili ya kutoa elimu juu ya mambo mbalimbali ya maambukizi wa Ukimwi na ulinzi wa mtoto.

Alisema kuwa programu ya mradi huo inatekelezwa na JSI Research and Training Institute Inc. kwa kushirikiana na World Education Inc. chini ya ufadhili wa Usaid/Pepfar kuanzia Novemba 2014 mpaka Novemba 2020.

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni akidaiwa kumfungia mtoto kwenye banda la kuku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, linamshikilia mganga wa jadi Cesilia Gregory (36), wa kijiji cha Shunu, Kata ya Nyahanga, baada ya kugundulika kumfungia mtoto wa kiume mwenye umri kati ya miaka minne hadi mitano asiyefahamika jina wala wazazi wake, kwenye banda la kuku.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, SSP Lutusyo Mwakyusa, tukio hilo lilitokea Februari 26, mwaka huu.

**Polisi haiwezi kubaini wahalifu bila wananchi, miongoni mwenu hutoa dawa kwa wahali-**

Mwakyusa alisema mtoto huyo inasemekana alitelekezwa na watu wasiofahamika nyumbani kwa mganga huyo ili apatiwe matibabu.

Alisema, wakati amefungiwa kwenye banda hilo lisilofanyiwa usafi, alikutwa akiwa na afya mbaya na vidonda mdomoni hali inayoonyesha kuwa alikosa chakula na matibabu kwa muda mrefu.

Aidha, Mwakyusa alisema kuwa mtoto huyo anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, huku mtuhumiwa akishikiliwa na Jeshi la Polisi ili asaidie kuwapata wazazi wa mtoto huyo.

Kaimu Kamanda Mwakyusa, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa mapema kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ili kukomesha tabia hiyo.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali Simon Sirro, akiaga mwili wa Naibu Kamishna wa Jeshi la Polisi (DCP), marehemu Renatus Matanga Mbushi, katika Kanisa la Parokia ya Mt. Petro, Oysterbay jijini Dar es Salaam juzi. DCP Mbushi alifariki dunia Machi 03 mwaka huu mkoani Mbeya, akiwa katika ziara ya kikazi. Kulia ni Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# MUCE yatoa zana za kufundishia

**Na George Tarimo,** IRINGA

WALIMU wa shule za sekondari mkoani Iringa wameviomba vyuo vikuu mkoani humo kikiwamo Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), kuzisaidia shule za msingi na sekondari katika kuwaandaa vizuri wanafunzi kuendelea na elimu ya juu ili kuondoa malalamiko.

Ushauri huo ulitolewa katika makabidhiano ya zana za kufundishia kwa walimu wa shule za sekondari yaliyofanyika katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa mjini Iringa na baadhi ya walimu akiwamo Sunday Kivike, kusema uhusiano imara katika ya shule zao na vyuo vikuu unaweza kuwa chachu ya kuandaa wanafunzi walio bora na mwisho kuboresha elimu kwa ujumla.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo hicho, Dk. Evaristo Haule, alisema kwenye makabidhiano hayo kuwa MUCE kimekuwa na utaratibu wa kutoa zana za kufundishia kwa vitendo kwa shule za sekondari mkoani hapa kwa lengo la kuwasaidia walimu kupunguza changamoto za ukosefu wa zana hizo, huku wanafunzi nao wakisema zana hizo ni nyenzo muhimu katika kuwafanya wanafunzi kuelewa.

Haule alisema kuna kulaumiana, vyuo vikuu vikilaumu sekondari kwa kutoa wanafunzi walio chini ya viwango vya ufaulu na sekondari wanatupia lawama walimu wa shule za msingi.

Jumla ya shule 10 zimekabidhiwa zana hizo ambazo huandaliwa na walimu wanaohitimu chuoni hapo ikiwa ni sehemu ya mitihani ya mwisho kuhitimisha safari yao ya elimu chuoni hapo.

# Serikali yatenga magereza 10 kilimo mkakati

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI imetenga jumla ya magereza 10 kwa ajili ya kilimo cha mkakati ili kuzalisha chakula cha kutosha kuwahudumia wafungwa pamoja na ziada itakayosaidia kuiingizia serikali mapato.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alisema hayo jana wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Ukimwi ilipotembelea katika Gereza la Kingolwila, mkoani Morogoro.

Alisema hatua hiyo imechukuliwa baada ya Rais John Magufuli kushangazwa na Jeshi la Magereza kutegemea bajeti ya chakula kutoka nje, huku kukiwa na nguvu kazi kubwa ya wafungwa ambao wangetumika vizuri wangezalisha chakula cha kutosha.

Aliyataja magereza yaliyotengwa kuwa ni makubwa ya Kiberege na Idete mkoani Morogoro na katika kukabiliana na changamoto hiyo tayari zana za kilimo zimeanza kupatikana ikiwamo matrekta 10 ambayo yatasambazwa katika magereza yaliyotengwa.

Kamati hiyo imelenga kuangalia huduma za wafungwa wanaoishi na virusi vya Ukimwi pamoja na ugonjwa wa kifua kikuu (TB) huku mjumbe wa kamati hiyo, Suzan Lyimo, akiomba kufahamu wagonjwa wa TB wanavyopata huduma pindi wanapogundulika kuwa na virusi vya Ukimwi wakati wakiwa gerezani.

"Hapa mmetuambia waliobainika na TB ni 147 kwa kipindi cha mwaka 2017 na maambukizi ya Ukimwi yana uwiano mkubwa na TB sasa wanapokutwa na maambukizi ya virusi vya Ukimwi huwa wanatengwa au wanabakizwa na wafungwa wengine?" Alihoji.

Mkuu wa Idara ya Tiba na Lishe Jeshi la Magereza, Hassan Mkwiche, alisema wafungwa wanaobainika kuwa na virusi vya Ukimwi na kifua kikuu wametengewa vyumba vyao maalum kwa kupatiwa lishe bora.

Alisema, suala la unyanyapaa bado lipo na ndio tatizo linalokabili watumishi wa magereza licha ya kuwa hupata elimu kwenye vyuo na elimu wanapokuwa kazini, lakini ni wachache hujitokeza wanapokuwa na ugonjwa wa Ukimwi.

# Tanelec chaongeza uzalishaji wa transfoma

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imekipongeza kiwanda cha kuzalisha transfoma cha Tanelec kilichopo jijini hapa kwa kuongeza uzalishaji wa transfoma kutoka 7,000 hadi 14,000 kwa kipindi cha mwaka jana.

"Ongezeko hilo la transfoma ni kuunga mkono jitihada za serikali za kukuza uchumi wa nchi kufikia wakati kupitia sekta viwanda ambavyo vingi vinatumia umeme," Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani alisema wakati alipotembelea kiwanda hicho pamoja na Kamati ya Bunge ya Bajeti, jana.

Akitoa pongezi hizo mbele ya Kamati ya Bunge ya Bajeti, Waziri Dk. Kalemani, alisema uzalishaji huo unawezesha uanzishwaji wa viwanda na kuchangia kukuza ajira.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inawezesha viwanda vya ndani ili viweze kupiga hatua katika kufanikisha kufikia uchumi wa kati.

Dk. Kalemani alisema kiwanda hicho kwa kushirikiana na serikali kimefanya jitihada za kukifufua na kufanikisha uongezaji wa uzalishaji unapanda toka mwaka 2016 walipokuwa wakizalisha transfoma 7,000, mwaka 2017 hadi 10,000 na sasa 14,000.

Aidha, alisema kuimarika kwa kiwanda hicho ni msimamo wa Rais John Magufuli wa kutaka Watanzania kujenga utamaduni wa kupenda vitu vinavyozalishwa nchini kumesaidia kuepuka gharama iliyokuwa ikitokana na uagizaji transfoma nje ya nchi.

Aidha, alisema kufikia kwa hatua hiyo kumeleta maumivu makubwa kwa baadhi ya wafanyabiashara ambao walikuwa wakinufaika na uagizaji transfoma hizo nje ya nchi.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, George Simbachawene, aliahidi kumpa ushirikiano Waziri Kalemani kwa kulisimamia suala hilo ili kukipa nguvu zaidi kiwanda hicho na vingine nchini.

## Taasisi yaomba utafiti uwafikie walengwa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania, (TARI), imevitaka vituo vya utafiti kuhakikisha matokeo ya utafiti wa teknolojia wanaofanya unawafikia walengwa ili utatue changamoto zinazowakabili.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. Geoffrey Mkamilo, wakati akizungumza na wafanyakazi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Mboga na Matunda, (Horti) Tengeru, ikiwa ni sehemu ya kutambulisha taasisi hiyo.

Alisema kituo hicho kimepewa jukumu la kitaifa la kuhakikisha teknolojia zote za matunda na mboga zinazogundulika kituoni hapo zinawafikia walengwa kwa wakati na kuleta matokeo chanya kwa wakulima, kwa kuwa wengi wao hawajafikiwa na teknolojia hizo ambazo zinaweza kuleta matokeo mazuri kwa wakulima.

Dk. Mkamilo alisema lengo la serikali ni kutaka kuona teknolojia zote zinazogundulika na kufanyiwa utafiti zinaleta matokeo mazuri kwa walengwa na kutatua changamoto mbalimbali, hivyo kuhakikisha wanaongeza bidii katika kufanya tafiti na kuja na mazao ambayo yatabadilisha maisha ya wakulima hao.

Aidha, Dk. Mkamilo alivitaka vituo mbalimbali vya utafiti kuhakikisha vinaongeza bidii na kuwa na uwezo wa kuzalisha mbegu chotara kutokana na mbegu hizo kuwa na uwezo wa kuzalisha kwa wingi.

Alisema kwa muda mrefu mbegu hizo zimekuwa zikizalishwa nje ya nchi tu, hivyo ni lazima wajiongeze ili ziweze kupatikana hapa hapa Tanzania.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya TARI, Dk. Yohana Budeba, alisema kituo hicho kina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kinabadilisha maisha ya wakulima wa mboga na matunda kwa kupeleka teknolojia mpya zilizofanyiwa tafiti na kuweza kuzisambaza kwa wakulima hao ili wazitumie.

Alisema umefika wakati wa vituo vya utafiti kufanya kazi zenye faida na hii nchi ambazo zitaleta mabadiliko makubwa na kutatua changamoto za wakulima kupitia tafiti hizo.

"Tunataka kuona kituo hiki kinafanya utafiti na kuja na mbegu mpya za matunda na mboga ambazo zitapelekwa kwa wananchi na kuchochea kasi ya maendeleo, kila siku tunataka kuona mnakuja na kitu kipya sio kufanya utafiti tu, badala yake utafiti huo ulete matokeo chanya kwa walengwa," alisema.

# Wapiga kambi kueneza teknolojia ya kutibu maji

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WATAALAMU wa utafiti na teknolojia ya kutibu maji kwa kutumia nyuzi za pamba kutoka Chuo Kikuu cha Shinshu, Japan, wapo Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, kuhawilisha teknolojia ya kutibu maji kwa kuondoa kiwango kikubwa cha madini ya fluoride.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Sayansi na Teknolojia, Yoshiko Shirokizwa, ambaye ni mtaalamu wa masuala ya utafiti kutoka chuo hicho, alisema teknolojia hiyo, itatumia nyuzi za pamba na malighafi ambazo zinapatikana hapa nchini.

Akizungumza katika mdahalo wa wadau wa sekta ya maji uliofanyika Jijini Arusha jana, Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema hali ya upatikanaji wa maji kwa Mkoa wa Arusha inakabiliwa na changamoto ya madini ya fluoride.

Alisema licha ya serikali kusambaza maji vijijini kwa asilimia 63, kuna baadhi ya maeneo bado yanakabiliwa na changamoto kubwa ya kiwango cha madini ya fluoride kwenye maji ambayo yanatumika kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

**Wataalamu kutoka Japan wameelezea aina tofauti za teknolojia ya kutibu maji na kuondoa madini yote yasiyo rafiki kwenye maji, ikiwamo madini hatari ya fluoride na teknolojia hii itatumia malighafi zilizopo hapa nchini.**

Kwitege alisema takwimu zinaonyesha takribani asilimia 42 ya vyanzo vya maji katika Mikoa ya Arusha, Shinyanga, Singida na Manyara imeathiriwa na uwepo wa madini ya fluoride iliyozidi ikilinganishwa na kiwango cha miligramu 1.5, kwa lita moja ya maji, kiwango ambacho kimetolewa na Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa, (WHO), kwa matumizi ya kawaida ya binadamu.

Aliongeza kuwa kutokana na takwimu hizo, miradi mingi ya maji inayoendelea kujengwa mijini na vijijini katika Mkoa wa Arusha, inahitaji mifumo na miundombinu bora na rahisi ya kutibu maji kwa ajili ya kuondoa fluoride kwenye maji kwa usalama wa afya za wananchi.

"Wataalamu kutoka Japan wameelezea aina tofauti za teknolojia ya kutibu maji na kuondoa madini yote yasiyo rafiki kwenye maji, ikiwamo madini hatari ya fluoride na teknolojia hii itatumia malighafi zilizopo hapa nchini," alisema Kwitega.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Wilson Mahera, alisema kuna haja kubwa katika halmashauri hiyo, kupata teknolojia ya kuondoa madini ya fluoride kwenye maji hususan katika Kijiji cha Lemanda kilichopo Kata ya Oldonyosambu.

Aidha, Dk. Mahera, aliongeza teknolojia hiyo, ina uwezo mzuri wa kutibu maji japo kuwa bado uwezo wake wa kutibu maji ni kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya wananchi.

Alishauri wataalamu hao, washirikiane na kituo cha utafiti cha hapa nchini ili tafiti zisaidie kupata njia mbadala wa kutatua changamoto hiyo.

Aliwataka watafiti hao kutoa mafunzo zaidi kwa wadau na wataalamu wa maji wa nchini juu ya uendeshaji wa teknolojia hiyo ili waifahamu zaidi.

Akizungumza katika hafla ya kusimika mtambo maalumu wa kupunguza madini ya fluoride katika kijiji cha Lemanda, ambao ulitolewa na kampuni ya O2 and B "Capacity of Deionization System," (CDI), Desemba 2018, Msimamizi Mkuu wa Maabara ya Ubora wa Maji Mkoa wa Arusha, Jovitus Kichumu, alisema kiwango cha madini ya fluoride kwenye maji katika eneo hilo, ni miligramu 18.7 kwa lita moja, kiwango ambacho ni kikubwa na kisichofaa kwa matumizi ya binadamu.

Alisema mtambo huo una uwezo wa kuchuja maji na kupunguza kiwango cha fluoride kutoka miligramu 18.7 kwa lita moja hadi kufikia miligramu 0.37 kwa lita moja.



Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara, Martha Umbullah (CCM), akiishukuru serikali kwa kuwajali wananchi wa Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro katika sekta ya afya juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mbunge Gekul ataka shule ipokonywe fedha

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

MBUNGE wa Jimbo la Babati Mjini, Pauline Gekul (CCM), ameiomba serikali kutoa Sh. milioni 37 ilizotoa kwa Shule ya Sekondari ya Kwaraa na kuzihamishia shule mpya ya Hangoni.

Alisema hayo kwenye mkutano wa wazazi na walezi wa wanafunzi wa shule mpya ya sekondari ya Hangoni mjini Babati jana.

Alisema hivi karibuni serikali imeipatia Halmashauri ya Mji wa Babati Sh. milioni 437 kwa ajili ya maboresho ya shule 10 za sekondari, huku Shule ya Sekondari Kwaraa nayo ikipatiwa Sh. milioni 10.

Alisema japokuwa Shule ya Sekondari ya Hangoni, nayo imepatiwa Sh. milioni 10, lakini Shule ya Kwaraa ingenyang'anywa fedha hizo na kupatiwa Hangoni yenye changamoto ya miundombinu.

"Hii shule ya Kwaraa kwenye matokeo ya kidato cha nne ilikuwa ya mwisho na kupitwa na shule ya Sigino ambayo wanafunzi wanatoka mbali kule Imbiriri na Shule ya Mutuka watoto wanatoka milimani," alisema.

Alisema Shule ya Sekondari Hangoni bado ina changamoto ya madarasa mengine kutomalizika pia watoto wanatoka mbali ili kufika shuleni, hivyo fedha hizo zitasaidia kumaliza tatizo hilo.

"Wananchi wengine wa eneo la Shule ya Sekondari Kwaraa msinielewe vibaya kwenye suala hilo kwa kuwa zote ni shule zetu ila Hangoni ina changamoto nyingi," alisema.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari Hangoni walipongeza jitihada za Gekul katika kuipa kipaumbele shule yao.

Mmoja kati ya wanafunzi wa shule hiyo, Zulfa Hussein, alisema wanatoa ahadi ya kuzingatia masomo ili waweze kulipa fadhila za mbunge wao anayewatetea.

Hamis Juma alisema shule hiyo ina changamoto nyingi, hivyo wanamshukuru mbunge wao kwa kuwapa kipaumbele na kuwasemea kwenye sehemu husika.

# Mwanafunzi chuo akutwa amefariki amepiga magoti

**Na Paul William,** ROMBO

MWANAFUNZI wa kozi ya utawala katika Chuo cha Kilacha kilichopo Wilaya ya Rombo, Godwin Firimin (24) ,amekutwa amefariki dunia, akiwa amepiga magoti chini ya shina la mti.

Firimini inaelezwa kuwa alitoweka nyumbani kwao kijiji cha Kisale, tangu Januari 24, mwaka huu na taarifa za kupotea kwake ziliripotiwa na wazazi wake katika kituo cha polisi Rombo.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Hamisi Issah, akizungumzia tukio hilo alisema mwanafunzi huyo alipatikana akiwa tayari amekufa Machi 3, mwaka huu, ndani ya msitu wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, upande wa kijiji cha Katangara.

**Mwili wa mwanafunzi huyo umehifadhiwa katika Hospitali Teule ya Misheni ya Huruma ya Wilaya ya Rombo, ukisubiri kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu.**

"Inasemekana marehemu Godwin alitoweka nyumbani kwao tangu Januari 24 na taarifa zilitolewa katika kituo cha polisi na jitihada za kuendelea kumtafuta zilifanyika hadi alipopatikana juzi jioni msituni akiwa tayari amepoteza maisha," alisema.

Mwili wake uligunduliwa na kinamama waliokuwa wakiokota kuni katika msitu huo ambao walikimbia na kwenda kutoa taarifa zilizosaidia kutambuliwa kwa mwanafunzi huyo na wazazi wake.

Habari zaidi zinaeleza kuwa, mwanafunzi huyo alitambuliwa na wazazi wake kutokana na mavazi aliyokuwa amevaa wakati anaondoka nyumbani akiwa amebeba kitabu kitakatifu cha 'Biblia' na vyote amekutwa navyo.

Mwili wa mwanafunzi huyo umehifadhiwa katika Hospitali Teule ya Misheni ya Huruma ya Wilaya ya Rombo, ukisubiri kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu.

Katika tukio lingine, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Reginald Mengi iliyopo katika Manispaa ya Moshi, Joyce Majali (16) mkazi wa Newland, amefariki dunia baada ya kuanguka ghafla akiwa shuleni anaokota takataka.

Kwa mujibu wa kamanda Issah, taarifa za uchunguzi wa awali za kitabibu zinaonyesha kuwa mwanafunzi huyo alikuwa na tatizo la upungufu wa damu mwilini.



Mkazi wa eneo la Jangwani akivuka maji yaliyojaa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini wakati akitokea katika makazi yake jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Wahamasishwa kulima zao la fiwi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WAKATI wakulima wa Mkoa wa Kilimanjaro wakiwa bado hawaelewi ni zao gani la biashara la kulima ambalo lina soko la uhakika baada ya kahawa na vanilla, watafiti wa mazao wameanza kuhamisha wananchi wa Wilaya za Same, Mwanga, Moshi na Hai kulima zao la fiwi.

Akitoa mrejesho kuhusu utafiti uliofanyika, baada ya kutoa matokeo chanya kwa wakulima wa Kijiji cha Mabilioni katika Wilaya ya Same, mtafiti mwandamizi wa mazao yanayovumilia ukame na mbegu bora nchini, Dk. Mary Mgonja, alisema zao hilo lina mafanikio makubwa kiuchumi na linaweza kustawi zaidi katika wilaya nne.

Dk. Mgonja alikuwa akiwasilisha jana taarifa yake ya utafiti kwa maofisa kilimo wa kata, madiwani na viongozi wa dini wa Wilaya ya Same.

"Utafiti wa majaribio nilioufanya kuanzia mwaka 1993 mpaka sasa, umeleta mabadiliko makubwa ya maisha ya wananchi wa kijiji cha Mabilioni kilichopo Wilaya ya Same. Wakulima wa ukanda wa Tambarare wa Wilaya za Same, Mwanga, Moshi na Hai tunawashauri kulifanya zao la fiwi kuwa zao kuu la biashara," alieleza Dk. Mgonja.

Fiwi ni aina fulani ya maharage jamii ya kunde ambalo hulimwa katika maeneo ambayo yana ukame, kwa sababu zao hilo hustahimili sana ukame kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa mtafiti huyo, zao la fiwi utafiti wake umeonyesha kuwa linastahimili ukame na gharama ndogo za uzalishaji, ikilinganishwa na mazao mengine ya biashara.

Soko kubwa la zao hilo kwa sasa ni nchi za Kenya na India ambako wananchi wake wengi hupenda kutumia kama chakula, lakini pia Kenya hupenda kutengenezea biskuti.

Sasa wakati zao hilo la fiwi linapigiwa debe, mwaka 2018 na mwaka 2017, serikali za wilaya hizo zilikuwa zikiwahamasisha wakazi wa Wilaya ya Moshi na Hai kuanzisha mashamba mapya ya kilimo cha korosho, vanilla na kahawa kama mazao makuu ya biashara.

# Wenye ulemavu wamlilia waziri umeme

**Na Mary Mosha,** SAME

GHARAMA kubwa ya zaidi ya Sh. milioni 11.3 kwa ajili ya kuunganisha umeme katika makazi ya watoto watano wa familia moja ambao wana ulemavu wa viungo na mtindio wa ubongo katika kijiji cha Gwang'a, kata ya Chome, Wilaya ya Same, zimeibua manung'uniko.

Msemaji wa familia ya walemavu hao, Chedieli Amini, amemwomba Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kuzungumza na Meneja wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), wilayani Same kufikiria upya gharama hizo, kwa kuwa zinaiumiza familia hiyo ambayo haiwezi kumudu.

"Gharama za kuunganishiwa umeme hapa nyumbani ni kubwa mno, tumeambiwa tulipe shilingi 11,367,221.40 ambayo kimsingi, sisi hatuna uwezo huo. Wadau wengi wa maendeleo wametusaidia mambo kadha wa kadha, lakini hili nadhani ni la waziri husika. Tunamwomba atusaidie maana kwetu hatujafikiwa na mradi wa umeme wa REA (Wakala wa Umeme Vijijini)," alisema.

Vijana hao watano wenye ulemavu waliozaliwa na Nirenjigwa Joseph ni Joseph Amini (38), Nafikahedi (33), Wediel (30), Gadson (28) na Julius (25). Wote ni walemavu wa viungo wanaotembea kwa kutambaa.

Mmoja wa wadau aliyejitosa kuisaidia familia hiyo, Isabela Mwampamba, ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Upendo Friends School alisema kwa kushirikiana na wadau wengine wameweza kujenga jiko na ukuta.

Alisema mbali na kujenga jiko na ukuta huo, pia wameweza kuwalipa wafanyakazi wawili wanaomsaidia mama wa familia hiyo.

Familia hiyo ilianza kupata matumaini mapya mwaka 2012, baada ya baadhi ya wadau kuanzisha kampeni maalum ya kuwajengea uzio kwenye makazi yao ili kuwaepusha na ajali mbalimbali wanazozipata kutokana na mazingira wanayoishi na ulemavu walionao.

Mama wa familia hiyo (Nirenjigwa), amejaliwa kupata watoto wanane, lakini watano kati yao wana ulemavu wa mtindio wa ubongo na viungo.

Ukurasa 18



**KASAKA ABAINISHA VIGINGI VILIVYOLIKUMBA KUNDI LA G55**

## MAKALA:

Marafiki Rwanda, Uganda wanavyotunishiana misuli



Ukurasa 19

## KIMATAIFA:



**Waziri Mkuu Netanyahu mtuhumiwa anayejiandaa uchaguzi mkuu Aprili**

Ukurasa 15


# siasa

JUMATANO MACHI 6, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




**Wakuu imetosha, acheni kuwasukuma ndani raia**

Ukurasa 20

# Msomi afunguka mambo 12 yanayohusu kuhama Lowassa


**Na Mwanshishi Wetu**

IJUMAA iliyopita katika uliongo wa siasa, ulishuhudiwa mshituko wa aina yake, umma uliokusanyika katika ofisi ndogo ya makao makuu ya CCM Lumumba jijini Dar es Salaam, wakati Edward Ngoyai Lowassa, alipotangazwa rasmi kurejea katika chama chake alichokulia.

Ni hatua iliyoamsha kila aina ya mazungumzo na mjadala kuhusiana na uamuzi huo kwani haikutegemewa kwa aliyekuwa mgombea urais wa Chadema katika uchaguzi mkuu uliopita kurudi nyumbani. Na baada ya hapo zikasikika dodoso kutoka pande mbalimbali za kisiasa kuhusu uamuzi huo.

Je katika mustakabali wa kisiasa, kuanzia vyama hivyo viwili vilivyoguswa na maamuzi hayo, mwenendo wa kisiasa nchini na tafsiri ya kiufundi kutoka taaluma ya sayansi ya siasa, kuhamahama huku kunamaanisha

ENDELEA UK 16



Edward Ngoyai Lowassa

UCHAMBUZI

Na Sabato Kasika

# La kujifunza kutokana na kuhama kwa Lowassa



Lowassa katika maisha ya kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, amerejea katika chama chake cha zamani, Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambacho alikihama muda mfupi kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Lowassa alihamia kwa wapinzani mara baada ya kumalizika kwa mchakato wa kumpata mgombea urais ndani ya CCM, ambao ulionekana kutomfurahisha, hivyo akahama na baadhi ya makada wa chama hicho kujiunga na Chadema.

Historia inaonyesha kuwa katika safari yake ya kwenda Chadema alisindikizwa na kila aina ya kejeli kutoka kwa baadhi ya wanachama wa CCM, waliokuwa pia wakidai kwamba hafai kupewa ridhaa ya kuongoza nchini.

Kwa ujumla ni kwamba kila aliyepata nafasi ya 'kumshambulia' kwa maneno alimsema alivyotaka, hasa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, lakini kama kawaida yake alikuwa kimya kama hasikii.

Wana-CCM waliokuwa wakimrushia madogo walikuwa ni wa pili, kwani walioanza ni wapinzani hasa Chadema, wakati huo akiwa bado hajahamia kwao, ambapo walidai kuwa ni fisadi.

Lakini alipohamia kwao, Chadema walinywea kana kwamba hawajawahi kumtuhumu kwa ufisadi, badala yake wakasema wameamua kubadili gia angani kwa kumpitisha awanie urais.

Ukiangalia kisa hiki unaweza kutoa ujumbe kwa wanasiasa wawe na akiba ya maneno na pia wajifunze kuwa na uvumilivu wa kisiasa, wakitambua kuwa kila mtu ana haki ya kujiunga au kuhamia chama chochote ya siasa anachokitaka.

Kushambuliana kwa maneno au kutolea matusi na kejeli na kashfa , kwasababu tu amehamia chama fulani huenda ni kutomtendea haki mhusika, pengine hizo ni siasa wanasiasa wanaweza kuziita za majitaka na huenda zimepitwa na wakati hazipaswi kupewa nafasi na watu waliokomaa kisiasa.

Yawezekana kila mtu akawa na maoni yake kuhusu uamuzi wa Lowassa kurudi CCM, lakini ni vyema kujifunza jambo kutoka kwa mwanasiasa huyo, ambaye ameonyesha ukomavu wa kisiasa.

Kama angekuwa hajakomaa kisiasa, angeweza kujibu mapigo kwa wale waliokuwa wakimshambulia kwa maneno kuwa ni fisadi au hafai kuwa kiongozi ama kumkejeli kwa kila namna.

Waliomtuhumu kwa ufisadi walikaa kimya alipojiunga katika chama chao, na sasa waliomtusi baada ya kuhamia upinzani, wamenywea kufuatia uamuzi wake wa kurudi katika chama hicho tawala.

Pengine ni vyema wanasiasa wakajifunza kwamba siasa hazina uadui wala urafiki wa kudumu na pia wasiwe wepesi wa kuwasema vibaya, bali watambue kuwa suala la mtu kuhama chama kimoja kwenda kingine ni haki yake ya kikatiba na kidemokrasia.

Wanasiasa wanatakiwa kujifunza kwamba mtu wanayemtukana kwasababu tu amehama kutoka katika chama chao, kesho anaweza kurudi kuungana nao hivyo kujikuta wakiona aibu hata kumsalimia . Wakumbuke siasa si uadui kwani kuna maisha baada ya kuhama chama.

Lowassa alipohamia upinzani, hakuwahi kuisema vibaya CCM na sasa amerudi CCM hajawasema kuichambua wala kuizungumzia vibaya Chadema, kwasababu inawezekana anatambua hizo ni siasa za majitaka ambazo aliamua asizipe nafasi.

Bahati nzuri uamuzi wake wa kurudi CCM hajapata mashambulizi kutoka katika upinzani kama ambavyo baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakifanya.

"Hakutuhonga wala hakununua chama kama tulivyotukanwa huko nyuma. Tulimkaribisha na kumpatia majukumu ya kutuongoza kwenye mapambano ya 2015. Na alitekeleza majukumu hayo vizuri, kwa kadiri alivyoweza na kadiri tulivyomwezesha. Matunda ya kazi yake na yetu yanajulikana. Sasa mwendo wa ugenini umemshinda."



Chama cha Demokrasia na Maendeleo kilichompoteza mwanachama huyo kinasema kuondoka kwa Lowassa na kurudi CCM hakutakuwa na madhara yoyote.

Katibu Mkuu wa chama hicho kikuu cha upinzani Tanzania, Dk. Vincent Mashinji anasema wanamtakia maisha mema huko alikokwenda kwa vile ni mtu mzima anayejua anachokifanya.

Hata hivyo, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, anasema kama kuna jambo la maana ambalo Lowassa amelifanyia Chadema ni kuamua kurudi CCM.

Kwa upande wake Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu anamtakia Lowassa, kila heri na mapumziko mema 'nyumbani' kwake alikorudi.

"Nimeulizwa na watu wengi sana juu ya maoni yangu kuhusu Mzee Edward Ngoyai Lowassa kurudi CCM. Nilisema nasubiri hili vumbi la hizi siku chache zilizopita litulie kwanza ndipo niweze kusema maoni yangu. Sasa ni muda mwafaka kufanya hivyo. Mzee Edward Lowassa mwenyewe amesema amerudi nyumbani. Maana yake ni kwamba alikuwa ugenini tangu Julai 2015." anaeleza Msigwa.

"Hakutuhonga wala hakununua chama kama tulivyotukanwa huko nyuma. Tulimkaribisha na kumpatia majukumu ya kutuongoza kwenye mapambano ya 2015. Na alitekeleza majukumu hayo vizuri, kwa kadiri alivyoweza na kadiri tulivyomwezesha. Matunda ya kazi yake na yetu yanajulikana. Sasa mwendo wa ugenini umemshinda. Misalaba ya upinzani imekuwa mizito sana. Ameamua kurudi nyumbani, kupumzika," anasema Lissu.

Anasema badala ya kumlaani kuondoka katika chama chao, anamtakia mapumziko mema nyumbani kwake na kwamba wataendelea na safari yao ya Kanani.

"Lowassa alijiunga Chadema Julai 2015, baada ya jina lake kuenguliwa kwenye mchakato wa kutafuta mgombea wa urais ndani ya CCM na baada ya kujiunga nasi alipambana na Rais John Magufuli na kuwa nyuma kwa kura 6,072,848 na Magufuli akishinda kwa kura 8,882,935. Mimi namtakia kila la heri na mapumziko mema 'nyumbani' kwake. Sisi tutaendelea na safari yetu ya Kanani," anasema.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, anasema hatua ya Lowassa kurudi nyumbani inaashiria chama hicho kinaanza kazi ya kujenga taifa.

"Kama alivyosema Waziri Mkuu mstaafu, Lowasa amerudi nyumbani, tunaanza kazi ya kujenga taifa letu na kulinda udugu wetu," anasema Dk. Bashiru.

Kauli za wanasiasa hao zinaonyesha ni jinsi gani wengine wanapaswa kubadilika na kuona uamuzi wa mtu kuhama chama kimoja kwenda kingine ni jambo la kawaida ambalo halihitaji 'kushambuliwa' kwa maneno.

Huenda hakuna matusi wala kejeli bali wanachokisema ni namna ya kuendelea kuimarisha vyama vyao kwa ajili ya maendeleo ya nchi siyo kumjadili au 'kumshambulia' kwa maneno mwanachama aliyehama chama.

Wenye mawazo na mtazamo kuwa mwanasiasa kuhama chama kimoja kwenda kingine ni kosa kubwa, hao wanaweza kuzalisha chuki za kisiasa ambazo hatima yake siyo nzuri.

Wajifunze jambo kutoka kwa Lowassa ambaye pengine ameonyesha uvumilivu wa hali ya juu ingawa amenangwa, kukejeliwa kwa kila namna, lakini hakuwahi kujibu mapigo.

# KIWEWE ISRAEL

## Waziri Mkuu Netanyahu mtuhumiwa anayejiandaa uchaguzi mkuu Aprili



Mtuhumiwa wa rushwa, Benjamin Netanyahu, akiwa na mgeni wake Rais wa zamani wa Marekani, Obama, kwenye moja ya mikutano ya kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya Mashariki ya Kati baina ya Wayahudi na Wapalestina. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

WACHUNGUZI wa masuala ya siasa na hasa mwenendo wa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, wanaangalia kwa makini nini anachokifanya na kwa madhumuni gani, kwani tayari polisi wa nchi hiyo wameeleza nia ya kumfungulia mashtaka ya rushwa.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Israel imefikia tamati kuwa kuna ushahidi wa kutosha Netanyahu kufunguliwa mashtaka ya rushwa.

Kwa vile tayari kampeni za uchaguzi zimeshaanza na Netanyahu ndiye kiongozi wa chama cha Likud, wadadisi wanaangalia atacheza karata zipi. Suala analotaka ni bunge likirudi itungwe sheria au marekebisho ili kuzuia asishtakiwe akiwa madarakani.

Wachunguzi wana uhakika kuwa endapo Netanyahu atafikishwa mahakamani kwa makosa yaliyoorodheshwa na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anaweza kuhukumiwa kifungo. Wanasema kuwa hakuna njia ya ofisi hiyo kubadili msimamo au mwelekeo wake, kwani iliorodhesha makosa kwa uangalifu, akipuuzia baadhi ya mapendekezo ya Mwendesha Mashtaka na Idara ya Upelelezi ya Jeshi la Polisi.

Kuna barua ya kurasa 57 ambayo Mwanasheria Mkuu Mendelblit alimpelekea Netanyahu na licha ya kuwa yapo maeneo ya faraja kwa waziri mkuu huyo, kwa jumla inamtaja kama mla rushwa na mtoa rushwa, asiyeaminika.

Wakati sehemu kubwa ya washindani wake wakijiandaa kwa yeye kufikishwa mahakamani, ni hatua ambayo itahitaji avuliwe madaraka kwanza na siyo lazima chama cha Likud kikubaliane na pendekezo hilo.

Moja lililotajwa katika vyombo vya habari vya Israel ni kuwa Netanyahu anataka aina fulani ya kupindua serikali, yaani kufuta mpangilio wa madaraka na uwezo wa kushtakiwa ulio mikononi mwa vyombo vya dola au mihimili mingine ya utawala.

Kilichobaki kwa Waziri Mkuu Netanyahu, kwa maoni yao, ni kutumia nafasi aliyonayo katika chama hicho, na uchaguzi, kuweza kuidhibiti hali kisheria.

Tayari baadhi wameanza kuandika tanzia za utawala wa Netanyahu, kuwa amedumu madarakani miaka 13 na sasa amefikia kiama chake, kama mlarushwa, mchafu na asiyeweza kujitetea katika orodha ndefu ya makosa aliyofanya.

Kilichobaki ambacho bado kina utata ni kama vyama vya siasa kuanzia Likud na vinginevyo vina uwezo wa kuunda umoja wa kutosha miongozi mwao wapate mkusanyiko tofauti usioongozwa na Netanyahu, ili uchaguzi mkuu ufanyike bila sehemu kubwa ya nchi kumtegemea na bila mparaganyiko wa kisiasa.

Na kwa nchi ambayo vyama vya siasa vinapigana kufa na kupona kupata kiti kimoja kwa Baraza la Mawaziri hiyo ni fursa.

Israel ni nchi iliyozoea kuwamulika viongozi wake na ikipata ushahidi wa kutosha wamefanya nini au wamekuwa wakifanya nini, haisiti kuwafikisha mahakamani na kwa jumla ikishafika hapo uwezekano wa kupona ni mdogo.

Tayari baadhi ya wachambuzi wanaona Netanyahu akili yake yote ni jinsi ya kukwepa kuingia jela yenye jina la kushangaza la Maasiyahu ambako waliwahi kufungwa viongozi akiwamo waziri mkuu na rais wa zamani, kuhani mkuu wa zamani, mawaziri, wakadau wakubwa miongoni mwa wanasiasa na wafanyabiashara.

Ni wazi kuwa kuingia Maasiyahu licha ya kuwa ni kitendawili, haitakuwa tukio la kushangaza.

> Licha ya kwamba miaka 13 katika nafasi ya uwaziri mkuu ni mingi sana na siyo ajabu nchi inahitaji mabadiliko, bado mlango wa kutokea hauko wazi kutokana na tuhuma hizo.

Wachunguzi wa habari wanasema haijapata kutokea mtu anayeongoza chama kikubwa na hasa akiwa ni waziri mkuu kuingia katika uchaguzi mkuu akiwa na tuhuma kama hizo, na tangazo limeshatolewa kuwa anaweza kushtakiwa wakati wowote.

Jemadari mmoja aliyeinuka ambaye amewahi kuwa mkuu wa jeshi la Israel, Benny Gantz, ambaye ameanza kuonekana kama anaweza kuchukua nafasi ya Netanyahu kuleta mazingira mapya, kuwa na waziri mkuu asiye na mzigo wa tuhuma zinazomwandama.

Hata hivyo hakuna uhakika au ushahidi bayana kuwa wapiga kura wa chama cha Likud watakikimbia chama hicho kutokana na tuhuma dhidi ya Netanyahu.

Ili Netanyahu awe na uwezo wa kuidhibiti hali hiyo inabidi kwanza ashinde uchaguzi mkuu, ambayo ina maana kuwa wapiga kura wa Likud waendelee kuwa na imani naye, pamoja na kuwa vyombo vya nchi kimsingi vimemtia hatiani kwa makosa ya rushwa , madai hayo inabidi yathibitishwe mahakamani.

Endapo wapiga kura wake wataendelea kuwa na imani naye, ashinde uchaguzi kama kiongozi wa Likud, anaweza kutoa ahadi zinazopasa kwa vyama vya siasa vyenye uwezo wa kuunda serikali pamoja naye, wapitishe marekebisho yanayotakiwa kuzuia Netanyahu asifikishwe mahakamani. Swali hapo ni kama wanamhitaji kwa kiwango hicho.

Wachunguzi wanasema inabidi Netanyahu ashinde uchaguzi halafu afikie makubaliano na vyama vya mrengo wa kulia vinavyopania ulinzi na usalama, kutotaka kusikia amani inayokubaliwa na Wapalestina na pia vikundi vya kihafidhina vya dini ya Uyahudi, ambao ni mwiba katika siasa za nchi hiyo.

Wakati kila kijana anatakiwa kisheria kutumikia jeshi kwa kipindi maalum kama JKT ilivyokuwa hapa zamani kwa Tanzania, makundi hayo hafidhina mara nyingine yanaweka pingamizi kwa wafuasi wao na hawasemi ni wa dhehebu au tafsiri fulani ya dini ila wanataka ijulikane kuwa wao ndiyo wenye tafsiri sahihi.

Ni walinzi halisi wa imani na utamaduni wa dini hiyo.Wako wachambuzi wanaomlaumu Jemadari Gantz kuchelewa kuunda chama kushindana na Netanyahu, kwani kwa kufanya hivyo hana njia nyingine ila kuwa katika mazingira ya kuunda serikali pamoja na Likud ya Netanyahu.

Hakuna serikali ya mrengo wa kulia inayoweza kuundwa bila Netanyahu na Likud kuwapo, hivyo Gantz anakuwa siyo mbadala kwa uongozi wa Netanyahu labda kama angekuwa ametoswa na Likud kama kiongozi wao, na siyo rahisi wao kufanya hivyo.

Licha ya kwamba miaka 13 katika nafasi ya uwaziri mkuu ni mingi sana na siyo ajabu nchi inahitaji mabadiliko, bado mlango wa kutokea hauko wazi kutokana na tuhuma hizo.

Wakati Israel imechanganyikiwa kuwa waziri mkuu wake ni mlarushwa lakini hakuna mbadala kwa uongozi wake kwenye chama cha Likud na kwa njia hiyo labda hata kwa taifa kwa jumla. Israel inaendelea kuzingirwa na maadui, hasa kwa kutumia makombora na mahandaki kuizunguka nchi hiyo.

Kimsingi hali hiyo imeleta pia kumtegemea Netanyahu kama kiongozi thabiti ambaye hata uongozi unapobadilika Marekani akatokea rais kama Barack Obama aliyeisukuma Israel ikubaliane na Wapalestina, kama Bill Clinton alivyomsukuma Ehud Barak aafikiane na Yasser Arafat, Netanyahu alisimama kidete akamgombanisha Obama na raia wa nchi hiyo.

MAKALA

Inatoka Uk.13

nini?

**MSOMI AFUNGUKA**

Katika kupata ufafanuzi huo kitaalamu, Nipashe ilizungumza na mwanataaluma wa sayansi ya siasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Respicius Shumbusho, ambaye anaainisha uamuzi huo wa Lowassa katika mitazamo 12 tofauti, akichambua kwa kuangalia vyanzo vilivyomsukuma kuchukua hatua hiyo.

Anaanza kwa kuiangalia hatua ya kurudi CCM, kwa kumtazama mhusika mkuu ambaye ni Lowassa. Anaeleza kwamba alichokifanya, mantiki yake ni kile ambacho kila binadamu anachotamaniwa ambacho ni kuwa ma ushawishi wa umma na kukubalika, ambacho kitaalamu anakiita 'power na influence."

Dhana hiyo kwa mujibu wa Dk. Shumbusho ni kitu ambacho binadamu yeyote anatamani kukifikia huku akiieleza hali hiyo katika uwanja wa siasa, ni pamoja na kuweza kushawishi wengi, ni pale mawazo au fikra na msimamo binafsi zinaposhinda na kufikia hatua ya kukubalika.

"Binadamu anapenda asikilizwe, akubalike, ushauri na maamuzi yake yawafikie wengine na wayakubali hiyo ndiyo influence na power ambazo kiongozi, mwanasiasa , mfanyabiashara na kila binadamu anapenda afikie hapo.

"Kwa hiyo kutamani kuendelea kuwa na power ni jambo linaloweza kusababisha kuhama kutoka upande mmoja kwenda mwingine," anasema katika uchambuzi huo.

**SIASA VS HISTORIA**

Anamtizama kiongozi huyu kihistoria akisema mienendo ya wanasiasa inaathiri na historia zao akiwarejea wakongwe wa siasa nchini, anaeleza kuwa ni watu walioandaliwa na kulelewa tangu mwanzo kuwa wanasiasa.

Msomi huyo wa siasa anawaeleza kuwa ni watu wanaoishi maisha yao katika siasa na hawawezi kuondoka, akiyafananisha na uraibu (addiction), hivyo wanatumia mbinu na fursa zote ili kuendelea kubaki katika ulingo wa siasa na kudumu zaidi.

Aidha, Dokta Shumbusho anakifafanua kilichofanywa na Lowassa kuwa ni hisabati za kisiasa, mtaaluma huyo anaweka maono ya kisomi kwamba mwanasiasa huyo ameangalia mbele zaidi ya miaka mitano na sasa amejipanga upya katika nafasi yake ya kisiasa.

Anaendelea: "Amesoma alama za nyakati na kuangalia upepo unavyovuma. Licha ya kusema kuwa CCM siyo mama na baba yake, lakini kwa kuangalia mbele zaidi, anabadilisha maamuzi. Kwani hisabati zinamwelekeza namna ya kufika mbele anapotaka.

"Anaangalia eneo ambalo anapata mafanikio na si kwenda kupoteza. Anafahamu anavyochanga karata zake, kwani anapiga hesabu za fursa zitakazoibuka baadaye. Kwa mfano 2020 ni uchaguzi mkuu, anajua anacholenga,"anaeleza mbobezi huyo wa siasa.

Katika uchambuzi wake, Dk. Shumbusho, anasema kuna baadhi ya wanaowaona wazee kama Lowassa, wanaangukia kundi la wale wanaopaswa kujiweka pembeni wakiwapa nafasi ya kung'atuka, kuwa washauri na watazamaji, lakini mbinu ya kisiasa ya Lowassa inakinzana na hilo kwa kujongea karibu zaidi na siasa iliko.

Anarejea nadharia ya kisiasa inayooanisha mazingira ya namna hiyo kuwa, katika mchezo wa kisiasa hata kama mhusika hukubaliani na mfumo unachokitaka au unachokifanya, anasimamia kuunga mkono mfumo huo ili aendelee kuonekana katika uongozi wa nchi , kupitia michango mbalimbali kama vile fikra , maoni na kazi zake .

# Msomi afunguka mambo 12 yanayohusu kuhama Lowassa

> "Tatizo linaloonekana sasa ni kwa vyama kuandaa viongozi wenye msimamo fulani kwa wakati fulani, lakini ukifika muda usiofahamika wanaondoka na kubadili misimamo yao,"



Edward Lowassa akisalimiana na Mwenyekiti wa CCM, Rais John Magufuli baada ya kuhamia CCM Ijumaa iliyopita. Wanaoshuhudia ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Mashiru Ali(wa pili kulia) na mwana-CCM Rostam Aziz. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Lowassa akipokea kadi kutoka kwa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe alipojiunga na chama hicho mwaka 2015.

**INAMAANISHA NINI?**

Dokta Shumbusho anajumuisha tafsiri ya kuhama kwa Lowassa kutoka CCM kwenda Chadema na kurudi tena CCM, akisema katika siasa za sasa ni uhuru wa kisasa uliopo katika mfumo wa vyama vingi usiowazuia watu kuhama.

Anataja kwa mfano, 'hakuna cha kuhofia wala cha kumzuia' mwanachama katika harakati zake kisiasa.'

Anareja mantiki ya demokrasia kwa wanasiasa kuwa ni kuwapa nafasi ya kufikia maamuzi pasipo cha kuhofia na wanakuwa huru kuamua watakacho, wakiongozwa na mapenzi yao ya wapi waelekee kwa mujibu wa vigezo binafsi.

Anaainisha baadhi ya vigezo vinavyochangia misukumo ya kuhama ni tofauti baina ya vyama katika mazingira kama ya sera, itikadi na mwelekeo.

Hata hivyo anagusia dhana ya hamu ya uongozi kuwa hamasa ya wanasiasa kuhama, kwani kadri umri unavyoongezeka ndivyo hamu ya kutafuta uongozi na ushawishi zaidi inavyoongezeka wakifikia kipindi hicho wanatamani kuheshimika, kukubalika na kuthaminiwa zaidi .

Kwa mujibu wa tafsiri rasmi za sayansi ya siasa kama zilivyoandika na wanataaluma David Easton na Harold Lasswel, siasa inahusu haja ya kushika mamlaka rasmi ya kusimamia watu na rasilimali, huku dhana ya kukubalika ni msingi muhimu sana katika utekelezaji wake.

**KWENYE VYAMA JE?**

Msomi huyo anasema ndani ya vyama vya siasa, tukio hilo la kuhama lina tafsiri kuu mbili chanya na hasi .Mosi ni kwamba inajenga uwanja wa demokrasia ndani ya vyama vya siasa , mtu kuwa na uwanda huru wa kuingia na kutoka katika chama chochote bila ya vikwazo.

Anasema hilo linaendana na kutengeneza mazingira ambayo chama cha siasa hakiwezi kujihisi au walau kujiamini kwamba kinammiliki mwanachama au mfuasi kwa kiwango kikubwa, kuliko fursa, utashi na maamuzi yake mwenyewe.

Dokta Shumbusho anatumia kielelezo cha mfano kwamba ni mazingira ya kuondoa uwezekano wa chama kuona kwamba kinammilikia mtu au mwanachama kufikia kiwango cha kufunga milango ya maamuzi yake binafsi .

Msomi huyo wa UDSM ambaye pia amebobea katika masuala ya sera na utawala wa umma, anasema: "Ndani ya vyama kuna uhuru wa mtu, ukomavu wa demokrasia na fursa sawa kwa Watanzania wote kufanya vile wapendavyo katika kujiunga na chama fulani.

Katika sura nyingine anasema kuhamahama ni mapungufu ya kiuwezo katika baadhi ya vyama vya kisiasa, ambavyo vinashindwa kutengeneza msimamo thabiti ambayo wanachama wanausimamia kama timu moja pasipo kutetereka.

"Vyama vimeshindwa kuwa na msimamo ambao si rahisi kumbadili mwachama anapouamini. Kila mtu anabaki alivyo, lakini kwa chama unachokitumikia unaamini na kusimamia misimamo yake. Kwa hili, vyama vimeshindwa kuwaandaa na kuwapata wanachama wanaosimamia na kutembelea misimamo iliyomo," anasema.

Pia anataja eneo la viongozi ambako baadhi ya vyama vinashindwa kuwaumba na kuwalea walio na misimamo isiyoyumba, kutapatapa wala kubadilika.

"Tatizo linaloonekana sasa ni kwa vyama kuandaa viongozi wenye msimamo fulani kwa wakati fulani, lakini ukifika muda usiofahamika wanaondoka na kubadili misimamo yao," anaeleza.

"Huku kuhamahama, kunaleta wasiwasi. Hivi viongozi hawa wanabeba itikadi, sera, malengo? Na kama kweli wanafanya na kutimiza malengo ya chama?" anahoji Dk. Shumbusho.

**VYAMA HAVITOFAUTIANI**

Tafsiri yake kuhusu kuhamahama na kurejea kwa wanasiasa maarufu nchini ni kwamba huenda vyama hivyo vya siasa havitofautiani kwa kiasi kikubwa, akitaja baadhi ya maeneo ya ukaribu kama sera, mipango na mikakati ya kuleta maendeleo ya nchi.

Msomi huyo ana mtazamo mwingine kuwa, suala la kuhama lina sura ya mwanachama binafsi kutumia fursa hiyo ya kidemokrasia kama nyenzo ya kutetea nafasi yake

**NINI KIFANYIKE?**

Kama ulivyo mwongozo na utaratibu wa wanataaluma, ambao mbali na kungia darasani , wamebobea kwenye utafiti na ushauri wa kitaalamu , majumisho ya hoja zao yanaendana na ushauri au hoja inayofungua mlango wa kuelekea kwenye neema zaidi, Dk Shumbusho anayo machache.

Anashauri kwamba vyama vya siasa katika maamuzi yake mengi yasiwe ya muda mfupi , bali yaundwe na mchakato wa kina unaochanganuliwa kwa kushirikisha wanachama wa ngazi zote na maamuzi yakubalike na wengi.

Historia inaonyesha kwamba huko nyuma mwaka 1995 aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani pia Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Augustine Mrema, alihama CCM na kujiunga na NCCR-Mageuzi, alikoteuliwa kuwa mgombea urais pia Mwenyekiti wa chama hicho.

Aidha, aliondoka NCCR -Mageuzi na kuhamia Tanzania Labour Party (TLP) hata hivyo japo hakurudi CCM, chama kilichomlea lakini, anaonekana kama Mrema nu mfuasi halisi wa CCM.

Mwaka 2015 katika kampeni za uchaguzi mkuu aliwahamasisha wanachama wa TLP Vunjo kumpigia mgombea wa CCM.

Halikadhalika, Lowassa, mara tu baada ya kujiengua kutoka CCM mwaka 2015, alijiunga na Chadema ambako aliteuliwa kuwa mgombea urais katika uchaguzi mkuu uliopita.



Fayez Sarraj Mkuu wa Serikali ya Libya, inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa. **PICHA: XINHUA**

# Libya hakukaliki miaka 8 baada ya Gaddafi

**TRIPOLI,** Libya

FEBRUARI mwaka huu inatimia miaka minane tangu kutokea uasi uliofuatiwa na mapinduzi ya kumuondoa madarakani na kumuua Rais wa zamani wa Libya Muammar Gaddafi.

Hali ni tete, uthabiti na demokrasia katika taifa hilo la kaskazini mwa Afrika, vinabakia kuwa ndoto.

Licha ya kwamba Walibya walifanikiwa kuuondoa uongozi wa kidikiteta wa Gadaffi mwaka 2011 kupitia vuguvugu la mageuzi katika nchi za Kiarabu, taifa hilo bado halijaweza kufikia uongozi bora wa kidemokrasia kutokana na machafuko ya mara kwa mara.

Lakini raia wengi wanasema hawajutii lolote kwa kumuondoa madarakani Gaddafi aliyeongoza taifa hilo kwa muda wa zaidi ya miaka 44.

Wanasema wanayo matumaini ya nchi hiyo kuwa na amani na kupata uongozi bora.

Mhandisi katika kiwanda cha mafuta, Marwan Jalal (43) anasema yanayotokea hivi sasa nchini Libya ni matokeo ya uongozi mbaya wa Gaddafi uliodumu kwa zaidi ya miongo minne.

Anaelezea matumaini kuwa kabla ya muda mrefu nchi yao itakuwa imara, japo safari hiyo itachukua muda mrefu.

"Mabadiliko yalihitajika na ilikuwa ndiyo nia ya kila mtu, walioongozwa na waliokuwa wakiongoza. Kila aliyeko katika uongozi, wabunge, wote walitaka mabadiliko.

"Kama raia tunataka mabadiliko, tulitaka kuandamana, kubeba mabango, kushangilia na kuinua bendera ya uhuru. Ila madhalimu walikuwa tayari wamepanga mipango yao," alisema mmoja wa raia wa Libya Ali Mohammed al-Suaihi.

**LIBYA UWANJA WA VITA**

Libya kwa sasa imesalia kuwa uwanja wa vita baina ya maelfu ya waasi na makundi ya wanasiasa wanaoongoza bila kujali sheria huku mgawanyiko ukizidi baina ya utawala na jeshi.

Hata hivyo jitihada za kuwaleta pamoja kwa ajili ya kumaliza mzozo huo zinakwama.

Mchambuzi katika kundi la kimataifa juu ya mizozo, Claudia Gazzini, anasema mkakati wowote wa kumaliza mzozo wa Libya unahitaji kuhusisha siasa, usalama na uchumi na kila upande uwe na lengo moja, ila hakuna njia ya moja kwa moja ya kumaliza migogoro ya kila aina iliyopo nchini humo.

Katika hatua za kidharura za hivi karibuni, kamanda mwenye nguvu wa vikosi vinavyodhibiti eneo la mashariki mwa Libya Generali Khalifa Haftar, alianzisha mashambulizi ya kijeshi kusini mwa Libya ya kuwafurusha magaidi na wapiganaji wa kigeni.

Japo hatua hiyo imezua hofu mpya na pia wachanganuzi wanaonya kwamba mashambulizi hayo yanaweza kuhatarisha kufanyika kwa mkutano wa kitaifa unaoongozwa na Umoja wa Mataifa kwa malengo ya kupanga uchaguzi ambao tayari umechelewa.

Ukosefu wa ustawi wa taifa hilo umewapa nafasi walanguzi wa binadamu kujificha kupitia watu wengi wanaolihama taifa hilo kwenda mataifa jirani.

Zaidi, Libya kwa sasa ni taifa ambalo halina utawala wa sheria kutokana na mvutano wa uongozi baina ya serikali ya mjini Tripoli inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa na uongozi sambamba wa kikosi cha jeshi la Libya (LNA) linaloongozwa na Generali Khalifa Haftar ,upande wa Mashariki.

Makundi yaliyo na silaha, wapiganaji wa Jihadi na waasi wa Chad wamefanya makao katika mipaka ya Libya inayopakana na Algeria, Niger, Chad na Sudan.

Mchambuzi Gazzini anasema pia kuna vita baina ya kabila dogo la Tubu na makabila ya Kiarabu wanaopigania kudhibiti maeneo ya mipakani kuendeleza biashara za magendo.

**Idhaa ya Kiswahili ya DW**

Na Mwandishi Wetu

MWAKA 1993 wakati wa Bunge la Bajeti, liliibuka vuguvugu la hoja ya kutaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika baada ya kuwapo kwa kero mbalimbali ambazo zilionyesha kuwa Muungano uko katika matatizo.

Kama wahenga wasemavyo panapofuka moto kuna moshi, jambo hilo lilianza kupata mashiko wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais aliyoiwasilisha bungeni, wakati huo katika ukumbi wa Karimjee.

Baada ya hotuba hiyo, wabunge mbalimbali kama kawaida, walichangia na mmojawapo akiwa Mbunge wa Chunya mkoani Mbeya, Njelu Kasaka. Katika mchango wake alikwenda moja kwa moja kuzungumzia suala la Muungano akiweka mkazo kuundwa kwa serikali ya Tanganyika.

Hatua hiyo iliibua msisimko mkali kutoka kwa baadhi ya wabunge na hatimaye kujitokeza kwa kundi la wabunge 55 maarufu kama G55 waliotia saini kutaka iundwe serikali ya Tanganyika. Awali wabunge waliotia saini na kuwasilisha majina yao kwa aliyekuwa Naibu Spika, Pius Msekwa, walikuwa 44, idadi ambayo ilikidhi matakwa ya kikanuni kuwasilishwa kwa hoja hiyo ndani ya Bunge.

Wabunge hao, baada ya kuwasilisha orodha yao chini ya mwenyekiti wao mateo Qaresi (Babati) na Kasaka aliyekuwa katibu na mratibu wa mchakato huo, Msekwa alizungumza na waandishi wa habari na kuweka bayana kuwa hoja hiyo imepangiwa ratiba kwa ajili ya kuwasilishwa.

**VIGINGI VYA HOJA**

Kasaka katika kitabu chake cha 'Njelu Kasaka- Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika- G55' anabainisha kuwa baada ya vyombo vya habari kuandika juu ya suala hilo, vilianza kuibuka vigingi ambavyo vilikuwa na lengo la kuizima hoja hiyo.

"Baadhi ya viongozi upande wa serikali walihoji busara ya kutaka kuwapo kwa serikali ya Tanganyika wakati idadi kubwa ya Watanzania wamezaliwa katika Muungano, hivyo hawajui lolote kuhusu Tanganyika. Lakini kwa kutazama mazingira yaliyokuwapo katika viwanja vya Karimjee, yalikuwa kinyume kabisa na mtazamo wa viongozi hao wa serikali.

"Watu wengi waliojaa kwenye viwanja vya Karimjee wakifuatilia na kushabikia hoja walikuwa vijana. Wengine walisikika wakisema "tunataka Tanganyika yetu". Viongozi hawa wa serikali walisahau au hawakujua kwamba hisia za utaifa huwa haziishi kirahisi hivyo," anasema Kasaka.

Katika kuthibitisha hilo, Kasaka anatolea mfano wa baadhi ya wananchi wa Scotland ambao mwaka 2015 walipiga kura kudai taifa lao baada ya zaidi ya miaka 300 tangu ilipoungana na England na kuunda Uingereza.

**MAJADILIANO NA SERIKALI**

Baada ya kupokea taarifa ya kuwapo kwa hoja ya Tanganyika kutoka kwa Naibu Spika, serikali iliunda timu ya kujadiliana na wabunge, ikiongozwa na aliyekuwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Samuel Sitta ambaye pia alikuwa Mbunge wa Urambo.

Wajumbe wa timu hiyo ya serikali walikuwa Edward Lowassa ambaye wakati huo alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais; Anne Makinda (Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto); na Muhammed Seif Khatib aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (Muungano).



# KASAKA
## abainisha vigingi vilivyolikumba kundi la G55

> "Kwanza, hoja ilikuwa inapingana na Kanuni za Kudumu za Bunge na kwa kuwa hoja binafsi inahitaji kibali cha Spika kujadiliwa, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais walimtaka Naibu Spika asitoe kibali, hivyo hoja itakufa.

Kwa upande wa wabunge, wajumbe walikuwa Kasaka, Qaresi, Patrick Qorro (Karatu), Walliam Mpiluka (Mufundi), Arcado Ntagazwa (Kibondo), Mussa Nkhangaa (Singida Mjini) na Abdalla Said Nakua (Lindi Mjini).

"Hatua ya awali ya selikali ilikuwa kututaka tuachane na hoja hiyo na kuiondoa bungeni. Pendekezo hilo tulilikataa na kulifanyika vikao sita bila mafanikio. Hatimaye upande wa serikali ukaunga mkono na ukakubali hoja ifikishwe bungeni isipokuwa muda wa utekelezaji ubadilishwe na mchakato mzima wa kufikia uamuzi huo uwahusishe wananchi," anasema Kasaka.

Kwa mujibu wa mwanasiasa huyo, baada ya mikutano hiyo sita, wabunge waliohudhuria walikwenda kwa wabunge wenzao waliokuwa wakiunga mkono hoja hiyo ambao baadaye walifikia 57 kutoka 44 lakini baadaye wawili walijitoa na hatimaye kubaki 55 na kufahamika kuwa G55. Wabunge waliojitoa ni Donald Kusenha (Dodoma Mjini) na Dk. Chinuno Magoti (Taifa).

"Kusenha alisema hakutaka au isingekuwa vizuri kwake kuunga mkono hoja inayombana Waziri Mkuu John Malecela aachane na msimamo wa serikali wa muundo wa serikali mbili kwa kuwa wanatoka sehemu moja, Dodoma. Dk. Magoti kwa upande wake alisema alikuwa karibu sana na Mwalimu Nyerere, hivyo kumwia ngumu kupingana naye. Niliwajulisha wabunge wengine uamuzi wa wabunge hao wawili na wakaridhia," anasema.

Baada ya makubaliano na serikali, Kasaka anabainisha kuwa walifanya marekebisho ya hoja kwa kubadili tarehe na kuingiza kipengele cha kuwahusisha wananchi katika kubadili sera ya CCM ya serikali mbili.

Anasema hoja hiyo ilirekebishwa na kuelekeza serikali kuandaa kura ya maoni kabla ya desemba 31, 1994 ili kupata maoni ya watu kuhusu kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano.

"Niliichapisha hoja iliyorekebishwa na kuiwasilisha kwa Naibu Spika ambaye aliijulisha serikali kuhusu mabadiliko ya hoja na kuyafikisha kwa wabunge wote. Wabunge wengi walikuwa wanaunga mkono lakini kwa sababu maalumu baadhi waliomba wasiorodheshwe.

"Pamoja na marekebisho kwenye hoja, upande wa serikali ulitaka hoja ifutwe. Timu ya serikali iliongezewa nguvu kwa kumwongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Damian Lubuva (wakati huo). Jitihada za kutaka hoja ifutwe ziliendelea ikiwa pamoja na kukwamisha hoja kufika na kujadiliwa na wabunge," anabainisha na kuongeza:

"Upande wa serikali inaelekea walidharau uwezo wa wabunge kuisimamia hoja hii hadi mwisho."

**JARIBIO LA WAZIRI SITTA**

Licha ya kudhani hivyo juu ya uwezo wa wabunge, Sitta ambaye alikuwa kiongozi wa upande wa serikali katika majadiliano hayo, Kasaka anasema walielezwa kuwa aliishauri serikali ifanye moja kati ya mambo matatu ambayo ni kwamba;-

Kwanza, hoja ilikuwa inapingana na Kanuni za Kudumu za Bunge na kwa kuwa hoja binafsi inahitaji kibali cha Spika kujadiliwa, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais walimtaka Naibu Spika asitoe kibali, hivyo hoja itakufa.

Pili, hoja iwasilishwe kwenye mkutano wa wabunge wa CCM ambako serikali itapata muda wa kueleza hatua ambazo inachukua kutatua matatizo ya Muungano kwa wabunge. Sitta alisema kwa kufanya hivyo, wabunge wengi wataelewa hivyo hawatakuwa na haja ya kuendelea na hoja, hivyo itakuwa imekufa.

Tatu, Naibu Spika aruhusu hoja ifikishwe na kujadiliwa bungeni na kwa kufanya hivyo, serikali kwa kutumia kanuni za Kudumu za Bunge itawasilisha mabadiliko kwenye hoja ambayo yatataka hoja iondolewe au serikali ipinge hoja wakati wa mjadala na kushawishi wabunge waikatae kwa kura.

Pamoja na ushauri huo wa Sitta, Kasaka anasema kwa kujua kuwa walikuwa wanaungwa mkono na wananchi na vyombo vya habari, kundi la G55 liliendelea na msimamo wa kutaka hoja ijadiliwe na wale wanaoipinga wajulikane.

Anasema baadhi ya wabunge, wakiongozwa na wale wa G55, walisisitiza kwamba kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano lilikuwa jambo lisilokwepeka na marekebisho ya mwisho yaiwasilishwa kwa Naibu Spika Agosti 19, 1993.

"Hadi wakati huo idadi ya wabunge waliokuwa wanaunga mkono hija walikuwa zaidi ya 100 ingawa jina la kikundi cha wabunge lilibaki lile lile la G55," anabainisha.

Je, nini kiliendelea baada ya hapo? Fuatilia Jumatano ijayo upate undani wa safari ya kuelekea Hoja ya Tanganyika.

# Marafiki Rwanda, Uganda wanavyotunishiana misuli

**Na Mashaka Mgeta**

UGANDA na Rwanda ni miongoni mwa nchi tano zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), licha ya kuwa majirani, mataifa haya yalikuwa katika historia ya uhusiano mwema wa kiurafiki, lakini leo, yumkini si shwari tena, wawili hao wamo kwenye uhasama unaowakaribisha kuingia vitani.

Ni 'urafiki wa mashaka' ukijikita katika historia inayoonyesha kuwa Rais Paul Kagame wa Rwanda, amewahi kuwa mmoja wa 'nguzo' zilizofanikisha kumuingiza madarakani Rais Yoweri Museveni mwaka 1986.

Taarifa zinaeleza kuwa baada ya Rais Museveni kutwaa dola na kuiongoza Uganda, Kagame alifanya kazi kubwa kusaidia serikali yake kuendelea kukaa madarakani.

Kwa upande wake, Rais Museveni pia anatajwa kuwa mshirika wa karibu aliyeibuka baadaye na kuwasaidia wapiganaji waliongwa mkono na Kagame (kabla ya kuwa Rais) kuingia madarakani.

Kwa maana nyingine, viongozi hao wawili wenye historia ya kutokea jeshini na kupigana vita vya msituni, wanajuana kwa muda mrefu na pia kusaidiana katika harakati za kisiasa na uongozi kwenye mataifa yao.

Lakini, wawili hao wamejikuta mara kadhaa wakiwa katika ushirikiano thabiti ama mgogoro unaokua na kufikia hatua ya kuhatarisha uhusiano wa wananchi wao na hata umoja na mshikamano ndani ya EAC.

Rais Museveni ndiye aliyemkabidhi Rais Kagame 'kijiti' cha Uenyekiti wa EAC mapema mwaka huu, licha ya hatua hiyo kupingwa na Burundi ambayo pia ipo katika mgogoro wa kidiplomasia na Rwanda.

Rwanda na Uganda zilinusurika kuingia kwenye vita katika miaka ya 1990 kutokana na mapigano ya majeshi yao huko DRC yalipokuwa yanashiriki katika mapigano ya kumuondoa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, wakati huo ikijulikana kama Zaire, Mobutu Sese Seko.

Ijumaa iliyopita, Uganda iliishutumu Serikali ya Rais Kagame kwa kuzuia malori ya mizigo na magari mengine kutoka nchini humo kuingia Rwanda.

Pia serikali Kampala ikaionyooshea mkono serikali hiyo kwa kuwazuia raia wake wasivuke mpaka kuingia nchini Uganda wakati ambapo mataifa hayo jirani yanaingia kwenye mgogoro.

Utawala wa Rwanda uliyazuia malori na magari mengine kutoka Uganda kuingia nchini humo kuanzia Jumatano iliyopita, Msemaji wa Serikali ya Rais Museveni, Ofwono Opondo, aliwaambia wanahabari.

Kwa mujibu wa Opondo, malori ya mizigo yanayofikia 129 kutoka Uganda yalikuwa yamekwama kwenye mpaka wa Gutuna kwa wakati huo.



Washirika, Rais Museveni (kulia) na Kagame (kushoto) wa Uganda wakiwa pamoja kwenye majukwaa ya siasa. Wawili hao wametofautiana katika masuala mengi yanayoweza kusababisha uhasama mkubwa. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo, serikali ya Rais Kagame kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Richard Sezibera, ilikanusha shutuma hizo na kufafanua kwamba magari hayo yalielekezwa kupitia mpaka wa Kagitumba uliopo kaskazini mwa nchi hiyo ili kupisha ujenzi wa barabara yenye shughuli nyingi katika mpaka wa Gatuna.

"Walioitikia wito wa kupitia mpaka wa Kagitumba wameingia Rwanda na kuendelea na shughuli zao," anasema Sezibera.

Kwa upande mwingine, Mamalaka ya Mapato Rwanda (RRA) ilisema hatua hiyo iliyofikiwa kwenye mpaka wa Gatuna unaojulikana pia kama Katuna, ilikusudia kupisha ujenzi wa jengo la kituo kimoja cha mpakani.

Inaelezwa kuwa barua iliyoandikwa na RRA kwenda kwa Kamishna wa Forodha wa Mamlaka ya Mapato Uganda (URA) ilifafanua kuhusu hatua ya kuyahamishia magari hayo kupita kwenye mpaka mwingine.

Barua hiyo iliyosainiwa na Kamishna wa Forodha wa RRA, Rosina Uwamariya, ilisomeka:

"Tumefikiria kwa makini kupunguza msongamano na foleni za malori ili kufanikisha ujenzi wa kituo hicho cha pamoja."

Pia Sezibera anasema zuio la raia wa Rwanda kuingia Uganda kunatokana na kukakamatwa kwao kwa kuhisiwa kuwa ni mashushushu wanaokwenda kufanya shughuli za upelelezi na pia hawapatiwi huduma muhimu wanapokamatwa.

"Watu wanaingia na kutoka isipokuwa kwa raia wa Rwanda ambao wamesisitizwa wasisafiri kwenda Uganda kutokana na changamoto za kiusalama wanazokutana nazo huko," anasema Waziri wa Mambo ya Nje.

Sezibera anaongeza, "sio juu yetu (Rwanda) kulitatua hilo, bali lipo kwa upande wa Uganda. Kwa maana Waganda wanakaribishwa kwetu na hatuna matatizo kwenye upande wa mpaka wetu."

Lakini Msemaji wa Serikali ya Uganda, Opondo anasema magari ya kutoka nchini humo yaliyopitia mpaka wa Kagitumba nayo yalizuiwa kuingia Rwanda.

Serikali ya Uganda imemwandikia Balozi wa Rwanda nchini humo, Frank Mugambage, aelezee sababu za kuwapo hali hiyo.

Pia Opondo alikanusha madai ya kushikiliwa kwa raia wa Rwanda kutokana naa tuhuma za kuwa mashushushu, badala yake anasema kama wapo Wanyarwanda kwenye magereza ya nchi hiyo watakuwa wanatokana na makosa yaliyoshughulikiwa kupitia polisi na mfumo wa mahakama nchini Uganda.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa kwa takribani muongo mmoja tangu vikosi vya majeshi kupigana hadi kumwaga damu kwenye jiji la Kisangani, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Uganda na Rwanda zimekuwa katika 'urafiki wa mashaka'.

Kutokana na tukio hilo, Novemba 2001 Rais Museveni alimuandikia barua aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Maendeleo ya Kimataifa wa Uingereza, Claire Short, akieleza kuhusu kufifia kwa uhusiano kati ya nchi mbili hizo na kwamba Rwanda ilikuwa inapanga njama za kuiagusha serikali yake.

Hata hivyo, mzozo huo ulichukua sura tofauti hadi Julai 2011 ambapo Rais Museveni alifanya ziara iliyowashangaza wengi kwenda Rwanda na kutumia siku kadhaa, akiwa na timu ya wataalamu wake walioingia mikataba kadhaa ya ushirikiano kati ya nchi mbili hizo.

Kwa kiasi kikubwa, wachambuzi wa masuala ya ushirikiano wa kidiplomasia wanaielezea hali iliyopo sasa kwamba ni matunda ya uhusiano uliokuwapo zamani na kutibuka kwake.

Ukanda wa Afrika Mashariki unakabiliwa na changamoto nyingi katika kufikia ustawi endelevu na maisha bora kwa wananchi wao, hivyo kuwapo haja ya kuepuka migogoro miongoni mwa nchi wanachama na majirani.

Pia kiwango cha kutegemeana kati ya nchi na nchi ni cha hali ya juu hivyo kutokuwapo mahitaji ya kuibua migogoro miongoni mwao.

Kwa raia wa kawaida, kufifia kwa uhusiano wa kidiplomasia kati ya Uganda na Rwanda unaonekana 'kushuka' hadi kwenye ngazi za msingi katika jamii na kuathiri maisha yao.

Mmoja wa wanaojulikana kuwa miongoni mwa raia hao, Agather Atuhaire, aliandika kwenye ukurasa wake wa twitter, "uhusiano huu usiofaa kati ya Rwanda na Uganda unapaswa kukoma, familia yangu imezuiliwa kuingia Uganda kwenye harusi ya dada yetu!"

Kisha Agather anaongeza, "inakuwaje kwa mamlaka za pande mbili iwe kwa kutofahamu ama kutofahamu ukweli kwamba kuna raia wenye familia zao kwenye nchi zote mbili."

Kwa hali ilivyo sasa, ni wazi kwamba EAC inapaswa kuboresha mifumo yake ya utatuzi wa migogoro ili inapotokea hali kama ilivyo sasa kwa Rwanda na Uganda, ipate suluhu kabla ya athari zake kuwaathiri raia wa kawaida.

Hatua hiyo ni muhimu hasa kutokana na jinsi mgogoro wa Rwanda na Uganda unapoibuka wakati EAC ikitambua kwamba Rwanda bado inaendelea 'kukataliwa' na Burundi kwamba haina hadhi ya kuwa mshirika wake.

Mchambuzi wa masuala ya uhusiano wa kimataifa, Josephat Oscar, anasema kitendo cha kuifumbia macho migogoro kama unaozikabili Rwanda na Uganda kunaibua matatizo yanayowekwa kukwamisha na ikibidi kuua ushirikiano wa kikanda.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali na mwandishi wake anapatikana kupitia namba +255 754 691540 ama barua pepe; HYPERLINK "mailto:mgeta2000@yahoo.com" mgeta2000@yahoo.com.**

MAKALA

Na Sabato Kasika

# Wakuu imetosha, acheni kuwasukuma ndani raia



Waziri Selemani Jafo



Waziri Mkuchika akiwa bungeni.

BAADA ya malalamiko ya muda mrefu kuhusu utendaji wa baadhi ya wakuu wa mkoa na wilaya kuwaweka mahabusu watumishi wa umma na raia wengine kwa saa 48, hatimaye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, George Mkuchika, anaibuka na kuwaambia walalamikiwa, itoshe sasa.

Mkuchika anasema hakuna sheria inayowapa mamlaka hayo na kuwataka kuacha kutumia mabavu kwenye utendaji wa kila siku kwa kuwa wakiendelea na tabia hiyo watakuwa wanahatarisha kazi yake ya uwaziri.

Akiwa katika kikao cha bunge mwezi uliopita jijini Dodoma, anasema, wakuu wa wilaya na mikoa wanapaswa kutumia busara katika kuwaweka rumande raia wanaowaongoza.

"Msiniponze. Mimi nataka Rais Magufuli asinibadili hapa, nataka Rais aseme mzee endelea, chonde chonde tuache masuala ya umwamba, nawaomba huko mliko msiniharibie kazi yangu. Mimi ndiye mwenye cheo cha utawala bora, ndiye waziri mwenye dhamana ya utawala bora, ukiendesha mambo kinyume cha utawala bora unaniharibia kazi," anasema Mkuchika.

Aidha, anasema madaraka ya wakuu wa wilaya kuwaweka ndani watu kwa saa 24, lugha iliyotumika ni kwa usalama wake, maana yake mtu ameua mtu na jamaa zake wamekasirika wanataka kumpiga aliyeua. Hapo ndipo dhana ya kumweka mtuhumiwa rumande saa 24 inapotumika kwa usalama wake.

Mkuchika anasema mkuu wa wilaya akishamweka mtu huyo ndani ya saa 24 na muda huo ukamalizika, ikifika asubuhi ni lazima apelekwe mahakamani.

"Nataka niseme mahali popote mkuu wa wilaya kumweka mtuhumiwa au mlalamikiwa rumande kwa saa 48 ni makosa kwa sababu sheria inampa saa 24 pekee. Lakini mkuu wa mkoa amepewa saa 48," anasisitiza Mkuchika.

Anafafanua kuwa mkuu wa mkoa amepewa mamlaka ya saa 48 na akipenda anaweza kumweka mtuhumiwa mahabusi saa 24, lakini si lazima amweke mtu ndani.

"Kama ni kosa la jinai OCD au Mkuu wa Polisi wa Wilaya yupo. Iwapo ni suala la uhamiaji mtu wa uhamiaji yupo, kama amekwepa kodi ofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania yupo, si lazima utamke wewe," anaonya Mwanasiasa huyo.

**ONYO LA RAIS**

Kauli ya Mkuchika imekuja ikiwa ni siku chache tangu Rais Magufuli akemee tabia hiyo katika sherehe za kuapisha Majaji 15 wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa, jijini Dar es Salaam.

Kutokana na kuendelea kuwapo kwa malalamiko dhidi ya wateule wake, Rais ameamua kuingilia kati na kuwataka watafakari kabla ya kuchukua hatua, ambazo zimekuwa zikilalamikiwa.

"Siyo haki, viongozi wengi wamezungumza kuhusu hili na mimi narudia. Kwa sababu una mamlaka ya kuweka watu ndani sawa. Mkuu wa mkoa wako naye akiamua akaweka watu ndani itakuwa vurugu, kuna masuala mengine hayahitaji kuweka watu ndani, ni kutoa maelekezo tu," anaagiza Rais.

Rais anawataka wakuu wa wilaya kutumia vizuri madaraka yao na kwamba, si haki mtu kuwekwa ndani kwa saa 24 kisha kuachiwa bila kufikishwa mahakamani, na kuwataka kusimamia sheria na kutotumia vibaya madaraka kuweka watu mahabusu.

> "Inasababisha chuki zisizo na maana kwa kutumia vibaya sheria hiyo. Unakuta leo mkuu wa wilaya anamweka rumande mtu au mtumishi wake kwa sababu ambazo hata hazina tija"

"Wakuu wa wilaya mna sheria na mamlaka mlizopewa. Msizitumie vibaya, sheria za kuweka watu rumande mnazo, lakini msizitumie vibaya. Mtu anatupwa mahabusu halafu unamtoa, eti ameshajifunza, hujampeleka mahakamani, si haki," anaonya.

**WAZIRI JAFO**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo ni kiongozi wa kwanza, mwanzoni kuwapa angalizo wakuu wapya wa wilaya wanaosweka watu rumande.

Anawaonya kwamba kiki za ajabu za kuwakamata watu na kuwasukuma ndani saa 48 bila sababu kunaweza kupelekea watu kuichukia serikali yao

Anaonya kuwa sheria zinaruhusu, lakini ni pale ambapo jinai inatakiwa itendeke machoni pa mkuu wa wilaya, kwa kuzuia au kudhibiti jambo hilo ndipo anatakiwa atumie sheria hiyo.

Waziri huyo anaonya kwamba ni ajabu mkuu wa wilaya kusikia jambo limetokea mahali tofauti kabisa na alipo anatoa maagizo kuwa mhusika huyo weka ndani.

"Inasababisha chuki zisizo na maana kwa kutumia vibaya sheria hiyo.Unakuta leo mkuu wa wilaya anamweka rumande mtu au mtumishi wake kwa sababu ambazo hata hazina tija, eti tu kwa sababu walishagombana huko nyuma na yeye anatumia mamlaka yake kulipa kisasi," anasema Jafo.

Kwa kauli za viongozi hao ni wazi kwamba wahusika watakuwa wamejifunza kitu na kutumia nafasi zao vizuri badala ya kuendelea kusababisha malalamiko, ambayo yanaweza kusababisha wananchi wakaichukia serikali.

Ikumbukwe kuwa moja ya vitendo, ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa na watu mbalimbali na hata asasi za kiraia, ni hatua ya baadhi ya wakuu na mikoa na wilaya kuweka watu ndani katika matukio tofauti.

Kutokana na hali hiyo, mwaka juzi Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (Tucta), liliwashitaki kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, baadhi ya wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri na manispaa, wanaowaweka mahabusu wafanyakazi mbalimbali na kuwashusha vyeo wakiwamo watumishi wa umma bila sababu za msingi.

Shirikisho hilo lilitoa malalamiko hayo jijini Dodoma katika mkutano wake mkuu mbele ya Waziri Mkuu Majaliwa, na kwamba tabia ya baadhi ya viongozi inakatisha tamaa watumishi wa umma kwa kuwa wanafanya kazi kwa hofu.

Katika majibu yake, Waziri Mkuu anasema serikali ya Rais Magufuli itaendelea kuzingatia utawala wa sheria na kanuni za utawala bora, ili kuhakikisha haki za wafanyakazi nchini zinalindwa ipasavyo.

Anawaagiza viongozi wa kisiasa nchini walioko katika wizara mbalimbali, mikoani, wilayani, idara za serikali, halmashauri na taasisi zote za serikali, wazingatie utawala wa sheria kushughulikia masuala mbalimbali.





# Serikali kutunga sheria kulinda maeneo ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SERIKALI inakusudia kutunga sheria ya kilimo mwaka huu, kwa lengo la kuhifadhi na kulinda maeneo yanayolimwa ili yasibadilishwe kuwa makazi au kutumika kwa shughuli nyingine.

Waziri wa Kilimo na Ushirika, Japhet Hasunga, aliyasema hayo jana jijini Mbeya, wakati akizindua Mradi wa Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu na Viuatilifu kwa wakulima wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambao unafadhiliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani la USAID - NAFAKA kwa kushirikiana na kampuni ya kimataifa ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu na viuatilifu (CORTEVA).

Waziri Hasunga alisema kuwa tangu nchi ipate uhuru, maeneo mengi ambayo yalikuwa yakitumika kwa shughuli za kilimo yamebadilishwa kuwa maeneo ya makazi hali ambayo inadhoofisha tija kwenye sekta ya kilimo nchini.

Alisema kuwa hali hiyo inatokana na kukosekana kwa sheria inayosimamia sekta ya kilimo na hivyo kusababisha ardhi ya kilimo kukosa ulinzi wa kisheria.

**Mwaka huu tunakusudia kutunga Sheria ya Kilimo ambayo itasimamia sekta ya kilimo kuanzia kuhifadhi ardhi ya kilimo na mambo mengine yenye maslahi mapana kwenye maendeleo ya kilimo nchini.**

"Mwaka huu tunakusudia kutunga Sheria ya Kilimo ambayo itasimamia sekta ya kilimo kuanzia kuhifadhi ardhi ya kilimo na mambo mengine yenye maslahi mapana kwenye maendeleo ya kilimo nchini."

Alisema zipo sheria ambazo zinasimamia mazao mchanganyiko, lakini hakuna sheria rasmi inayosimamia sekta ya kilimo, hivyo umefika wakati wa kuanzisha sheria hiyo.

Akifafanua zaidi, Waziri Hasunga, alisema kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa kasi nchini, lakini ardhi haiongezeki hivyo kama hatua hazitachukuliwa za kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo, upo uwezekanao wa ardhi yote inayofaa kwa kilimo kubadilishwa kuwa ardhi ya makazi ndani ya miaka michache ijayo.

"Wakati taifa linapata uhuru, idadi ya watu ilikuwa chini ya milioni tisa, hadi sasa ikiwa ni baada ya Miaka 58 ya Uhuru, idadi ya watu imeongezeka na kufikia watu takribani milioni 55, lakini ardhi ni ile ile haiongezeki na badala yake ardhi ya kilimo ndiyo inabadilishwa kuwa makazi, hivyo ni lazima tuchukue hatua ya kutunga sheria ya kilimo kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo.

Alisema kuwa endapo hatua hiyo haitachukuliwa, kuna uwezekano wa taifa katika siku za usoni kupatwa na uhaba mkubwa wa chakula unaosababishwa na ukosefu wa ardhi kwa ajili ya kilimo.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi huo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Hassan Mkwawa, alisema wakulima wengi nchini hawana teknolojia za kisasa za kuhifadhi mazao yao, hivyo wanahitaji elimu na uwezeshaji kuanzia kwenye kilimo hadi kwenye kuhifadhi mazao baada ya mavuno.

Mkwawa alisema kuwa mazao mengi ya wakulima yanaharibika baada ya mavuno kutokana na teknolojia duni ya kuhifadhi mazao, hali ambayo inawasababishia wakulima hasara kubwa.

Aliwataka wadau wa kilimo kutoka ndani na nje ya nchi kujikita katika kutoa elimu na kuwasaidia wakulima kupata mbinu na teknolojia za kisasa za kuhifadhi mazao yao ili waweze kunufaika na jasho lao.

# Mashine kutambua wakwepa faini zaja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, linatarajia kufunga mashine maalum katika mikoa yote ili kutambua magari yanayodaiwa faini.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Muslimu, alitoa kauli hiyo mkoani Mbeya wakati wa kikao na askari wa usalama barabarani, ambapo alisema baadhi ya madereva na wamiliki wamekuwa wakikaidi kulipa madeni hayo.

Alisema mashine hiyo itasaidia kukabiliana na wimbi la madereva ambao wanakwepa kulipa faini za makosa ya usalama barabarani na kuongeza pato kwa taifa.

Alisisitiza kuwa madereva na wamiliki wa magari kulipa kwa wakati madeni ya faini yanayotakana na makosa ya barabarani ili kuepuka usumbufu wa kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

"Tumenunua mashine ambayo inaweza kutambua gari inayodaiwa na mashine hizo tutazigawa nchi nzima ili zifungwe kwenye njia panda na kwa kuanzia tumegawa jijini Dar es Saalam tumeona manufaa alisema," alisema.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo ya ukwepaji kulipa faini kwa wamiliki na madereva, maofisa wa jeshi wameanza kupewa mafunzo ya namna gani kutumia mashine hizo na kutoa wito wa kuhakiki magari.

Vilevile aliwasisitiza askari wa usalama barabarani kuwachukulia hatua madereva wa serikali ambao wamekuwa hawatii sheria za usalama barabarani ikiwamo mwendo kasi.

Kwa upande wake, Kamanda wa kikosi hicho Mkoa wa Mbeya, Jumanne Mkwama, alisema jeshi hilo limefanikiwa kupunguza wimbi la ajali mkoani humo kwa kuweka utaratibu wa kupitisha magari ya abiria na mizigo kwa awamu na ukaguzi kwenye sehemu za miteremko mikali kama Igawilo, Mlima Nyoka, Iwambi na Iganzo.

Alisema tangu utaratibu huo uanzishwe mwaka jana, hakuna matukio makubwa ya ajali yaliyotokea na kwamba wamekuwa wakiwachukulia hatua madereva wanaokiuka utaratibu huo ikiwa ni pamoja na kuwapokonya leseni zao.



Mwendesha guta akiwa amelisheheni mzigo katika Barabara ya Morogoro, eneo la Magomeni Mwembechai, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Mkuu wa Mkoa Chalamila akabidhi ofisi yake magari

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amekabidhi magari mawili yenye thamani ya Sh. milioni 60 ili kuongeza vitendea kazi na kurahisisha utendaji katika ofisi yake.

Magari hayo aliyakabidhi jana kwa Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Jeremiah Minja, huku akisema kuwa magari mengine saba yatakarabatiwa na wadau ili kuboresha vitendea kazi.

Akizungumza wakati akabidhi magari hayo, Chalamila alisema kuwa ofisi ya Katibu Tawala inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitendea kazi, hivyo magari yao yatasaidia kuendesha shughuli kwa ufanisi.

"Kutokana na changamoto ya vitendea kazi inayoikabili ofisi ya mkoa nimefanya jitihada za kutafuta magari ili kurahisisha utendaji kazi, lakini pia tumeongea na wadau wamesema watatengeneza magari mengine saba ambayo yatagharimu shilingi milioni 20," alisema Chalamila.

Chalamila alisema kati ya magari mawili aliyoyakabidhi kwa Katibu Tawala alipendekeza moja litolewe kwenye Idara ya Masijala ambayo inakabiliwa na changamoto kubwa ya magari kwa ajili ya kutolea huduma.

"Nawashukuru watumishi kwa utendaji kazi wenu ambao umesababisha tuongeze vitendea kazi, nimekuwa nikikabidhi magari kwenye taasisi nyingine lakini hapa sikutoa, nitaendelea kutafuta magari mengine ili kukabiliana na changamoto hii," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa ofisi yake inaendelea na mchakato wa kutafuta basi kubwa kwa ajili ya kusafirisha watumishi na kutembelea sehemu mbalimbali ikiwamo vivutio vya utalii ikiwa ni sehemu ya kujifunza na kujenga mshikamano.

Akipokea magari hayo, Katibu Tawala Jeremiah Minja, aliahidi magari hayo kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuyatunza ili yaendelee kurahisisha shughuli za kuwaletea maendeleo wananchi.

Mmoja wa watumishi Mrisho Rashid, alisema magari hayo yatasaidia kwenye utendaji kazi ambao unakabiliwa na changamoto ikiwamo hali ya hewa kama vile mvua ambayo inasababisha shughuli kusimama.





# Wanafunzi wajitosa ujenzi wa viwanda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAFUNZI wabunifu wameishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuwakusanya pamoja ili kutengeneza hoja bunifu zitakazoweza kuisaidia kufikia uchumi wa viwanda.

Ushauri huo waliutoa jana jijini hapa walipokuwa wakizungumza na gazeti hili katika mashindano ya ubunifu katika sayansi na teknolojia yaliyoambatana na utoaji tuzo kwa washindi.

Mashindano hayo yameandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo yalianza jana na kilele chake kitakuwa Machi 7, mwaka huu.

Mmoja wa wanafunzi hao ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Feza, Erick Alex Erick, alisema yeye amebuni teknolojia ambayo itaweza kutumika kuzalisha maji safi na umeme.

**Tunatambua nchi yetu inataka kufikia uchumi wa viwanda wito wangu kwa serikali itukusanye wanafunzi sisi wenye bunifu zetu mbalimbali za kusaidia kufikia azima hiyo.**

Alisema kutokana kwa sasa serikali kujenga mradi wa kuzalisha umeme wa Stigler's Gorge, inaweza kutumia teknolojia hiyo ambayo itaweza kuzalisha umeme na maji safi.

"Tunatambua nchi yetu inataka kufikia uchumi wa viwanda wito wangu kwa serikali itukusanye wanafunzi sisi wenye bunifu zetu mbalimbali za kusaidia kufikia azima hiyo," alisema.

Naye mwanafunzi wa kidato cha sita kutoka Shule ya Sekondari Same, Furaha Mgaya, aliishukuru serikali kwa kuwashindanisha wabunifu kuonyesha teknolojia zao ambapo itawasaidia kubuni vitu vikubwa vya kusaidia kufikia azima hiyo.

"Naomba tu kama serikali itaweza kutafuta hata wafadhili na kutukusanya sisi wanafunzi wenye ubunifu kutengeneza teknolojia mbalimbali, itasaidia nchi yetu kuwa na teknolojia za kipekee na mataifa mengine yataweza kuiga," alisema.

Mgaya alisema kutokana na changamoto zilizopo za msongamano wa magari kwenye miji mikubwa, aliamua kubuni mfumo wa kuruhusu magari katika muungan iko wa barabara ambao utasaidia askari wa usalama barabarani kutosimama kuongoza magari.

Kwa upande wake, mwanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Kondo, Maleo Lameck, ambaye amebuni mashine ya kutoa taulo za kike vyooni utakaosaidia wanafunzi wa kike waweze kuhudhuria masomo yao ipasavyo.

"Mashine hii itawekwa chooni na mwanafunzi atapata taulo yake kwa kuweka Sh. 200 tu, niliona nitengeneze ili kusaidia wanafunzi wa kike kupata taulo hizo kwa bei rahisi kutokana na wengine huwa hawana uwezo wa kununua kwa Sh.2000," alisema.

Aliiomba serikali kumsaidia ili aweze kutengeneza mashine hizo kwa wingi kusaidia wanafunzi wenzake shuleni.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Seleman Jafo, akijaribu kurusha tofali chini ili kulipima uimara wake wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chamwino katika Kijiji cha Mlowa barabarani, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jafo ataka kasi ujenzi wa hospitali ya Chamwino

**Na Ibrahim Joseph,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameonyesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Chamwino na kuagiza uongozi wa wilaya hiyo kuhakikisha unakamilika kwa muda uliopangwa.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika kijiji cha Mlowa Barabarani wilayani humo alipofika baada ya kukagua ujenzi huo.

Jafo alisema hajaridhishwa na kasi ya ujenzi wa hospitali hiyo na kuwataka uongozi na mkandarasi kuongeza kasi ili kukamilisha kwa wakati uliowekwa.

"Sijaridhishwa na kasi ya ujenzi wa hospitali hii, naomba muongeze, fanyeni haraka kuagiza vifaa vya ujenzi ili kukamilisha kwa wakati tulioweka," alisema.

Alisema fedha za ujenzi wa hospitali hiyo zimetolewa na serikali ili kuweza kuwahudumia wananchi wake.

Aliwataka makandarasi wanaotekeleza ujenzi wa hospitali hiyo kujenga majengo yote kwa wakati na kulingana na thamani ya fedha zilizotolewa na serikali.

Waziri Jafo aliwashukuru wananchi wa Kijiji cha Mlowa Barabarani kwa kukubali kutoa ardhi ya eneo lenye ukubwa wa ekari 24 kwa ajili ya ujenzi huo wa hospitali.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga, alisema ujenzi wa miundombinu ya hospitali hiyo ulianza rasmi Januari 22, mwaka huu na mradi unatarajiwa kutumia gharama ya Sh. bilioni 1.5 zilizotolewa na serikali. Nyamoga alisema awali hospitali hiyo ilitakiwa kujengwa eneo la Chamwino Ikulu, lakini baada ya serikali kutoa fedha za ujenzi wa Hospitali ya Uhuru ilibidi wapendekeze kujengwa katika Kijiji cha Mlowa Barabarani ili kusogeza huduma kwa wakazi wa ukanda wa barabara kuu ya Dodoma hadi Iringa.

Alisema katika ujenzi huo wananchi wa kijiji hicho wameshiriki ujenzi huo kwa kutoa nguvu zao ikiwa sawa na thamani ya Sh. milioni 1.6.

# Waiomba serikali kupunguza gharama za matibabu

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za matibabu ya kibingwa ili wananchi wa hali ya chini waweze kumudu.

Rai hiyo ilitolewa jana na baadhi ya wananchi jijini Dodoma, baada ya hivi karibuni Hospitali ya Benjamin Mkapa kuzindua mtambo maalum wa uchunguzi wa magonjwa ya moyo na uzibuaji wa mishipa ya moyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi hao walisema kitendo cha serikali kuanzisha huduma hiyo kitasaidia jamii kwa kuwa wagonjwa wa moyo wamesogezewa karibu huduma hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, Jamila Haruna, alisema licha ya kuwapo kwa mtambo huo inawezekana huduma hiyo wananchi wasio na uwezo wasiweze kumudu gharama zake.

"Vifo vingi vinatokea hasa kwa wananchi wa vijijini kutokana na kutokuwa na fedha za kugharamia matbabu kwa kuwa matibabu ya ugojwa wa moyo yanagharimu fedha nyingi," alisema.

Naye Hellen Amos, aliomba huduma hiyo irahisishwe na ikiwezekana isogezwe hata katika vituo vya afya, ili kukidhi mahitaji ya wananchi walio wengi ambao hawana uwezo wa kusafiri umbali mrefu.

"Maisha ni magumu, watu wa vijijini ndio wanaoteseka na magonjwa ya moyo kwa kuwa wengine bado hawana elimu ya kutosha juu ya ugojwa huu," alisema.

Katika uzinduzi huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainab Chaula, alisema lengo la serikali ni kuona watu wake wanapata huduma bora za afya na zinazokidhi mahitaji.

Alisema maendeleo nchini yanaletwa na watu wenye afya bora na serikali inatambua kuwa huduma ya matibabu ya kibingwa inagharimu fedha nyingi, hivyo ili kila Mtanzania afikiwe na huduma hiyo sharti kujiunga na mfuko wa bima ya afya.

Alibainisha kuwa huduma hizo ni gharama, hivyo ili Watanzania wasio na uwezo kifedha wapate huduma ni muhimu kujiunga na mifuko ya bima ya afya.





# Asasi za kiraia zazindua sheria maalum zitakazowa-ongoza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), kwa kushirikiana na asasi za kiraia Zanzibar wamezindua sheria maalum zinazosimamia utendaji kazi wa asasi za kiraia Zanzibar.

Sheria hizo zina lengo la kusimamia utendaji wa kazi wa asasi za kiraia Zanzibar, ambapo uzinduzi ulifanyika Mjini Unguja.

Akizungumza katika uzinduzi huo Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, alisema asasi za kiraia nchini zinamchango mkubwa wa kuleta Maendeleo, hivyo kuwapo kwa sheria zinazowaongoza asasi hizo, zitasaidia katika kuleta ufanisi wa kazi kwa asasi hizo.

Alisema sheria hizo zitasababisha wana asasi kupata mwongozo ambao utawasaidia katika utendaji wa kazi zao za kila siku na kuondoa mgongano unaoweza kujitokeza.

"Uwepo wa sheria hizi umekuja kupunguza mvutano wa maslahi baina yenu wana asasi za kiraia, hivyo naamini kila mmoja atafanya juhudi ya kufahamu sheria hizi na hatutegemea kupokea kesi mahakamani kutoka kwenu," alisema Jaji Mkuu wa Zanzibar.

Aidha, alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaoletwa na asasi za kiraia katika maendeleo nchini hivyo ipo haja ya wana asasi mbalimbali za kiraia kuzifahamu sheria zinazowaongoza ili kufanya kwa mujibu wa sheria na ukiukaji wa sheria.

Jaji Makungu alitoa wito kwa asasi za kiraia kufanya kazi kwa kuibua matatizo mbali mbali yanayowakabili wananchi na kutojiingiza katika matatizo ya kisheria.

Aidha, amekiri kuwapo kwa upungufu kwa baadhi ya sheria zilizoko ambapo aliwataka kutoa maoni juu ya sheria ambazo zitakazo onyekana kuwa na upungufu kwa lengo la kufanyiwa marekebisho.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji Mshibe Ali Bakari, aliwaambia wanaharakati hao kwamba wapo tayari kuzifanyia kazi sheria zote zenye upungufu.

"Tume ya kurekebisha sheria itasikiliza maoni yenu juu ya sheria ambazo zinaupungufu na kuzifanyia kazi kwa lengo la kuleta maendeleo na mabadiliko chanya nchini," alisema Jaji Mshibe.

Aidha, Jaji Mshibe, alisema kuwa serikali inathamini juhudi zinazofanywa na asasi za kiraia katika kupigania haki za wananchi ambao hawana uwelewa wa sheria.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema uwepo wa sheria hizo ni muongozo bora kwa asasi za kiraia nchini.

Alisema wana asasi za kiraia wanatakiwa kuzifuta katika ufanyaji kazi wa taasisi zao pia ni mwongozo huo utatumika katika utetezi.

"Tunatakiwa tuzisome sheria hizi na tuzizingatie ili iwe utetezi katika ufanyaji kazi wa asasi zetu," alisema Onesmo Olengurumwa.

# Jamii yatakiwa kufuatilia nyendo za watoto wao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya Milele Foundation imeitaka jamii kuongeza bidii na kufuatilia nyendo za watoto ili kuhakikisha wanafaulu katika mitihani yao hadi elimu ya juu.

Hayo yalisemwa na mratibu wa taasisi hiyo, Abdalla Said Abdalla, wakati akishiriki katika zoezi la ugawaji wa vitabu 37,000 vya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la nne.

Alisema taasisi hiyo imechukua jukumu la kuchapisha vitabu hivyo baada ya kubainika kuwapo kwa mahitaji kwa wanafunzi wa shule za msingi katika kuimarisha masomo ya lugha.

"Vitabu hivi vimechapishwa na taasisi yetu kwa ajili ya kuona wanafunzi wanapata msingi mzuri wa lugha kwa ajili ya ufaulu wa baadaye," alisema.

**Vitabu hivi vimekuja wakati mwafaka ambapo sisi Tawala za Mikoa tunakabiliwa na uhaba wa vitabu kwa ajili ya shule za msingi ziliopo Pemba.**

Juma Faki Mtumweni ambaye ni ofisa kutoka Wizara ya Nchi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa aliipongeza taasisi ya Milele kwa juhudi zake za kuchapisha vitabu hivyo ambavyo vitatumika kwa wanafunzi wanaosoma elimu ya msingi.

"Vitabu hivi vimekuja wakati mwafaka ambapo sisi Tawala za Mikoa tunakabiliwa na uhaba wa vitabu kwa ajili ya shule za msingi ziliopo Pemba," alisema.

Aidha, Ofisa Elimu Wilaya ya Micheweni Pemba, Raya Khamis Hamad, alisema wamevipokea vitabu hivyo ambavyo wamepanga kuvisambaza katika kila shule za msingi ziliopo katika Wilaya ya Micheweni Pemba.

"Vitabu 8,929 tumepanga kuvisambaza katika shule kumi ziliopo Wilaya ya Micheweni Pemba ambazo zilikuwa zikikabiliwa na uhaba wa vitabu vya lugha ya Kiingereza," alisema.

Aidha, vitabu vingine vitasambazwa katika mikoa miwili ya Pemba pamoja na wilaya zake kwa ajili ya shule za msingi.

Vitabu vya lugha ya Kiingereza vimelengwa kusambazwa kwa wanafunzi wa shule za msingi ambazo zipo katika mpango wa ugatuzi katika sekta ya elimu.

Milele Foundation ni taasisi iliyoanzishwa miaka mitano iliyopita ambayo imejikita zaidi katika kufanya kazi za kuelimisha jamii ikiwamo elimu na masuala ya afya pamoja na kuwakuza wajasiriamali.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, juzi aliwaapisha mawaziri, naibu waziri, makatibu wakuu na manaibu katibu wakuu, Ikulu mjini Zanzibar. Pichani akimwapisha Mohamed Ramia Abdiwawa kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. **PICHA: KABEMBA MARTIN**

# UWT wamwaga sifa kwa Rais Shein

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake Zanzibar wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) umempongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuonyesha upendo kwa jamii ya wanawake kwa kuwapa nafasi za juu za uongozi.

Hayo yalisemwa na Makamu Mwenyekiti wa UWT taifa, Thuwaiba Edikton Kisasi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea Siku ya Wanawake Duniani Machi 8.

Kisasi alisema wanawake wamepata nafasi kubwa za uongozi katika ngazi za maamuzi ikiwamo uwaziri, makatibu wakuu pamoja na mahakimu.

Alisema nafasi walizochaguliwa wanawake na Rais Shein ni za juu za maamuzi ambazo zimeonyesha uwezo mkubwa wa jamii hiyo katika kuongoza.

Kwa mfano alisema katika Baraza la Mawaziri la Rais Shein wapo jumla ya mawaziri watano ambao wameshika wizara nyeti na kuonyesha kupata mafanikio makubwa siku hadi siku.

"Wakati wanawake tukielekea katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Rais Shein kwa kuonyesha mapenzi makubwa kwa jamii ya wanawake ikiwamo kuchagua mawaziri watano katika baraza lake la mawaziri," alisema.

Aidha, alisema katika ngazi za maamuzi, hivi sasa wapo mahakimu wengi wanawake pamoja na majaji, hatua ambayo inaonyesha Rais kutekeleza usawa wa kijinsia kikamilifu.

Naibu Katibu Mkuu Jumuiya ya Wanawake Zanzibar, Tunu Kondo, alisema jumuiya imejipanga vizuri kuhakikisha vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vinatokomezwa moja kwa moja.

Aliitaka jamii kuhakikisha kwamba inakuwa tayari kutoa ushahidi mbele ya vyombo vya sheria kwa ajili ya kuwatia hatiani watuhumiwa.

"Umoja wa Wanawake (UWT) umejipanga kikamilifu kuhakikisha kwamba vitendo vya udhalilishaji vinadhibitiwa lakini watu wawe tayari kutoa ushahidi mbele ya vyombo vya sheria," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

# Mgonjwa wa pili wa Ukimwi aondolewa virusi

**LONDON,** Uingereza

JOPO la wanasayansi limetangaza kumwondolea virusi mwathirika wa virusi vya Ukimwi (VVU) kwa kutumia tiba ya uboho kutoka kwa mtu ambaye hajaathirika na virusi hivyo.

Tukio hili ni la pili lililoonyesha mafanikio baada ya lile la kwanza lililotokea mwaka 2007.

Madaktari wametumia njia ya kupandikiza uboho ili kuviondoa virusi vya Ukimwi kwa mwathirika mmoja wa virusi hivyo vinavyosababishwa Ukimwi.

Kiongozi wa jopo la utafiti huo, Ravindra Gupta, alinukuliwa akisema; "Kufikiwa kwa hatua hii kunaonyesha ahueni kwa mgonjwa huyu wa pili na kulitokana na mbinu ileile iliyotumiwa awali, kutokana na mgonjwa wa kwanza wa Berlin kutoonyesha shida yoyote."

Katika visa vyote viwili, wagonjwa walipandikizwa uboho kutoka kwa watu waliokuwa na uwezo wa kuhimili VVU.

Gupta alisema kubadilisha chembe hai za mwathirika na watu hao kumeonekana kumwezesha mgonjwa kuzuia virusi vya Ukimwi kurejea baada ya matibabu.

Kwa mujibu wa Gupta, mgonjwa wa London aligunduliwa na VVU mwaka 2003 na amekuwa katika tiba ya kudhoofisha makali ya virusi vya Ukimwi tangu mwaka 2012.

Ingawa watafiti hao wanasifu matokeo ya utafiti huo, lakini wanaonya kwamba ni mapema mno kumthibitishia kwamba amepona.

Watafiti hao wametangaza kuwa mtu huyo aliyekuwa ameambukizwa virusi vya Ukimwi sasa yuko katika hali nzuri.

Huyo ni mwathirika wa pili wa VVU kufanyiwa matibabu kama haya, aliyepachikwa jina "mgonjwa wa London," ambaye amefanikiwa kuondolewa virusi hivyo vilivyowaathiri takribani watu milioni 37 duniani.

Mgonjwa huyo, aliomba timu yake ya matibabu kuficha utambulisho wake.

Matibabu na matokeo yalichapishwa katika jarida la kisanyansi la kimataifa la "Nature" na yanatarajiwa kutangazwa rasmi katika mkutano wa masuala ya tiba utakaofanyika huko Seattle, Marekani, jana.

Wanasayansi walitumia njia ile ile ambayo ilitumiwa na kuonyesha mafanikio kwa mgonjwa wa VVU mjini Berlin, Ujerumani mwaka 2007.

Tiba hiyo hudhoofisha tu virusi hivyo na si kuviondoa. Alifanikiwa kupandikizwa uboho mnamo mwaka 2016, lakini akiendelea kutumia tiba kwa muda wa miezi 16 kabla ya kuacha matibabu hayo. Na tangu hapo, hajaonyesha dalili yoyote za kuwa na virusi kwa miezi 19 sasa.

Gupta amesema hawajaona virusi hata baada ya kumpima ila ameonya kuwa ni mapema mno kusema kwamba amepona.

**DW**




Charles Sirleaf (katikati) anaendelea kushikiliwa nchini Liberia, baada ya kushutumiwa uhujumu uchumi.

# Mtoto wa Rais mstaafu Liberia ashtakiwa uhujumu uchumi

**MONROVIA,** Liberia

MTOTO wa aliyekuwa Rais wa Liberia Ellen Sirleaf, Charles Sirleaf, ameshtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi uliohusisha vitendo vya uchapishaji wa fedha wa mamilioni ya dola kinyume cha sheria.

Charles anashukiwa kufanya vitendo hivyo alipokuwa Gavana wa Benki Kuu mwaka 2016 hadi 2018.

Taarifa zinaeleza kuwa maofisa wengine wa zamani wanne wa benki wameshtakiwa pia.

Hata hivyo, taarifa zinaeleza kuwa watuhumiwa hao mpaka sasa hawajasema lolote kuhusu tuhuma dhidi yao.

Ripoti kuhusu mamilioni ya fedha yaliyopotea ilitolewa wiki iliyopita.

Liberia ni moja kati ya nchi maskini ambayo imekuwa ikijinasua kwenye vitendo vya rushwa vilivyokithiri.

Rais mstaafu wa taifa hilo, Sirleaf tangu mwaka 2006 mpaka 2018, alisifika kwa kuinua uchumi baada ya miaka kadhaa ya mzozo nchini humo.

Siku ya Jumatatu, Charles, Mkuu wa zamani wa benki ya Milton Weeks na ofisa mwingine wa benki, Dorbor Hagba, walishtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya fedha za umma na kupanga njama za uhalifu.

Jaji wa mjini Monrovia, aliamuru wawekwe gerezani wakisubiri kusomewa mashtaka.

Wanasheria wa watuhumiwa hawajazungumza lolote kuhusu shutuma dhidi ya wateja wao. **BBC**

# Marufuku polisi kubeba silaha vilabu vya pombe

**BUJUMBURA,** Burundi

POLISI nchini Burundi imepiga marufuku askari wake kubeba silaha na kuvaa sare za polisi wakati wanapokwenda kwenye vilabu vya pombe au mahali pengine popote kunakouzwa vileo.

Kwa mujibu wa waraka uliosainiwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Polisi nchini humo, Jeshi la Polisi nchini humo limechukua hatua hiyo baada ya watu wanne kuuawa kwa bunduki.

Waraka huo ulieleza kuwa watu hao waliuawa katika kitongoji cha Gatumba yapata kilomita 15 Magharibi mwa mji mkuu, Bujumbura na polisi waliokuwa wamelewa mwishoni mwa wiki.

Amri hiyo ilitolewa na maofisa nchini humo kwa polisi kuhakikisha kutokuwa na silaha au kuvalia sare za polisi ambao hawako kazini.

"Hakuna ofisa wa polisi anayeruhusiwa kubeba guruneti, vinginevyo atahesabiwa kama mhalifu, ofisa yeyote wa polisi atakayekwenda kwenye baa na silaha lazima ataadhibiwa kikamilifu," ulieleza waraka huo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, miongoni mwa watu waliouawa, alikuwa ni ofisa wa polisi wa eneo hilo.

"Ni marufuku pia kwa polisi kubeba gurunadi na kilipuzi cha aina yoyote ile. Pia polisi hawaruhusiwi kwenda likizo na silaha," ulisema waraka huo.

Tangu kuibuka kwa mzozo mwaka 2015, polisi walikwenda vilabuni na silaha hata wakati wa likizo ili kujihakikisha usalama wao, lakini kwa sasa matukio ya polisi kuwaua raia yanaonekana kuongezeka.

Mwezi uliopita, polisi alimfyatulia risasi mwendesha baiskeli mjini Bujumbura, ambaye alikufa uwanjani.

**BBC**

# Rwanda yakanusha kufunga mpaka baina yake na Uganda

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda imekanusha ripoti ya kuwa imefunga mpaka kati yake na Uganda.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda, Richard Sezibera, aliyasema hayo jana katika mkutano wake na waandishi wa habari katika makao makuu ya wizara hiyo, mjini Kigali.

"Shughuli ya ujenzi wa barabara katika mji wa mpakani wa Gatuna umefanya magari kuelekezwa katika mpaka wa Kagitumba," alisema.

Kuhusiana na uhusiano wa mataifa hayo mawili alisema: "Uhusiano wetu kwa sasa sio mzuri vile, lakini tunashughulika hilo."

Sezibera aliongeza kuwa Rwanda inaendelea na majadiliano na majirani zake kuhusiana na masuala kadhaa ikiwa ni pamoja na kuzuiliwa kiharamu kwa raia wake nchini Uganda.

Alisema kuwa suala la kuunga mkono makundi yaliyojihami yanayoipinga Rwanda pia ni baadhi ya mambo yanayojadiliwa.

Waziri Sezibera pia amekanusha ripoti ya vyombo vya habari kuwa taifa hilo limepeleka vikosi maalum vya kijeshi katika mpaka wake na Uganda tangu ilipochukua hatua ya kufunga.

Alhamisi iliyopita mamlaka ya mapato ya Rwanda iliamrisha maroli ya mizigo kutotumia tena mpaka wa Gatuna kwa madai ya shughuli za ujenzi wa kituo kimoja cha mpakani 'one stop border' baina yake na Uganda.

**BBC**

# Mawaziri wajifungia saa 10 kutafuta suluhu

**Na Mary Mosha,** HAI

WAZIRI wa Fedha, Dk. Philip Mpango na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angela Kairuki, jana walijifungia kwa zaidi ya saa 10 kutafuta suluhu ya mgogoro unaofukuta, kati ya wawekezaji wa kigeni na serikali Wilaya ya Hai.

Kwa mujibu wa Waziri Mpango, Januari 9, mwaka huu, alipokea barua ya maelekezo kutoka kwa Rais Dk. John Magufuli ikimwelekeza kuwaita wawekezaji hao na kusikiliza madai yao.

Kutokana na maelekezo hayo, Waziri Mpango na Waziri Kairuki wametua rasmi kuanza kazi ya kutafuta muafaka wa kudumu.

"Barua ilikuwa imeandikwa na mwekezaji (hakumtaja jina) kwenda kwa Rais (Magufuli) ikiwa na malalamiko yaliyogawanyika katika makundi sita.

"Moja ni kutakiwa kulipa shilingi milioni 713 ndani ya siku saba, kufungiwa kwa akaunti zao za 'Kuza Afrika' na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)."

Wawekezaji hao wanadaiwa kuwekeza katika mikoa ya Mbeya na Kilimanjaro.

Wawekezaji walioitwa katika kikao hicho, yumo mwakilishi wa mwekezaji raia wa Ujerumani, James Powell, Robert Olewes ambaye ni Mkurugenzi wa Kuza Africa Ltd., na wakili maarufu Boniface Mwabukusi.

Akizungumza kabla ya kuanza kwa kikao hicho, Waziri Mpango alisema wawekezaji hao wanadai kunyimwa kuendeleza mashamba ya Kibo na Kikavu kabla ya mkataba kusainiwa.

Waziri Mpango alisema wawekezaji hao wamemweleza Rais kuwa mazingira ya uwekezaji ni magumu na hawawezi kuwaalika wawekezaji wengine.

Aidha, Waziri Mpango alisema mwanasheria wao kuwekwa mahabusu kwa saa 48 bila kufuata taratibu pamoja na mkurugenzi wao kuwekwa mahabusu kwa saa 48 kwa amri ya Mkuu wa Wilaya.




Mkurugenzi wa Mafunzo na Ufundi Stadi (TVET), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Noel Mbonde, akifungua mafunzo ya siku tano kwa wadau wa elimu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jambazi ajisalimisha polisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

EMANUEL Mwakilili, mkazi wa Dodoma aliyedai anajihusisha na vitendo vya uhalifu ukiwamo ujambazi, amejisalimisha kwa Jeshi la Polisi mkoani Dodoma na kutangaza kuachana na vitendo hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alidai Mwakilili alikuwa akijihusisha na matukio ya uhalifu, lakini sasa ametangaza kuwa raia mwema.

"Niwatake na wale wengine ambao wanajihusisha katika matukio ya aina hiyo, wajisalimishe, wasisubiri tuwakamate,"alisema.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muroto alisema jeshi hilo limekamata lori la wizi lenye namba za usaji T 519 CPB na trela lenye namba za usajili T 544 CBF likiwa na shehena ya mahindi magunia 200.

Muroto alisema gari hilo linadaiwa kufanya matukio ya wizi zaidi ya manane katika maeneo mbalimbali nchini.

"Lori hilo liliibwa Oktoba 26, 2018, likiwa na mzigo wake uliokuwa ukisafirishwa kwenda DRC likiwa na namba za usajili T 506 BXD/ T 619 CVZ aina ya Iveco," alidai.

Kamanda Muroto alidai kuwa baada ya gari hilo kuibwa, kesi ilifunguliwa Kijitonyama jijini Dar es Salaam na katika ufuatiliaji wa awali, ilibainika kuwa gari lenye namba ambazo lori hilo lilikutwa nayo, liko jijini Dar es Salaam na ni mali ya Kampuni ya Shaimark Co. Ltd.

"Ufuatilia pia ulibaini gari hilo limekuwa likibadilishwa namba mara kwa mara, hivyo kufanikiwa kuiba mali za watu katika maeneo tofauti," alisema.

"Waliiba chumvi iliyokuwa ikisafirishwa kwenda Lindi na Mpanda, waliiba shehena ya mahindi Singida, waliiba shehena ya mbaazi Kongwa, Dodoma, waliiba mbao Mbeya, lakini pia waliiba mahindi ya serikali (DFP) Makambako mkoani Njombe," Muroto alisema.

Muroto aliwataja watuhumiwa waliokamatwa katika tukio hilo kuwa ni Emmanuel Kitinye (42), mkazi wa Ubungo Kibangu ambaye anadaiwa kukamatwa na leseni mbili, moja ikiwa na jina lake na nyingine ina jina la Michael Ngoh, pamoja na Idrissa Nassoro (35), mkazi wa Ubungo jijini Dar es Salaam.

Kamanda Muroto pia alisema wamekamata magari mawili ya wizi aina ya prado yanayodaiwa kuibwa Dar es Salaam yakiwa yamehifadhi kwenye nyumba ya kulala wageni jijini hapa wakati wezi wakisaka wateja.

Alitaja magari yaliyokamatwa kuwa ni Prado isiyo na namba ya usajili yenye RZJ120-0012931 na ya pili ni T 777 CVN lakini ilikuwa na namba za chassis RZJ 120-0010946, yote yana rangi ya fedha.

Hata hivyo, Kamanda Muroto alisema watuhumiwa wawili walitoroka kwa kuruka ukuta wa nyumba ya kulala wageni walikokuwa wamefikia, lakini wamefanikiwa kupata majina na picha zao huku akiwataka wajisalimishe.

# Mama wa kichanga atoa yake ya moyoni

**Na Beatrice Moses**

AMINA Nunga (17), mama mzazi wa mtoto mchanga Shazina Yahya aliyeibwa katika Kijiji cha Likalangiro, Songea mkoani Ruvuma, ameelezea adha aliyoipata kutokana na tukio hilo.

Akizungumza na Nipashe juzi kwa njia ya simu, Amina alisema alijifungua mtoto huyo Septemba 19, mwaka jana kisha akaruhusiwa kuondoka na mwanawe huyo Septemba 25 lakini saa 6 usiku baada ya kuamka kutoka usingizini ili kumnyonyesha, alistaajabu kutomwona kitandani hapo.

Alisema huyo ni mwanawe wa kwanza, hivyo alijikuta katika wakati mgumu kwa kuwa alikuwa anajiuliza maswali kama amechukuliwa vipi kama yu hai au ameuawa.

"Tuliamsha majirani kutusaidia, tukatafuta bila mafanikio ndipo tukatoa taarifa polisi. Walifanya juhudi za kumtafuta, hatimaye baada ya miezi kadhaa tukajulishwa kuwa amepatikana mkoani Kilimanjaro," alisema.

Mama huyo huku akilishukuru Jeshi la Polisi kwa kufanikisha kumpata mwanawe, alisema baada ya kujulishwa taarifa za kupatikana kwake, alipelekwa Songea kumtambua.

Alisema pamoja na kupatikana, bado hajakabidhiwa mtoto huyo na bado yuko mikononi mwa maofisa wa ustawi wa jamii na kwamba amejulishwa kuwa kuna masuala ya uchunguzi yanakamilishwa ndipo akabidhiwe.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Gemini Mushy, alisema polisi wamemkabidhi mtoto huyo ustawi wa jamii, baada ya kupatikana Februari 18 katika Kijiji cha Kokirie, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Alisema mtoto huto ambaye sasa ana miezi mitano, inaaminika kuwa aliuzwa kwa Sh 30,000.

Awali, Kamanda Mushy alimtaja mtuhumiwa aliyehusika kumwiba mtoto kisha kwenda kumuuza kuwa ni Abrahamu Kilewa (20) mkazi wa kijiji cha Mahanje katika Halmashauri ya Madaba.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kumuuza mtoto huyo kwa Anonsiata Luambano (36) mkazi wa Marangu Moshi, mfanyabiashara ambaye inadaiwa kuwa uzazi wake ni mgumu kwa kuwa ana mtoto mmoja ambaye ana miaka 10.

Kamanda alimtaja askari aliyehusika na upelelezi huo kuwa ni Koplo Victor ambaye alijituma kwa kujitolea uhai wake kwenda kumwokoa mtoto.

Babu wa kichanga huyo, Abdallah Nunga, naye alielezea furaha yake ya kupatikana kwa mjukuu wake.

"Kwa sasa nipo msibani siwezi kuongea mengi ila nashukuru polisi walivyoangaika na kuonyesha juhudi kubwa ambazo zimewezesha mjukuu wangu kupatikana,"alisema Nunga.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kiwanja kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani,eneo la Sanzale "B" lenye Sq.meters 3920 linauzwa. Eneo hilo limepimwa na lina hati ya umiliki. Linafaa kwa shughuli za kibiashara, kujenga kituo cha kuuzia mafuta nk. Kwa maelezo zaidi piga simu Na.0715 263 683/0784 263 683.

**ENEO LINAUZWA,** NAUZA ENEO LIKO MPIJI MAGOE YANAPOGEUKIA MAGARI YA KUTOKA MBEZI NI UNATEMBEA MITA 200 HADI KWENYE ENEO UKUBWA NI MITA 20@40. BEI NI NAFUU KABISA SIMU NAMBA: 0621 607825.

## MAGARI/VIPULI

**LEYLAND DAF ZINAUZWA**, DAF TANKI YA MAJI LITA 10,000, DIESEL CC 5880. DAF PICK UP DIESEL CC 4200 TANI 4.5. MAGARI YAPO KWENYE HALI NZURI ZOTE ZINATEMBEA. MAWASILIANO: 0657 370655 DAR ES SALAAM.

## MCHANGANYIKO

**PATA RAMANI ZA MAJENGO MBAL**imbali kama vile ramani za nyumba,shule na kadhalika.Mawasiliano;0744113969


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE


## CHETI KIMEPOTEA



**SAADA KASIMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0351-0645** kilichotolewa na BAGAMOYO SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1355/2019.**

115096902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EMMANUEL PROSPER TEMU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 466 DGX FORTUNER**.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**CID/TR/RB/701/2019.**

115096302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**YAH: SHAURI LA MADAI NA. 89/2010**
**MDAI............PUNUNTA'S COMPANY LTD**
**DHIDI YA**
**MDAIWA.....................ENOCK NKONOKI**

Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 22/03/2019 saa 2:00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani.

Endapo hutafika Mahakamani shauri litasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

215094902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi **No;53/2019**
Ombi la **MARIA ISSAYA DAUDI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SESILIA AGUSTINO SHAURI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/03/2019

115093602

**IN THE DISTRICT COURT OF NYAMAGANA**
**AT MWANZA**
**CIVIL APPEAL 54 OF 2018**
**JITELEJA MASHISHANGA LUZALIA APPELLANT**

**VERSUS**

**FELISTA ISDORY RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fixed for hearing/ mention on the 07 day of MARCH 2019 at 08:30 a.m in the forenoon.

**YOUR ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the document upon which you intend to rely in support of your case.

**GIVEN UNDER** my hand and the seal of the court

This 1 day of MARCH 2019.

215095502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SARATI ABDI ISSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina ya LITEACE yennye namba za usajili T769 DGR chesis na. YM550015433 engen na.2Y0743218.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi
**URM/TR/RA/4000/2018**

215094502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Mhina Abdallah** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba ya usajili MC 695 BYJ aina ya BOXER yenye chasis namba **MD2BISBYDJWM88767** na engine namba JVZWJM19137.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KMR/B.I/VOL VIII517**

115095002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 05/03/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamis tarehe 7/3/2019 kampuni ya M.M Corporate Ltd itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Mlandizi kuelekea Dar es salaam gari hilo lenye namba za usajili:

   **T898 APY Horse/T 933 AFZ Trailer.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 3.50**
   **Kimo - mita 4.80**
3. NJia itakayotumika Mlandizi hadi Dar kupitia Morogoro Road gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa **12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

115094702

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF TANZANIA**
**AT ARUSHA**
**TAX.CAUSE CFIVIL/CASE NO 18 FOR 2018**
**ZAKARIA MBATA PLAINTIFF/APPELLANT**
**VERSUS**
**REVIVAL CHURCH SACCOS LIMITED**

**NOTICE OF MENTION**

**TO ZAKARIA MBATA OF ARUSHA**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing in the Resident Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the 25 day of MARCH 2019 at 08:30am o'clock in the forenoon.
You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE** .That in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this 04 day of MARCH 2019.

215095301

**RE;THE LAND ACT NO 4 OF 1999**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF**
**REF NO;MMC/LD/20637**
**REGISTERED OWNER; DONARD NGASSA SOPELA**
**LAND; PLOT NO. 33 BLOCK "N.2" KIWANJA CHA NDEGE**
**MOROGORO MUNICIPALITY**


**APLICANT; DONARD NGASSA SOPELA**

TAKE NOTICE that the ORIGINAL LETTER OF OFFER to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a REPLACEMENT OF THE ORIGINAL LETTER OF OFFER in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days(30) from the date of this pubication.

THE ORIGINAL LETTER OF OFFER is found, should be delivered to the office of the ; Municipal Director, Morogoro Municipal Council,P.o box 166 Morogoro.

115093702

## KUPOTEA KWA CHETI



**Werema M. Matiko** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2812/0029** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2015 katika chule ya Sekondari Mekomariro.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**NYEG/RB/2667/2018**

115094802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo

MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi **No;52/2019**
Ombi la **JARIA HAMISI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **HAMISI MOHAMED MUHANGE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/03/2019.

215094402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 05/03/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamis tarehe 7/3/2019 kampuni ya M.E and Company Ltd itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Lindi kuelekea Mahenge gari hilo lenye namba za usajili:

   **T802 AJN Horse/T 812 AKE Trailer.**

2. Gri hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 22.00**
   **Upana - mita 2.80**
   **Kimo - mita 4.80**
3. Nija itakayotumika Lindi hadi Mahenge kupitia Dar es salaam gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa **12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

115094002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**MAHAKAMA YA MWANZO KIGWE**
**WILAYA YA BAHI**
**MADAI TALAKA NA. 02/2019**
**MDAI RASHID OMARI KILANGO**
**MADAIWA JOYCE TIMOTHEO MRELO**

KWA JOYCE TIMOTHEO MRELO
popote alipo
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya kuachana (Talaka) kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya alhamisi 14/03/2019 saa mbili na nusu asubuhi kwa kujibu Masai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo/ni lazima kuleta mashaidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hiyo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalizi: kama hukuhudhira/bamkuhudhuria siku iliyotajwa hapk juu/ mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shauri ni hiyo/ itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapta ya mahakama hii leo25/2/2019.

215094602


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

0767 223311

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MODRIC:
## Ronaldo gonjwa la Real

**MADRID,** Hispania

LUKA Modric amebainisha kwamba Real Madrid imekuwa na matatizo ya kufunga mabao na wameshindwa kumpata mrithi sahihi wa Cristiano Ronaldo msimu huu.

Real Madrid ikiwa bila Ronaldo ipo nyuma kwa pointi 12 dhidi ya Barcelona kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, baada ya mechi 26, huku mechi zote mbili za El Clasico wakifungwa.

Karim Benzema ndiye mfungaji bora wa Madrid msimu huu hadi sasa akiwa amefunga mabao 11, lakini ana mabao saba kwenye La Liga.

"Kwa kile tunachokifanya hapa, tunamkosa Cristiano," amesema Modric akiiambia BBC Sport.

"Klabu zilimhitaji mchezaji mwingine kwa ajili ya kuziba pengo la Ronaldo, lakini haikuwa kazi rahisi kumpata mrithi wake.

"Cristiano alifunga mabao 50 na huwezi kumpata mtu anayeweza kufunga mabao hayo leo. Wengine tumeweza kujaribu, lakini hatujaweza kufunga mabao 50, ila angalau tumefunga 15, 20, au 10.

"Hili ndilo tatizo kubwa kwetu mwaka huu. Kwa mfano kwenye mchezo dhidi ya Barca tulikuwa na nafasi nyingi, lakini unaposhindwa kufunga unaadhibiwa na timu pinzani."

# Tottenham wajiandaa kurudi uwanja wao

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham baada ya kusubiri kwa muda mrefu, hatimaye wanatarajia kuhamia kwenye uwanja wao mpya, huku wakiwa na matumaini kwamba wameshacheza mchezo wao wa mwisho pale kwenye dimba la Wembley.

Awali ilitarajiwa kwamba, Tottenham wangeanza msimu mpya wa 2018/19 kwa kucheza katika uwanja wao mpya uliokarabatiwa wa White Hart Lane, baada ya kuutumia Uwanja wa Wembley kwa miaka miwili.

Kucheleweshwa kumalizika kwa uwanja huo, kukaifanya Spurs kulazimika kucheza kwenye uwanja huo, lakini sasa habari njema ni kwamba wanarudi kwenye uwanja wao wa zamani, kwa mujibu wa Gazeti la Evening Standard.

Uwanja huo utafunguliwa rasmi kwenye mchezo wa Tottenham dhidi ya Brighton Aprili 7, mwaka huu na pia kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Huddersfield Aprili 13.

Tottenham, ambao sasa wamejikuta wakiwa kwenye wakati mgumu wa kugombea nafasi nne za juu katika Ligi Kuu baada ya kutoka sare ya kufungana 1-1 na Arsenal, wanatumaini watacheza michezo yao ya mwisho ya Ligi Kuu dhidi ya Brighton, Huddersfield, Crystal Palace, West Ham na Everton katika uwanja huo.

Uwanja huo ndio utakuwa mkubwa zaidi katika Jiji la London, huku ukichukua watazamaji 62,062 dhidi ya ule wa Arsenal wa Emirates wenye uwezo wa kuchukua watazamani 60,161.

# CHAMBERLAIN akaribia kurudi dimbani Liver

**LONDON,** England

ALEX Oxlade-Chamberlain (pichani chini), anatarajia kurudi dimbani kucheza mchezo wake wa kwanza kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kuwa nje akiuguza majeraha na kiungo huyo atakichezea kikosi cha Liverpool cha umri chini ya miaka 23, Ijumaa wiki hii.

Kiungo huyo mshambuliaji alikuwa nje ya dimba tangu Aprili mwaka jana, wakati alipoumia kwenye mchezo wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Roma.

Hata hivyo, kurudi kwake kwenye mazoezi na kikosi cha kwanza ni katika wiki za hivi karibuni, Oxlade-Chamberlain sasa ana nafasi ya kucheza kwa mujibu wa Gazeti la Mirror.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, atarudi kwenye mchezo huo wa timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23 dhidi ya Derby.

Gazeti la Mirror limeripoti kwamba mchezaji huyo atatarajiwa kuchezeshwa kwa dakika zote ili kujiimarisha zaidi.

Jurgen Klopp hivi karibuni alisema kwamba, Oxlade-Chamberlain anatarajiwa kurudi uwanjani wakati wowote baada ya kupona kabisa.

Klopp alisema: "Ox anafanya mazoezi kwa asilimia 70. Anafanya mazoezi na wachezeji wenzake.

"Kila mmoja anamtarajia kurudi uwanjani hivi karibuni na ninaimani kwamba atarejea na kuwa fiti."






# LENO:
## Ozil, Mustafi sababu kutua Arsenal

**LONDON,** England

BERND Leno amesema majadiliano na Wajerumani wenzake, Mesut Ozil na Shkrodan Mustafi, yalimshawishi yeye kuhamia katika Klabu ya Arsenal wakati alipopewa nafasi hiyo kipindi cha majira ya joto mwaka jana.

Leno alijiunga na kikosi hicho cha kocha, Unai Emery akitokea Bayer Leverkusen kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 22 Julai mwaka jana, na tangu hapo amejiimarisha mwenyewe kwa 'Washika Bunduki' hao na kumpiku, Petr Cech.

Na Mjerumani huyo sasa amebainisha kwenye tovuti ya Arsenal kwamba kuwajua wachezaji wa klabu hiyo wakiwamo Ozil na Mustafi, ndiko kulikosababisha yeye kutua klabuni hapo.

"Kucheza kwenye Ligi Kuu ya England ilikuwa jambo linalonivutia, na bahati nzuri nilikuwa nawajua wachezaji wachache."

"Nimemjua Mustafi kwa kipindi cha miaka 10 au 11 kwa sababu tumekua pamoja kwenye timu za Taifa za Vijana, chini ya umri wa miaka 17 na 21.

"Nilicheza na Mesut kwenye timu ya taifa pia, na pia nilikuwa nawajua Granit Xhaka, Pierre-Emerick Aubameyang na Henrikh Mkhitaryan kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, nilifurahia pia kuwaona hapa Arsenal.

"Kabla sijfanya maamuzi nilizungumza na Mustafi na Mesut kuhusu hilo. Wote waliniambia Arsenal ni klabu kubwa na wangependa kuniona nikicheza hapa.

"Nilizungumza na kaka yangu, wazazi wangu na mchumba wangu na wote walifurahia mimi kuja kucheza hapa. Niliamua kusajiliwa Arsenal."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alisema kufanya mazoezi na Cech kumemsaidia na anafurahia katika kila dakika.

# CAVANI
## kuikosa United

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inaweza kuwa na wakati mzuri kwenye mchezo wake wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya leo Jumatano dhidi ya PSG, baada ya Edinson Cavani (pichani chini), kuonekana kwamba hatoweza kucheza.

United, ambayo inakabiliwa na majeruhi wengi kwenye kikosi chake, itahitaji kupindua matokeo kwenye mechi hiyo, baada ya mchezo wa kwanza kufungwa mabao 2-0 na PSG katika Uwanja wa Old Trafford.


Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, ambaye aliumia kwenye paja wakati wa mchezo dhidi ya Bordeaux Februari 9, alitarajiwa kurudi dimbani Jumatano, lakini akashindwa na hivyo uwezekano wa kushuka dimbani leo ni mdogo.

Cavani angeweza kukaa benchi, lakini PSG wanatarajiwa kumpumzisha mshambuliaji huyo, wakati wakitaka kuulinda ushindi wao wa kwanza ambapo mabao yake yalifungwa na Presnel Kimpembe na Kylian Mbappe.


Cavani, ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa PSG, ametikisa nyavu mara 17 katika mechi 16 za Ligue 1, huku pia akifunga mabao mawili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Pamoja na kumkosa Cavani, PSG pia hawataweza kumtumia Neymar kwenye mchezo huo, kwani mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil bado anauguza majeraha.

United, inayonolewa na kocha wa muda, Ole Gunnar Solskjaer itawakosa Ander Herrera, Jesse Lingard, Nemanja Matic, Anthony Martial, Juan Mata, Phil Jones, Antonio Valencia na Alexis Sanchez ambao ni majeruhi, huku Paul Pogba akitumikia adhabu ya kadi nyekundu.



# Mourinho amchokonoa Solskjaer



**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, amesema haamini Manchester United inaweza kumpa Ole Gunnar Solskjaer (pichani), nafasi ya kuwa kocha wa kudumu wa klabu hiyo, licha ya kuwa na mafanikio kwa kipindi kifupi alichokaa hapo.

Mourinho alifukuzwa Desemba baada ya kufungwa 3-1 na Liverpool katika dimba la Anfield, na tangu, haijafungwa mchezo wowote chini yake na sasa imerudi kwenye nne bora.

Lakini Mourinho amesema haamini kwamba Solskjaer anafaa kupewa nafasi hiyo, baada ya kuulizwa maamuzi ya Fulham kumchukua Scott Parker kuwa mrithi wa Claudio Ranieri, ambaye atainggoza timu hiyo hadi mwishoni mwa msimu huu.

Aliiambia beIN Sports: "Fulham inaweza kupata kocha bora kuliko Claudio? Hapana.

"Unaweza kulinganisha uzoefu wa Claudio na Scott, ambaye anakinoa kikosi cha kwanza kwa mara ya kwanza? Hapana.

"Lakini kwenye soka unaweza kuwa na mfano mzuri kutoka kwenye klabu yangu ya zamani, kwamba kuna wakati unatakiwa kufanya mabadiliko ya haraka.

"Lakini siamini kwamba mabadiliko haya yanakuwa ya kudumu."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO NJIA PANDA MBIO KIATU SERIE A

**TURIN,** Italia

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo, ambaye yupo kileleni mwa orodha ya wafungaji Serie A huku pia akiongoza kwa pasi za mwisho katika ligi hiyo, anaweza kushuhudia akifunikwa na straika wa Sampdoria, Fabio Quagliarella, wakati huu akiendelea kumvuta shati Mreno huyo.

Sampdoria ilipata ushindi wa mabao 2-1 nyumbani kwa SPAL Jumapili usiku, shukrani kwa mabao mawili ya mapema kutoka mshambuliaji mkongwe, Quagliarella.

Mabao ya Quagliarella, dhidi ya SPAL yanamfanya kucheka na nyavu mara 19 kwenye ligi msimu huu, hivyo kumfikia Ronaldo katika orodha ya wafungaji, lakini nyota huyo wa Ureno anabaki akibebwa zaidi na pasi zake nane za mwisho hadi sasa msimu huu.

Hata hivyo, Quagliarella mwenye umri wa miaka 36 kwa sasa, hayupo mbali kwa upande wa pasi za mwisho kwa kuwa hadi sasa ameshatengeneza mabao sita.

Mbio hizo za ufungaji Serie A, zinafuatiwa kwa karibu na mshambuliaji wa AC Milan, Krzysztof Piatek ambaye yupo karibu akishika nafasi ya tatu nyuma ya wawili hao, akiwa na mabao yake 18.

Mshambuliaji wa zamani wa Real Madrid, Ronaldo alishindwa kuongeza idadi hiyo na kumpiku Quagliarella wakati wakiivaa Napoli na anaweza kujikuta akifunikwa kama atashindwa kuziona nyavu mwishoni mwa wiki hii.

Juventus, kwa upande mwingine iliongeza ukinara wake katika msimamo wa Serie kwa pointi 16 zaidi baada ya kushinda 2-1 nyumbani kwa wapinzani wao, Napoli.

Licha ya kutokuwa katika orodha ya wafungaji kwenye mechi hiyo, Ronaldo alitengeneza vichwa vya habari kwa kile ambacho wengi walidhani amejirusha na kusababisha kipa wa Napoli, Alex Meret, kutolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya 25 ya mchezo.

Refa hakutaka kutumia VAR na hakurudia tukio hilo kabla ya kutoa kadi nyekundu. Kurejea kuangalia tukio hilo kutaonyesha, ukweli hapakuwa na kugusana kati ya wachezaji hao wawili katika nafasi ya kwanza.

Orodha hiyo ya wafungaji huenda ikabadilika mwishoni mwa wiki hii wakati Juventus itakapoivaa Udinese na Sampdoria itakapokabiliana na Atalanta.

## KWA UFUPI

### POGBA, LUKAKU WATIBUANA

WACHEZAJI wa Manchester United, Romelu Lukaku, 25, na Paul Pogba, 25, walitibuana katika chumba cha kubadilishia kufuatia ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Southampton. Tukio hilo lilitokana na straika Mbelgiji Lukaku kunyimwa fursa ya kukamilisha hat-trick kwa mkwaju wa penalti na kiungo Mfaransa Pogba ambaye hata hivyo alikosa tuta hilo. **(Sun)**

### BARCA, MADRID ZASUBIRISHWA

BARCELONA, Real Madrid na Chelsea zitapaswa kusubiri katika mpango wao wa kuwania kumsajili straika wa Eintracht Frankfurt na Serbia, Luka Jovic, 21, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Fredi Bobic. **(Sky Sports - in German)**

### UNITED, PSG KWA SANCHO

MANCHESTER United ipo tayari kutoa upinzani mkali dhidi ya Paris St-Germain katika kuipata saini ya winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, 18, wakati kinda huyo akijiandaa kuwa mchezaji wa kwanza England kuuzwa kwa pauni milioni 100. **(Telegraph)**

### ASENSIO ATEGWA JUVENTUS

JUVENTUS inavutiwa na huduma ya winga wa Real Madrid, Mhispania Marco Asensio, 23, baada ya kusugulishwa benchi Jumamosi kwenye mechi ya El Clasico wakati Barcelona ikiibuka na ushindi. **(Tuttosport - in Italian)**

### SILVA KUPEWA MIAKA SITA

MANCHESTER City inajiandaa kumtunuku kiungo Mreno Bernardo Silva, 24, mkataba mpya wa miaka sita. **(Sky Sports)**

### BUTLAND AIVUTIA PALACE

CRYSTAL Palace inavutiwa na kipa wa Stoke City, Muingereza Jack Butland, 25. **(South London Press)**

### HOLLAND KUMRITHI SARRI

KOCHA msaidizi wa England, Steve Holland, ni mmoja anayepewa nafasi Chelsea kama itaachana na Maurizio Sarri. **(Mail)**

### MASHUSHUSHU ARSENAL WATUA ROMA

ARSENAL inajiandaa kutuma mashushushu Roma kwenda kumchunguza winga Mturuki Cengiz Under, 21, ambaye amerejea kikosini akitokea chumba cha majeruhi. **(Calciomercato - in Italian)**

### PIRES: SARRI HATOBOI MSIMU

NGULI wa zamani wa Arsenal, Robert Pires, anaamini ni "vigumu kuona" kocha wa Chelsea, Maurizio Sarri akiendelea kuwamo Stamford Bridge msimu ujao, na amesema itakuwa ni "habari njema" kama tetesi za Zinedine Zidane kutua EPL zitatimia. **(Bwin)**

### WACHEZAJI UTD WAMTAKA SOLSKJAER

IMANI imejengeka miongoni mwa wachezaji wa Manchester United kuwa kocha wa muda Ole Gunnar Solskjaer atapewa kazi hiyo jumla. **(Telegraph)**

### TIELEMANS KUITOBOA LEICESTER

LEICESTER City itapaswa kulipa pauni milioni 40 kama itamgeukia jumla kiungo Mbelgiji Youri Tielemans, 21, anayeichezea kwa mkopo kutoka Monaco. **(Mail)**

### BAYERN MAWINDONI ARSENAL

BAYERN Munich inamwinda winga kinda wa Arsenal, Xavier Amaechi, 18. **(FootballLondon)**

### SPURS KUMFUATA ETETE

TOTTENHAM inafikiria kwenda kumsajili mshambuliaji kinda wa Notts County, Kion Etete, 17. **(Mail)**

## HABARI MICHEZO

# POPADIC ATOA SIKU TISA KUTIMKA SINGIDA UNITED

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

KOCHA Mkuu wa Singida United, Dragan Popadic, amefunguka kwamba katika kipindi cha siku tisa anatarajia kuvunja mkataba na klabu hiyo na kurejea kwao iwapo uongozi utashindwa kumlipa haki zake zote anazodai.

Akizungumza na mwandishi wetu juzi, Popadic alidai kuwa kutokana na mazingira yaliyopo Singida United kwa sasa, ni vigumu kuiongoza kutokana na viongozi wake wakuu, akiwamo Mwigulu Nchemba na Festo Sanga kuishi jijini Dar-es-Salaam na kuendesha timu hiyo kupitia mawasiliano ya simu.

"Kiongozi pekee aliyepo karibu na timu ni katibu mtendaji ambaye hata hivyo kumekuwapo na changamoto kubwa ya mawasiliano na huyu Festo anapaswa kuwa karibu na timu ili wasaidiane, lakini ameamua kuishi jijini Dar es Salaam," alifafanua.

Alisema kuendelea kuishi mbali na timu hususan katika kipindi cha Ligu Kuu ambayo imejaa ushindani mkubwa, hatakuwa na wala hawatakuwa na msaada kwa timu yao, na kibaya zaidi akadai Sanga hata kama timu yake inapokuwa na mchezo jijini Dar es Salaam, ni nadra kuhudhuria katika mechi.

Akitoa malalamiko zaidi Popadic alianika wazi kwamba kwa mujibu wa mkataba waliosaini, aliahidiwa yeye pamoja na kocha wa viungo, Dusan Momcilovic maarufu kwa jina la Dule, kupatiwa gari kwa ajili ya usafiri, mpishi na mhudumu wa usafi, ahadi ambayo haijatekelezwa mpaka leo.

Aidha, Popadic alibainisha kuwa tangu alipoanza kufanya kazi ya ukocha katika nchi mbalimbali za Afrika ya Kusini na Ulaya, hajawahi kuishi maisha kama hayo anayoishi Singida kwani ni magumu na yanayosikitisha.

"Ilifika wakati hatuna fedha hata za kulipia usafiri wa bajaj kwenda na kurudi Uwanja wa Namfua kwenye mazoezi, kutokana na kutokuwa na uwezo hata wa kununua chakula, tumepewa nyumba nzuri bora, lakini haina mpishi,"aliongea kwa masikitiko makubwa.

Alisema endapo watamlipa fedha zake katika kipindi cha muda aliotoa, ataendelea kufanya kazi na kutumia wasaa huo kuomba uongozi huo kuhakikisha unampa mkataba wa kazi kocha wa viungo, Dusan ili aweze kushirikiana naye katika kukisuka kikosi cha timu hiyo.

Alipotafutwa Meneja wa Singida United, Sanga, alikiri timu hiyo kudaiwa mishahara na makocha hao pamoja na wachezaji, lakini akikanusha kuwa madai ya miezi minane hayana ukweli wowote kama inavyodaiwa, isipokuwa wanadaiwa miezi michache tu.

## Massawe wa Stand akiri Simba kuwazidi

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI na nahodha wa Stand United, Jacob Massawe, amesema kipigo walichokipata Jumapili iliyopita dhidi ya Simba, kimetokana na kuzidiwa mbinu na mabingwa hao watetezi.

Massawe, alisema walikuwa na uhakika mkubwa wa kupata pointi kwenye mchezo huo lakini Simba wapo vizuri na ina wachezaji wenye uzoefu na kilichotokea kwenye mechi hiyo ni kuzidiwa ufundi.

"Mpira ni mchezo wa makosa... unapokosea mwenzako anakuadhibu na hicho ndicho kilichotokea kwetu, Simba walituzidi ujanja," alisema.

Alisema kwa sasa wanaelekeza mkazo wao kwenye michezo inayofuata na watahakikisha wanapambana kupata ushindi.

Katika mchezo huo wa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Kambarage, Stand ilikubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Simba yote yakifungwa na nahodha John Bocco.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 26 | 20 | 4 | 2 | 43 | 17 | 64 |
| 2.Azam | 26 | 15 | 8 | 3 | 36 | 17 | 53 |
| 3.Simba | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4.Kinondoni MC | 28 | 9 | 14 | 5 | 31 | 18 | 41 |
| 5.Lipuli | 29 | 9 | 11 | 9 | 24 | 26 | 38 |
| 6.Alliance | 29 | 9 | 9 | 11 | 23 | 30 | 36 |
| 7.Mbao | 28 | 9 | 9 | 10 | 19 | 26 | 36 |
| 8.Mtibwa Sugar | 26 | 10 | 5 | 11 | 26 | 21 | 35 |
| 9.JKT Tanzania | 28 | 8 | 11 | 9 | 16 | 17 | 35 |
| 10.Mbeya City | 27 | 9 | 7 | 11 | 27 | 29 | 34 |
| 11.Coastal Union | 28 | 7 | 13 | 8 | 26 | 30 | 34 |
| 12.Ruvu Shooting | 29 | 8 | 10 | 11 | 27 | 35 | 34 |
| 13.Kagera Sugar | 27 | 7 | 12 | 8 | 21 | 25 | 33 |
| 14.Mwadui | 29 | 9 | 6 | 14 | 31 | 36 | 33 |
| 15.Stand Utd | 29 | 9 | 6 | 14 | 27 | 37 | 33 |
| 16.Ndanda | 27 | 8 | 9 | 10 | 17 | 27 | 33 |
| 17.TZ Prisons | 28 | 7 | 11 | 10 | 20 | 24 | 32 |
| 18.Singida Utd | 27 | 8 | 8 | 11 | 20 | 26 | 32 |
| 19.Biashara Utd | 27 | 5 | 9 | 13 | 18 | 29 | 24 |
| 20.African Lyon | 28 | 4 | 9 | 15 | 17 | 35 | 21 |



Mmoja kati ya washiriki wa mbio za Kili Marathon, akipatiwa huduma ya kwanza na AAR Healthcare wakati wa mbio hizo zilizofanyika Moshi mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# AAR yapongezwa Kili Marathon 2019

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKATI mbio za Kili Marathon 2019, zikimalizika kwa mafanikio makubwa mwishoni mwa wiki mjini Moshi mkoani Kilimanjaro, Kampuni ya Huduma za Afya nchini, AAR Healthcare, imepongezwa kwa kuwahudumia bure washiriki takriban 4,000 kwenye kinyang'anyiro hicho.

AAR Healthcare ilitoa huduma za uchunguzi wa afya kwa washiriki, kwa upande wa huduma ya kwanza pamoja na huduma ya gari la wagonjwa (standby ambulance service).

Akizungumza baada ya kuwa miongoni mwa waliopata huduma hiyo, Lydia Nasimiyu, mshiriki wa Kili Marathon kutoka Kenya, mbali na kuwapongeza AAR kwa hatua waliyoichukua, alishukuru kwa kuhudumiwa vizuri.

"Ningependa kuwashukuru AAR Healthcare kwa msaada wao wa huduma ya afya walionipa. Kweli nilipata huduma kwa muda. Ninashukuru wamekuwa hapa kuhakikisha washiriki tunapata huduma hii muhimu," alisema Nasimiyu na kusisitiza.

"Ningependa pia kuwapongeza kwa hiki walichokianzisha ili wengine pia waige kwa manufaa ya wote na ninaamini huduma ya matibabu ni muhimu sana kwenye kila mashindano ya mbio (marathon).

Kwa upande wake Meneja wa kampuni hiyo mkoani Arusha, Dk. Aggrey Mapunda, aliwaambia waandishi wa habari kuwa kutokana na uzoefu wao katika ushiriki wa Kili Marathon, wamebaini kuwapo changamoto ya washiriki kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kufanya uchunguzi wa afya zao kabla ya kushiriki, suala ambalo alilielezea kuwa wamelifanyia kazi katika tukio la mwaka huu ili washiriki wawe na uhakika wa afya zao na hivyo kuepukana na madhara wakati wa kushiriki mbio hizo.

"Kitaalamu, washiriki wote wa mbio wanapaswa kuchunguzwa afya zao, na sisi kama kampuni inayotoa huduma bora za afya, tunaamini ni jukumu letu kutoa elimu inayohitajika pamoja na kuwapa huduma hiyo bure ili kuwahamasisha kuwa na utamaduni huo katika maisha yao ya kawaida," alisema Dk. Mapunda na kuongeza: "Tunafahamu kuwa ajali na dharura za aina mbalimbali hutokea katika kipindi kama hiki, na hii ndio sababu imetufanya kutoa huduma ya gari la wagonjwa ambalo liko tayari muda wote kutoa huduma hapa, nalo pia tumelitoa bure."

Mbali na huduma hiyo, AAR Healthcare pia ni moja kati ya wadhamini wakuu wa Kili Marathon, na mwaka huu ni wa pili kwao kudhamini mbizo hizo kwa kutoa huduma.

"Tumekuwa tukifanya kazi na Kili-Marathon tangu mwaka jana kwa lengo la kufikisha kwa usahihi huduma bora za afya kwa watu. Na kwa kuwa sisi ni wadau muhimu kwenye sekta ya afya na michezo, tunaamini kula vizuri na kwa usahihi pamoja na kufanya mazoezi ni kitu bora kwa afya ya kila mmoja wetu. Hivyo, tutaendelea kutoa mchango wetu na kuunga mkono kwa vitendo Kili Marathon kwa ajili ya kuhuisha afya bora," alisema Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa AAR Heathcare, Doscar Massaba.

Takriban watu 9,000 kutoka nchi mbalimbali walijiandikisha kushiriki kwenye Kili Marathn 2019, kwa mujibu wa tovuti ya waratibu wa mashindano hayo.

Michezo
Jumatano Machi 6, 2019
Nipashe

## Ronaldo njia panda mbio Kiatu Serie A



HABARI UK. 30



## Modric: Ronaldo gonjwa la Real

**MADRID,** Hispania

LUKA Modric amebainisha kwamba Real Madrid imekuwa na matatizo ya kufunga mabao na wameshindwa kumpata mrithi sahihi wa Cristiano Ronaldo msimu huu.

INAENDELEA UK 28




## Cavani kuikosa Man United leo

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inaweza kuwa na wakati mzuri kwenye mchezo wake wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya leo Jumatano dhidi ya PSG, baada ya Edinson Cavani kuonekana kwamba hatoweza kucheza.

INAENDELEA UK 29



## Popadic atoa siku tisa Singida United

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

KOCHA Mkuu wa Singida United, Dragan Popadic, amefunguka kwamba katika kipindi cha siku tisa anatarajia kuvunja mkataba na klabu hiyo na kurejea kwao iwapo uongozi utashindwa kumlipa haki zake zote anazodai.

INAENDELEA UK 31

NITATUPIA...



Mshambuliaji wa Manchester United, Romelu Lukaku, akiwa mazoezini kabla ya jana kuelekea Ufaransa, wakati leo akitarajiwa kuongoza safu ya ushambuliaji dhidi ya PSG kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora itakayopigwa katika Uwanja wa Parc des Princes, Ufaransa. **HABARI UK. 29**

# AUSSEMS AJIAMINI SIMBA BILA OKWI

●●● Aachwa Dar na Juuko, Mlipili, Ndemla, Zahera aipa ushindi kwa JS Saoura, aiombea ishinde ili Tanzania...

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya kikosi cha Simba jana jioni kukwea pipa la Shirika la Ndege la Emirates kueleka Algeria bila baadhi ya wachezaji wake nyota, Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema anaamini watashinda katika mchezo wao wa marudiano wa Kundi D dhidi ya wenyeji, JS Saoura, kauli ambayo imeungwa mkono na Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera.

Simba ambayo itashuka dimbani Jumamosi saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, imeondoka na kikosi cha wachezaji 20 huku ikimwacha mshambuliaji wake nyota, Mganda Emmanuel Okwi kutokana na kuwa majeruhi, ambaye amebaki sambamba na Juuko Murushid, Yusuph Mlipili, Said Ndemla na Erasto Nyoni.

Aussems alisema juzi kuwa hana wasiwasi kwa kikosi alichonacho kutokana na kuimarika katika mechi za Ligi Kuu walizocheza na kwamba hatarajii kupoteza kama ambavyo walipoteza mechi mbili za ugenini dhidi ya AS Vita na Al Ahly kwa kufungwa jumla ya mabao 10.

Alisema anatambua kuimarika kwa JS Saoura tangu walipowafunga mechi ya kwanza Uwanja wa Taifa kwa mabao 3-0, lakini hilo halimtii hofu kwa kuwa wamejipanga vema na anaamini watashinda mchezo huo ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutinga robo fainali.

Hata hivyo, wakati Aussems akishuka na mistari hiyo, Zahera, amewapa nafasi kubwa ya kufanya vizuri kwenye kundi lao hilo ambalo linaongozwa na Al Ahly ikiwa na pointi saba moja mbele ya Simba, huku JS Saoura ikishika nafasi ya tatu kwa alama tano na AS Vita ikiburuza mkia kwa pointi nne.

Zahera aliliambia Nipashe jana kuwa Simba ina nafasi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo na kuipa nafasi Tanzania ya kuingiza timu mbili kwenye michuano msimu ujao.

"Wakati Simba walipofungwa mabao 5-0 na AS Vita ya DR Congo, nilisema kama wachezaji wake hawatajengwa kisaikolojia wanaweza wakafungwa na Al Ahly hata kwa idadi kama ile ya Congo na ndicho kilichotokea, lakini nasema Simba hii haiwezi kufungwa kwa idadi ile ya mabao wakiwa Algeria..., uwezo wa kufanya vizuri wanao na kwangu naona Simba wana nafasi ya kusonga mbele," alisema Zahera.

Alisema Simba wakichanga vema karata zao kwenye michezo miwili iliyobaki inawezekana msimu ujao wa michuano hiyo Tanzania ikaingiza timu mbili.

"Mimi nawaombea Simba washinde, Simba wakifika robo fainali ni faida kwa Tanzania..., tutashuhudia timu tatu zikishiriki michuano ya Caf, mbili Ligi ya Mabingwa na moja Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Zahera.

Wakati siku hiyo Simba ikiumana na JS Saoura, Al Ahly itakuwa na shughuli pevu ugenini dhidi ya AS Vita ambayo Machi 19 itafunga hatua ya makundi dhidi ya Wekundu wa Msimbazi hao kwenye Uwanja wa Taifa.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema wamejipanga vema katika mechi hiyo na kwamba wanatarajia msafara wa takriban watu 40 utaungana nao katika safari hiyo ya Algeria.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >